

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 19 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilisha Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

**K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

Na. 263

**Kuvutia Wawekezaji kwenye Viwanda vya  
Kubangua Korosho**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio maalum ili kuvutia Wawekezaji kwenye viwanda vya kubangua korosho?

**MWENYEKITI:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa korosho ni miongoni mwa mazao matano ya kimkakati yanayolimwa hapa nchini, kuanzia mwaka 2018 Serikali inatekeleza mpango wa uhamasishaji wa kilimo cha korosho katika mikoa yote inayostawisha kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, huduma za ugani na pembejeo ili kuimarisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda nchini. Hadi sasa, takribani mikoa 20 inazalisha zao hilo kwa viwango tofauti. Msimu wa mwaka 2020/2021 uzalishaji ulikuwa tani 200,010 na kuipatia nchi kiasi cha shilingi bilioni 477.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya kubangua korosho, Serikali imeweka vivutio mbalimbali vikiwemo vivutio visivyo vya kikodi kama vile kuweka mfumo wa soko la awali kwa wabanguaji wa ndani kuanzia mwaka 2020 kwa lengo la kuwawezesha kununua korosho bila kushindana na wanunuzi wanaosafirisha korosho ghafi kwenda masoko ya nje ya nchi na kuwahakikishia malighafi kwa bei nafuu. Katika mnada huo jumla ya tani 2,021.7 kimenunuliwa na viwanda tisa vilivyoshiriki soko hilo la awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka pia vivutio vya kikodi kwa viwanda vya kubangua korosho kupitia Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje Sura 373 ikiwemo: Msamaha wa Kodi ya Makampuni (*Corporate Tax*) kwa miaka 10; msamaha wa asilimia 100 wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kwa bidhaa za mtaji (*capital goods*); msamaha wa asilimia 100 wa Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*); na riba ya mikopo kutoka nje; pango na gawio; na msamaha wa asilimia 100 wa Kodi ya Ushuru wa Forodha kwa mitambo na vifaa. Kupitia utaratibu huo, jumla ya viwanda vitano vimesajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji kwa Mauzo Nje (*EPZA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kubuni na kuweka vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyo vya kikodi ili kuvutia zaidi uwekezaji ikiwemo kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda kwenye Halmashauri zinazolima korosho hapa nchini, ambapo maeneo hayo yatakuwa na huduma muhimu kama vile umeme, maji na barabara; na

kupitia kodi mbalimbali zinazotozwa katika mitambo, vipuri na vifungashio.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa utaratibu huu wa mfumo wa soko la awali huwa unawakutanisha wenye viwanda na wakulima lakini hauna ushindani kwa sababu bei ni ndogo na wakulima hawavutiwi kupeleka korosho zao kama ilivyo kwenye minada mingine ya kawaida, kwa sababu wakulima wanaona kama ni kangomba ya aina fulani tu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *top up* kwa bei ile inayotolewa na wawekezaji ili kuhakikisha kwamba wawekezaji hawa wanapata korosho katika soko?

Swali la pili, kwa kuwa viwanda hivi vimeajiri vijana wengi na akina mama wengi; na kwa sasa hivi viwanda takriban vyote vinafanya kazi chini ya uwezo wake kwa sababu ya changamoto mbalimbali ikiwemo ukosekanaji wa malighafi kwa sababu hawapati korosho mnadani: Je, Serikali inatoa kauli gani sasa kwa wawekezaji ambao wameshafungua viwanda nchini na wale ambao wanatarajia kufungua viwanda vipya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa korosho kwa sababu wakulima hawana imani na mfumo wa soko la awali, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Chikota kwamba kwa sababu ndiyo mfumo umeanza, Serikali itaendelea kuchukua jitihada kuboresha ili kuweza kuvutia wakulima waone kwamba ile siyo kangomba, bali ni soko ambalo lipo lenye lengo la kuhakikisha kwamba viwanda vya ndani vinapata korosho kwanza kabla havijauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto hiyo aliyozungumzia kwamba ajira zile hazizalishwi kwa sababu viwanda havipati korosho, naomba nimhakikishie kwamba katika utaratibu huo huo wa kushughulikia changamoto ambazo zipo katika soko la awali, Serikali itaendelea kufikiria namna bora ya kuhakikisha kwamba korosho inapatikana ili viwanda hivi na vingine ambavyo tunategemea kuvutia viwezwe kuanzishwa, viweze kutoa ajira kwa ajili ya vijana wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Grace Tendega.

Na. 264

**Ukosefu wa Huduma za Bure kwa Wazee,  
Watoto na Wajawazito**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto ya huduma za Afya katika Zahanati zetu hasa ukosefu wa dawa pamoja na huduma bure kwa wazee, watoto na akinamama wajawazito.

Je, ni lini Serikali itahakikisha Sera ya Afya inatekelezwa bila tatizo lolote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea

huduma za afya nchini kwa kuongeza bajeti ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba kutoka shilingi bilioni 31 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi bilioni 270 katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hilo la fedha limewezesha kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu (*tracer medicine*) kutoka wastani wa asilimia 31 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 90 kufikia Aprili 30, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2021 Serikali imetoa huduma ya matibabu bila malipo yenye gharama ya shilingi bilioni 30.1 kwa wananchi wa makundi maalum milioni 12 ikijumlisha wazee, wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi, bado kuna changamoto ya upatikanaji wa baadhi ya dawa za makundi maalum kama wazee, wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, mwezi Novemba, 2020 Serikali ilitoa shilingi bilioni 41.2, mwezi Februari, 2021 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 18.2 katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi kwa ajili ya ununuzi wa dawa na mwezi Mei, 2021 Serikali imepeleka shilingi bilioni 80 na kufanya jumla ya fedha zote zilizopelekwa kwa ajili ya dawa kufikia shilingi bilioni 140.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya ili kuboresha huduma kwa makundi maalum na wananchi kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tumekuwa tunaongeza bajeti ya dawa katika Serikali yetu na tumekuwa tukiona bado zahanati na vituo vya afya havipati dawa. Swali langu: Je, mmefanya utafiti gani wa kuhakikisha kwamba hizo

fedha, shilingi bilioni 270 na hiyo shilingi bilioni 140 ndizo zitakwenda kutatua changamoto ya dawa katika zahanati zetu na vituo vya afya?

Swali langu la pili; hivi tunavyozungumza wananchi wenye changamoto hizi wa kutoka Jimbo la Kalenga na wengine wengi wanaangalia; je, wananchi wategemee nini kuwa hizi dawa katika zahanati na vituo vya afya itakuwa ni historia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Grace Victor Tendega ametangulia kusema, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vitandanishi na vifaa tiba kwa takriban mara tisa ndani ya miaka mitano na hii ni kwa sababu Serikali inajali sana wananchi na inahitaji kuona wananchi wanapata dawa za kutosha ili kuhakikisha kwamba huduma za afya ni bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ni kweli kwamba bado tuna changamoto ya uhitaji wa dawa na Serikali inatambua kwamba bado tuna kazi ya kufanya kuhakikisha tunaendelea kupunguza sana upungufu wa baadhi ya dawa katika vituo vyetu vya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza namna ambavyo Serikali imepeleka fedha mpaka sasa, zaidi ya shilingi bilioni 140 zimepelekwa katika vituo vyetu na mpaka mwisho wa mwaka huu wa fedha, ifikapo Juni, tutakuwa tumepeleka fedha zaidi kuhakikisha tunaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa katika vituo hivyo na kwa makundi maalum na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimhakikishie kwamba Serikali imefanya tathmini kwamba kadri inavyoongeza fedha

ndivyo upungufu wa dawa unavyopungua na ndiyo maana lengo la Serikali ni kuendelea kuongeza fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa dawa na kuondoa kabisa upungufu wa dawa katika vituo vyetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana. Kusema kweli Serikali imetenga fedha nyingi. Kwenye Jimbo letu la Vunjo Kata 16 hakuna kituo cha afya cha Serikali isipokuwa vituo vikongwe, vichakavu vya Mwika, *OPD* Himo na Kiruavunjo. Ni chakavu hata havistahili kuitwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atueleze ni lini watakarabati vituo hivi na kuviinua hadhi ili viweze kuwa vituo vya afya vinavyotumika na watu wa Vunjo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunatambua sana kwamba katika Jimbo la Vunjo kuna upungufu mkubwa wa vituo vya afya lakini hata vile vituo vya afya ambavyo vipo, vina uchakavu kwa sababu ni vya siku nyingi. Ndiyo maana katika mpango wetu ambao tumeuwasilisha na bajeti yetu ya mwaka 2021/2022 tumeweka kipaumbele kwanza cha kwenda kuhakikisha tunajenga vituo vya afya 211 katika maeneo ambayo hayana vituo vya afya.

Pili, kuhakikisha tunaweka mpango wa kwenda kukarabati na kupandisha hadhi vile vituo ambavyo vina sifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kimei kwamba Jimbo la Vunjo pia litapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi vituo hivyo vya afya. (*Makofi*)



**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 265

**Hitaji la Vifaa vya Maabara za Sekondari  
Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaweka vifaa vya maabara kwenye maabara zote za Shule za Sekondari katika Wilaya ya Mkalama zilizojengwa kwa nguvu za wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ina jumla ya shule 20 za Sekondari ambapo 19 kati ya hizo ni shule za Serikali. Usambazaji wa vifaa vya maabara mashuleni huzingatia ukamilishaji wa vyumba vya maabara katika shule husika. Hadi Machi, 2021, Serikali imepeleka vifaa vya maabara kwenye shule 18 kati ya shule 19 za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shule ya sekondari Kikhonda haijapelekewa vifaa kwa sababu haina vyumba vya maabara. Hata hivyo, Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Kikhonda wameanza taratibu za ujenzi wa maabara katika shule hiyo ili ujenzi utakapokamilika iweze kuingizwa kwenye mpango wa kupatiwa vifaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imepeleka vifaa vya maabara kwenye shule 18 kati ya 19: Je, sasa wana kauli gani kuhusu kupeleka walimu wa kutosha wa sayansi katika huu mgao unaokuja wa walimu ili vifaa hivi viweze kuwatendea haki wanafunzi wetu wa Mkalama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Wilaya ya Mkalama ina *High School* moja tu na ambayo iko kwenye mchepuo wa Sanaa: Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kuongeza *hostel* katika Sekondari ya Gunda ambayo sasa wana *hostel* moja ili angalau sasa tuweze kuanzisha mchepuo wa sayansi katika sekondari hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tunapokea pongezi ambazo amezitoa kwa sababu, Serikali imefanya kazi nzuri katika jimbo lake na Halmashauri yake ya Mkalama kwa kupeleka vifaa vya maabara katika sekondari 18 kati ya 19 za jimbo lake. Swali lake la msingi ambalo ameiliza ameuliza tu ni lini Serikali itapeleka Walimu wa Sayansi wa kutosha katika shule hizo zenye maabara, ili angalau sasa pamoja na vifaa basi pawepo na basi pawepo na Walimu wa kutosha kwenye huo mgawo unafuatia. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea ombi lake na tutazingatia wakati wa mgawanyo ambao tutautoa hivi karibuni kabla ya mwisho wa mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ameomba tujenge *hostel* ya Sekondari ya Dunga ili angalau na wao

waweze kupata kidato cha tano na cha sita. Niseme tu ombi lake limepokelewa na tutalifanyia kazi kulingana na mahitaji ya jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika baadhi ya shule zetu za sekondari zilizoanzishwa kabla ya Serikali kuweka mkazo kwamba, lazima shule kabla haijasajiliwa iwe na maabara, kuna shule chache zimebaki zikiwa hazina maabara kabisa kama Shule ya Flamingo iliyoko katika Wilaya ya Longido, Tarafa ya Ketumbeine, Kata ya Meirugoi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha, ili kila shule ya kata iwe na maabara ukizingatia kwamba, sayansi ni muhimu? Pia wananchi wanajitahidi kuchanga, lakini bajeti ya TAMISEMI imetoa 25,000/= tu kama umaliziaji wa maabara ambazo zimeshafikia hatua ya juu; hii ambayo haina kabisa Serikali ina mpango gani kutusaidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu upi niseme ni mkakati wa Serikali wa kuhakikisha katika zile shule zote, yaani ikiwemo Shule yake ya Flamingo iliyopo katika jimbo lake, ambazo hazina maabara tunazikamilisha. Moja ya mpango wetu na ndio maana katika bajeti mtaona kabisa tumetenga fedha, moja kwa ajili ya kuhakikisha tunamalizia maabara zote ambazo wananchi walikuwa wamezianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumezitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha katika yale maeneo ambayo kuna

shule za sekondari za kata ambazo hazina maabara zinaanzisha ujenzi, ili sisi tuweze kuongezea fedha. Kwa hiyo, moja ya huo mkakati ni pamoja na kumaliza katika sekondari ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, nimhakikishie kabisa kwamba, hata hiyo Sekondari ya Flamingo itakuwa na maabara, tutapeleka vifaa na watoto watasoma sayansi kwa vitendo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Singula, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba Mheshimiwa Vuma.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mheshimiwa Vuma kwa niaba ya Mheshimiwa Sylvia. Naomba sasa swali langu lipatiwe majibu.

Na. 266

### **Mkakati wa *Taifa Stars* Kufanya Vizuri**

**MHE. VUMA A. HOLLE K.n.y. MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, nini Mpango wa Serikali kuhakikisha kuwa Timu ya Taifa Stars inafanya vizuri katika Michezo ya Kimataifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Timu za Taifa ikiwemo *Taifa Stars* zinafanya vizuri katika mashindano mbalimbali, kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imeendelea kuboresha maandalizi ya timu zetu kwa kutenga fedha za kuzihudumia timu hizi. Mipango mingine iliyowekwa

na Serikali ni ile ya muda mrefu na muda mfupi. Mipango ya muda mfupi ni pamoja na:-

(a) Kushirikiana na *TFF* katika maandalizi ya kambi za Timu ya Taifa ndani na nje ya nchi.

(b) Kuongeza motisha kwa kutoa posho na bonasi kwa wachezaji na benchi la ufundi la Timu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya muda mrefu ni pamoja na:-

(a) Kuwekeza katika michezo ya UMITASHUMTA, UMISSETA.

(b) Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo nchini.

(c) Mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara yetu na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha fedha hizi zinatengwa.

(d) Kuanzisha shule maalum za michezo katika kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine ya Serikali iliyopo ni ushirikiano kati ya Wizara yangu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya TAMISEMI juu ya uendeshaji bora wa michezo nchini na mipango ya uanzishaji wa tahasusi za kidato cha Tano zenye somo la michezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa uvumbuzi wa vipaji, lakini pia na uendelezaji wa vipaji unapaswa kuanzia ngazi ya chini kabla ya kufika kwenye *National level* hasa kwenye shule zetu za sekondari, vyuo na huko halmashauri kwa ujumla. Je, Serikali haioni haja kwamba inapaswa kutenga fedha za kutosha

kwenye bajeti yake ili kuendeleza vipaji vya michezo mashuleni, vyuoni na huko chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; tumesikia kwamba, Serikali imeanzisha *combination* za elimu ya michezo (*physical education*). Nataka kujua utekelezaji wa jambo hili umefikia wapi mpaka sasa? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge maana yeye ni mdau mkubwa wa michezo, lakini pia niwapongeze Wabunge wote pamoja na Waheshimiwa Madiwani katika halmashauri zao kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakishirikiana na Wizara hii kwa suala zima la michezo. Swali lake la kwanza alitaka kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha michezo katika ngazi za chini inapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la muhimu sana. Sisi kama Wizara nimesema tangu mwaka 2019/2020 tumeanza, lakini nitoe rai sasa kwa Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wabunge katika ngazi za halmashauri, fedha za michezo zitengwe. Kwa hali ilivyo sasa ni Madiwani na baadhi ya wadau wanahangaika na hili suala, lakini halmashauri zetu zitenge fungu chini ya Idara ya Elimu Msingi kwa ajili ya kuhakikisha michezo inadumishwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili alitaka kufahamu mkakati tulionao wa Wizara kuanzisha hizi *combinations* za michezo kwa *A Level* zimefikia hatua gani. naomba nimjulisha Mheshimiwa Vuma kwamba, Kamati ilishaundwa kati ya Wizara ya Elimu, Wizara ya Michezo pamoja na TAMISEMI na ipo *site* ikitembelea zile shule 56 za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati hiyo kuleta majibu maana yake tunaendelea na zile shule ambazo tumeshazitambua ikiwemo Shule za Kibiti, Mpwapwa na Makambako ili kuanzisha sasa hii *combination* na tupate *network* kuanzia msingi mpaka vyuo vikuu. Endapo kazi hii itakuwa imekamilika itasaidia sana kutoa mafunzo kwa vijana wetu kuhusu masuala ya michezo. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Nafahamu nchi inatambua kwamba, tarehe 22 kutakuwa na mchezo mkubwa ambao unaweza ukabeba *record* ya nchi wa *Simba Sports Club* na *Kaiza Chiefs* hapa Dar es Salaam. Nataka niulize kwa sababu, mchezo huu unaenda kubeba mafanikio ya timu karibu nne endapo Simba itafuzu, Yanga na timu nyingine. Je, ni mkakati upi wa Serikali wa makusudi kuhakikisha *Simba Sports Club* tarehe 22 inashinda na mashabiki wanajaa uwanjani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nikupongeze Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuchaguliwa na kurudi kwenye Kiti chako, unatosha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi. Sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumekuwa tukisema timu inaposhinda na kuiwakilisha nchi yetu inakuwa ni timu ya Taifa. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuipongeza *Simba Sports Club* kwa hatua waliyofikia na nitoe wito kwa Watanzania wote kuhakikisha tunaiunga mkono timu ya *Simba Sports Club* ili *match* itakayoicheza tarehe 22 waweze kupata ushindi. Ushindi huo utakuwa ni heshima kwa nchi yetu. Kwa hiyo,

tunawatakia heri *Simba Sports Club* na sisi Serikali tuko pamoja nao pamoja na vilabu vyote nchini kwa manufaa ya maendeleo ya michezo nchini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Yatoke moyoni hayo. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki.

Na. 267

### **Ujenzi wa Barabara ya Maswa – Lalago**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Maswa hadi Lalago?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanlaus Haroun Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Maswa – Lalago yenye urefu wa kilometa 34 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Barabara hii ni sehemu ya Mradi wa *Serengeti Southern by-pass* ikianzia Maswa – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti hadi Karatu yenye urefu wa kilometa 338. Mradi huu ulihusisha kazi ya Upembuzi Yakunifu chini ya ufadhili wa Serikali ya Ujerumani na umeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza usanifu wa kina na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kupitia



Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali sehemu hii ya Maswa – Lalago na inapitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza, ni jepesi tu; ni lini ujenzi unaanza, basi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kama Serikali ya Ujerumani imeweza kutoa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, inakuwaje Serikali inasuasua kutoa fedha kwa ajili ya usanifu wa kina? Hivi hata hao wanatoa fedha za ufadhili katika hatua hizi za awali hatuoni kama tunawa-*discourage* kwa kitendo cha Serikali kusuasua kutoa fedha za kuendeleza mradi huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimesema barabara hii itaanza mara fedha itakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie katika swali lake la pili, kuhusu kwamba Serikali inasuasua. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi hii Barabara inapita Maswa – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Hydrom – Mbulu – Karatu. Katika baadhi ya barabara, hii tayari kama mlivyosikia jana kwenye bajeti, kipande cha Mbulu – Haidom kitaanza kujengwa. Pia Mheshimiwa Waziri jana amesema barabara hii itatangazwa siku za karibuni ambayo ni sehemu ya hii barabara kwa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata hicho kipande ambacho sasa tutafanya ni *design and build*, yaani ni kufanya usanifu na ujenzi, basi hela ikipatikana hata kipande hiki cha Lalago – Maswa kitajengwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Changamoto zilizoko Maswa Mashariki kuhusu barabara zinafanana sana na changamoto ambazo ziko Arumeru Mashariki. Kuna barabara inayoanzia Tengeru kwenda Mererani, inaunganisha Mkoa wa Arusha na Manyara, lakini pia ni kiungo muhimu kwa shughuli za uchimbaji Mererani na soko ambalo liko Mjini Arusha. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii ni muhimu sana na Mheshimiwa Pallangyo amekuwa akiifuatilia sana, lakini bado tunasema nia ya Serikali ni kujenga hizi barabara ambazo zimeainishwa na zinarahisisha maisha ya wananchi kama zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Pallangyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha na fedha ikipatikana basi hii Barabara ya Tengeru kwenda Mererani, sehemu ambayo kuna machimbo ya *tanzanite* itajengwa ili kuweza kuboresha maisha na kupandisha uchumi, lakini pia kurahisisha biashara ya *tanzanite* kule Arusha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa ahsante. Mheshimiwa Oran Manase, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 268

## Ujenzi wa Barabara ya Mbalizi – Shigamba

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Shigamba kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mbalizi – Shigamba yenye urefu wa kilometa 52.2 ni barabara ya mkoa inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Songwe kupitia Wilaya ya Mbeya Vijijini na Wilaya ya Ilege. Barabara hii ni ya changarawe na udongo ambayo hupita sehemu zenye miinuko na miteremko mikali, hivyo kupitika kwa shida wakati wa mvua kutokana na utelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa katika Kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2020, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alipokuwa akiongea na wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi aliahidi kujenga Barabara ya Mbalizi – Shigamba kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, utekelezaji wa ahadi za Viongozi, ikiwemo ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Mbalizi – Shigamba hufanyika kwa awamu kulingana na upatikanji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inatafuta fedha ili kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo ili ijengwe kwa kiwango cha lami. Wakati

Serikali inatafuta fedha za kuanza taratibu za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pia nashukuru sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na hata pacha wake kwenye Wizara hiyo, wanaifahamu sana jografia ya Wilaya ya Mbeya na hasa Mbalizi. Swali la kwanza, ahadi nyingi zimetolewa, hata wewe utakumbuka kuwa, eneo la miteremko ya Iwambi – Mbalizi lina ajali nyingi na zinaendelea. Mheshimiwa Rais wa sasa tarehe 15 alipotembelea na kuwapa pole wananchi wa Mbalizi kwa ajali mbaya iliyoua watu zaidi ya 20, aliahidi ujenzi wa Barabara ya *By-pass* ya Uyole – Songwe na *By-pass* ya Mbalizi – Iwambi. Sasa ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; bandari kwa muda mrefu walitwaa eneo la Inyala kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Kavu, lakini kwa miaka mingi sasa hawajaweza kuwalipa wananchi na wananchi hawafanyi shughuli zozote za uzalishaji. Sasa ni lini Wizara itaipa nafasi na kuiamuru Mamlaka ya Bandari walipe fidia kwa wananchi wa Inyala, Mbeya? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais, Mama Samia, alipita katika eneo ambalo ametaja na akatoa maelekezo. Bahati nzuri tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha

bajeti yetu jana na miongoni mwa fedha ambazo zimetengwa ni pamoja na malipo ya Barabara hii ya *By-pass* pale Uyole – Songwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na amani tutakapoanza utekelezaji wa bajeti hii hili eneo tutazingatia maelekezo ya kiongozi mkuu wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, anazungumza habari ya fidia ya Bandari Kavu, Inyala. Miongoni mwa maeneo muhimu ambayo tumepanga kujenga Bandari Kavu ni pamoja na Inyala, ambayo itahudumia ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. Kwa hiyo, kwa sababu anasema kwamba, kuna shida pia ya mawasiliano naomba nimhakikishie kwamba, shida hiyo itamalizika fidia iweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane baada ya maswali na majibu tuongee na Mheshimiwa Mbunge tupate *exactly* hasa malalamiko yako wapi, ili utekelezaji wa jambo hili ufanyike, wananchi walipwe fidia zao, wafanye shughuli za maendeleo, lakini pia bandari hii ijengwe na Serikali iweze kumiliki eneo hili ili na kupunguza migogoro kati ya wananchi na Serikali yao pendwa ya Chama Cha Mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daniel Awack, jandae Mheshimiwa Getere.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye majibu ya Waziri, Barabara hii ya Karatu – Mbulu – Haidom – Sibiti, lakini kwenye Ilani kuna barabara hii ya Lalago – Mwanhuzi – Kolandoto – Matala – Karatu. Sasa kwenye majibu ya Waziri amesema kilometa 25 kupitia Barabara ya Karatu – Mbulu, sasa ni lini Barabara ya Lalago – Kolandoto – Mwanhuzi – Matala – Karatu itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Majibu, yeye anataka kujua ni lini tusianze kuzunguka sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara zote mbili ambazo amezitaja ziko kwenye bajeti lakini pia zinajengwa kwa awamu kwa Kulandoto na maeneo mengine ambayo yametajwa tutaenda hatua kwa hatua kadri ambavyo tutapata fedha. Lakini bahati nzuri kwamba ipo kwenye bajeti, pia vipande baadhi vimeanza kujengwa kwa mwaka wa fedha huu ambao unaendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, barabara ya kutoka Makutano, Butiama Nyamswa na Sanzati ni barabara imejengwa kwa muda mrefu sana mkataba wake ulikuwa miaka miwili sasa ni miaka minane toka imeanza kujengwa kama ni bajeti ilikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 46 sasa inaenda mpaka Bilioni 50 ni lini sasa hiyo barabara itakamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI – (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hii imechukua muda mrefu ni miongoni mwa miradi ya barabara ambayo ilikuwa na mkwamo na Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba changamoto zimetatuliwa barabara inaendelea kujengwa na kazi itakwisha matarajio mwaka huu kabla haujakwisha hadi mwaka ujao itakuwa imeshakamilika barabara hii, na tumepanga baada ya Bunge kukamilika tutaenda kutembelea barabara ile ili kuona hali halisi katika eneo la ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Martha Festo Mariki Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 269

### **Kuitangaza Hifadhi ya Taifa Katavi**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa Katavi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Katavi ili iweze kupata watalii wengi na kuongeza mapato. Aidha, Hifadhi ya Taifa Katavi imekuwa ikitangazwa kupitia vyombo vya habari vilivyomo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Katavi iliandaa Mpango Mkakati wa Kukuza Utalii kwa Mkoa wa Katavi mwaka 2019 ambao umesaidia kwa kiwango kikubwa kuitangaza Hifadhi ya hiyo na mikakati mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na Kuitangaza vivutio vilivyomo ndani ya hifadhi ikiwa ni pamoja na wingi wa Viboko, Simba na Twiga weupe. Vilevile Wizara ina mkakati wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa Katavi kupitia tovuti na mitandao ya Kijamii yaani *Instagram*, *Facebook* na *Twitter* lakini pia kuimarisha miundombinu ya barabara ndani ya Hifadhi husika ili kurahisisha kufikika kwa maeneo ya vivutio ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuitangaza Hifadhi hii kupitia chaneli maalum ya Tanzania Safari *Channel*, lakini pia kusimika mabango kwenye mkoa ya jirani kama vile Mbeya, Songwe, Tabora na Kigoma. Serikali pia inaandaa safari za mafunzo kwa wanahabari, mawakala na wadau mbalimbali wa utalii kwa lengo la kuwapa fursa ya kuvielewa vivutio vya utalii na kuvitangaza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine ni pamoja na kujenga sehemu ya malazi ya bei nafuu kwa ajili ya wageni wa ndani na nje ya nchi, na pia kuandaa video au filamu na machapisho mbalimbali na kuyasambaza kwa wananchi na mabasi ili kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Katavi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzitangaza Hifadhi za Taifa kupitia maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ili kuwezesha kupata wawekezaji na watalii. Ni imani ya Serikali kwamba jitihada zinazoendelea kufanywa za kutangaza vivutio hivyo katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi zitaendelea kuzaa matunda na hivyo kuwapatia wananchi wa Katavi na Taifa kwa ujumla manufaa stahiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza naanza kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa kuitangaza hifadhi yetu ya Taifa ya Katavi lakini nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali la kwanza ilikuwa ni ahadi ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, mwaka 2019 ya kujenga hoteli ya Kitalii katika Mkoa wa Katavi katika Kata ya Magamba, ili hoteli hiyo iweze kuwavutia zaidi watalii kwa kupata malazi yaliyo bora na malazi yanayoridhisha. Je, huo mpango wa kujenga Hoteli ya kitalii katika Kata ya Magamba ambapo tulishatenga eneo umefikia wapi Ukizingatia hoteli hii itakwenda kuibua fursa nyingi kwa vijana wanaozunguka katika Mkoa wa Katavi kuweza kuapta ajira? *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili vijiji vinavyozunguka hifadhi ya Taifa ya Katavi vikiwepo vijiji vya Mwamapuri, Chamalindi, Ikuba, Starike, Mangimoto, na Kibaoni vijiji hivi kwa muda mrefu vimekuwa havinufaiki na ujirani mwema kwa kupata miradi ya maendeleo kupitia TANAPA. Je, Serikali inatoa tamko gani ili vijiji hivi viweze kunufaika na hifadhi hiyo ukizingatia vijiji hivyo ndivyo vinavyotunza hifadhi hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Maliki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la hoteli ya kitalii kujengwa katika hifadhi ya Katavi ni kweli Hayati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, aliahidi katika ziara zake kwamba kujengwe hoteli ya kitalii katika hifadhi ya Taifa ya Katavi. Mpango huo umeshapangwa na kwenye mpango wa bajeti wa mwaka 2021/2022 mpango huu tumeuweka na hoteli hii ya kitaifa itanza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu ujirani mwema, ujirani mwema ni kweli Serikali imekuwa ikisaidia vijiji vyote vinavyozunguka maeneo ya hifadhi ikiwemo hifadhi ya Taifa ya Katavi lakini kwa mwaka wa fedha 2021 tulikuwa na changamoto ya Korona hivyo tulishindwa kuhudumia haya maeneo ya hifadhi kama ambavyo Serikali imekuwa ikipanga. Lakini nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili sasa tunaenda kulitekeleza katika mpango wa fedha wa mwaka 2021/2022 vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi za Taifa, ujirani mwema utaenda kutekelezwa kwa kiwango cha juu, ahsante, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Asia Halamga,

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Serikali ina mpango gani

wa kuutangaza utalii wa ndani kwa kutumia Wabunge pamoja na Halmashauri zetu? Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali zuri fupi, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi na wewe.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimpongeze Mheshimia Asia kwa swali lake hilo zuri pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkakati kabisa wa kushirikiana na Halmashauri zote na Serikali za Mikoa na Wilaya katika kutangaza Utalii ikiwemo kuwatumia Wabunge pia katika kutangaza utalii. Ni wazi umeona tayari Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na baadhi ya Wabunge tumeshaanza kushirikiana nao kuhakikisha kwamba tunatangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongezea kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli yalikuwa ni kwamba tupunguze gharama za utalii ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi na watalii wengi zaidi kwenda kwenye sehemu za vivutio vya Utalii, zoezi hili tumeshalianza tunaamini gharama hizo zitashuka na Watanzania waweze kufaidi maliasili zao. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca jandae Kakoso.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kwa kuwa utalii unakwenda kwa *package* na mbuga ya Katavi pamoja na hifadhi nyingine ni sehemu ya utalii kusini na kituo cha utangazaji na taarifa zote kinatakiwa kujengwa lringa katika sehemu inayoitwa Kisekiroro ni lini Serikali itaanza ujenzi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo hicho unafadhiliwa na Benki ya Dunia katika Mradi wa *RIGRO*. Mradi huo ulichelewa kidogo kutokana na tatizo la *COVID* ambalo liliwakuta nchi mbalimbali ikiwemo wafadhili wa Mradi huo. Sasa hivi tayari mradi huo umeshaanza, jana Katibu Mkuu amekabidhi magari 12 kutokana na mradi huo kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Jesca na Wabunge wote wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini kwamba kituo hicho kitajengwa haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, Jiandae Bulaya.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana Mheshimiwa Rais alipokuja Mkoa wa Katavi aliagiza Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ardhi kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi kati ya mapori ya akiba na hifadhi ya Taifa ya Katavi. Lakini utekelezaji mpaka sasa bado haujafanyika ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja Mkoa wa Katavi ili asimamie zoezi hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sasa unamtaka Naibu au Waziri mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Katavi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili Tukufu tutaongozana naye kwenda kutatua taizo hili kwa hiyo nimuondoe wasiwasi tutaondoka naye, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Aya. Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Ni dhahiri kwamba kwa Afrika nchi yetu inahifadhi nzuri inawanyama wengi ukienda Ruaha ukienda Serengeti, Ukienda Tarangire na maeneo mengine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya ukipewa swali la nyongeza usianza na utalam mwingi nenda *straight to the question*.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mikakati ya Serikali ni ile ile ya kushiriki matamasha ya Kimataifa, kutangaza kwenye TV lakini bado hayajatuletea manufaa chanya ya ongezeko la watalii kulingana na vivutio vyetu na hifadhi zetu.

Je, hamuoni kwamba ni wakati muafaka wa kuwa na mikakati Madhubuti ya kiushindani ili idadi ya watalii iendane na hifadhi zetu na vivutio vyetu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimshukuru Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake hilo, takwimu zetu zimeonesha kwamba idadi ya watalii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Ongezeko hilo limetokana na juhudi ya Serikali ambayo imeifanya katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeelekeza wazi kwamba tuje na mazao mapya na mikakati mipya katika kutangaza utalii, mikakati yote ipo mezani iko tayari kinachotukwamisha ni gonjwa hili la *Covid*, nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya pindi ugonjwa huu utakapokwisha ataona ongezeko kubwa la watalii hapa Tanzania, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe Mbunge wa Kibiti.

Na. 270

**Serikali kuruhusu Uvuvi wa Kamba Koche**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa kuwaruhusu Wavuvi wa Kamba Koche kuvua kuanzia mwezi Desemba hadi Julai kila mwaka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Meshimiwa Mweyekiti, kwa niaba wa Waziri ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpmembenwe Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2009 na Marekebisho yake ya mwaka 2020, Serikali haijawahi kuzuia uvuvi wa Kamba Koche au maarufu kama *prawns*. Hata hivyo, Serikali imeweka utaratibu kwa ajili ya uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa Kambamiti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo unaruhusiwa kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Septemba kila mwaka kwa ukanda wa Kaskazini unaohusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani Chalinze na kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti kila mwaka kwa ukanda wa Kusini unaohusisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichobaki kimeachwa ili Kambamiti kwa maana ya *prawns* waweze kuzaliana na kukua. Maamuzi haya yamefanyika baada ya taarifa za utafiti wa Kisayansi na kwa kuzingatia uendelevu wa Rasilimali hii.

Meshimiwa Mweyekiti, Serikali imekuwa ikisisitiza kwa wadau wote wa Uvuvi hususani Uvuvi wa Kambamiti yaana *Prawns* kufanya shughuli zao kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu kwa maslahi mapana ya vizazi vilivyopo na vile vijavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nimpungeze kwasababu Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtaalam sana katika mambo ya uvuvi na ni imani yangu kwamba majibu yake yamesikilizwa kwa makini na watu wa Mkuranga pamoja na Kibiti. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kibiti hasa katika maeneo ya Delta kuna kata kama tano kuna Kata ya Kihongoroni, Kata ya Mbochi, Kata ya Maparoni, Kata ya Msara na Kata ya Salale vile ni visiwa shughuli zao kubwa wanazozitegemea ni uvuvi wa hawa Kambamiti hatuna shughuli nyingine yeyote ya kilimo. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka umefika kuweza kutoa Muarobaini wa tatizo hili la muda wa uvuvi kwamba wananchi hawa waruhusiwe kuanzia kipindi cha mwezi wa 12 mpaka mwezi wa tano? hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili tunajua Kambamiti wanapatikana Kibiti na sisi kama watu wa Kibiti tunapenda sana kuona rasilimali ile inawanufaisha vile vile Watanzania wengine yaani kuchangia pato la Taifa. Je, Serikali ina mkakati gani ili sasa kuweza kuhakikisha Kambamiti wale wanawanufaisha sio tu wananchi wa Kibiti Halmashauri lakini vile vile kuongeza pato la Taifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti *Comrade* Twaha Mpembenwe. Kwanza naomba nikiri swali hili ni la muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Kibiti na wale wa Jimbo langu la Mkuranga, anataka kujua ni mbinu na mkakati gani muarobaini tutakaokuwa nao wa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wa maeneo ya kisiju maeneo ya Mdimni, maeneo ya Nganje, maeneo ya Kifumangao, maeneo ya Nyamisati, maeneo ya Mfisini, maeneo ya Kiasi, Mbwera mpaka kule mpakani na Kilwa kwa maana ya Marendego.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa maana Wizara imejipanga vyema tumeshaelekeza mahsusi kabisa kwamba Shirika letu la utafiti la TAFIRI kwa kushirikiana na idara yetu kuu ya uvuvi ifanye mapitio ya utafiti tuliokwisha kuufanya na sasa tutakwenda kufanya zaidi kwa kushirikiana na wananchi wenyewe na wadau katika maeneo yote haya ili tupate suluhu ya kudumu ni ukweli usio pingika, kwamba wananchi wa maeneo haya wao wamekuwa wakihifadhi maeneo haya Samaki wanapokuwa wamekuwa wanaondoka Bahari kuu na sasa matokeo yake hawana uwezo wavuvi wale wa kuwafikia Samaki wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelekeza pamoja nami Mheshimiwa Waziri kwamba tufanya kazi ya kutoka nje kuondokana na yale mazoea ya kuwazuia tutafuta *alternative* ambayo itawafanya wananchi hawa sasa wawe na uwezo wa kuweza ku-*enjoy* rasilimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ametaka kujua juu ya mkakati wetu, ni namna gani tutawasaidia. Wananchi hawa hawana jambo jingine la kufanya hakuna kilimo kinachoenea kikakubali katika eneo lile isipokuwa uvuvi tu wa *Prawns* kwa maana ya Kambamiti, ni maelekezo tuliyo yatoa pia tutafute njia mbadala za kuwasaidia waweze kufanya uzalishaji zaidi katika miaka mitano iliyopita wananchi wa Mkuranga na Kibiti wamezalisha tani 1,200 zenye thamani ya shilingi bilioni 16 na zikaingiza Serikalini Milioni 600 sasa tunataka tutoke hapo tuongeze uzalishaji zaidi ili na wao waweze kuondokana na umaskini ambao ulioenea katika eneo hili wakati wamekalia rasilimali kubwa sana. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Subiri hapo hapo Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri kuna tatizo soko la Feri Dar es Salaam, wavuvi wanashindwa kusajili vyombo vyao mpaka wazungumze chini ya meza na hasa Zone Na.8, hebu itolee maelezo. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Mussa Azan Zungu,

Mbunge wa Ilala ambapo eneo la Feri linamiliki wapiga kura wake. Kwa mujibu wa Sheria yetu ya Uvuvi ya mwaka 2003 Na. 22 haitambui mtoaji wa leseni kuwa mtu mwingine yeyote isipokuwa Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia Idara yake ya Uvuvi ama Afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama Feri soko ambalo linamilikiwa na Manispaa ya Ilala kuna vitendo visivyokuwa vya vya uvunjifu wa sheria, kama ulivyosema watu wanatoa rushwa, natoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala na mamlaka zote pale Ilala zishughulike na jambo hili. Hawa wanaofanya vitendo hivi tumepata taarifa za awali na vyombo vyetu vya dola vinafanyia kazi kwamba wako viongozi wa sehemu inayoitwa Zone Na.8 wanafanya vitendo visivyo vya kiungwana vya kuwa-*force* wavuvi kutoa rushwa ndiyo wasajiliwe, hiyo ni kinyume cha sheria. Kwa hiyo, vyombo vyetu vitachukua hatua stahiki na jambo hilo liachwe mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuongeza nguvu kwenye uchumi wa bahari, Serikali wakati ikijibu swali la Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga katika Bunge lililopita iliahidi kuwasaidia wavuvi wa ukanda wa bahari ya Mkoa wa Lindi vifaa vya uvuvi na hasa boti ya kusaidia uvuvi wao.

Kwa kuwa ahadi hiyo imechukua muda mrefu na muda unakwenda, wakati Serikali ikijipanga kuitimiza ahadi hii, je, iko tayari kuwasaidia walau mashine ndogo ndogo zivasaidie kuboresha uvuvi wao wavuvi wa eneo hili hasa wanaotoka Jimbo la Mtama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.



**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko tayari, tutapeleka mashine kwa wavuvi wa Mchinga na Mtama. Nataka tu nimhakikishie kwamba tunao mpango mkubwa zaidi wa kuwawezesha wavuvi wa Ukanda wa Pwani *In Shaa Allah* katika bajeti yetu hii ya 2021/2022 mambo yatakuwa mazuri sana katika kuhakikisha kwamba wanafanya vizuri katika shughuli zao za uvuvi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini uliza swali lako.

Na. 271

### **Kuanzisha Wilaya ya Kitanesco - Mji wa Mafinga**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Wilaya ya *TANESCO* kwa ajili ya kuhudumia viwanda na wananchi katika Mji wa Mafinga ili kuendana na kasi ya uchumi wa viwanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mufindi ina Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, ipo Ofisi ya Wilaya ya *TANESCO* inayotoa huduma kwa wananchi wa Mji wa Mafinga pamoja na wananchi wa Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, Ofisi ya *TANESCO* iliyopo Mafinga inakidhi mahitaji ya kutoa huduma kwa wananchi wote wa Mji wa Mafinga ikiwa ni pamoja na wateja wa viwanda vikubwa 80, wateja wa viwanda vidogo vidogo 445 na wateja wadogo 23,207. Hata hivyo, Serikali kwa kutambua ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika Mji wa Mafinga, *TANESCO* imefungua Ofisi Ndogo (*Sub Office*) katika Kata ya Igowelo, Kibao na Mgololo katika Kata ya Makungu. Ofisi hizi zimeanzishwa ili kusogeza huduma karibu kwa wananchi walio mbali na Mji wa Mafinga ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa urahisi kwa wananchi wa maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwanza kabisa, nakupongeza kwa kurudi kwenye hicho kiti, tuliku-*miss* sana Mzee wa Jaza Ujazwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza na msingi wa maswali haya ya nyongeza la kwanza, asilimia thelathini ya muda wa kufanya kazi katika Mji wa Mafinga na maeneo yanayozunguka unapotea kutokana na kukatikakatika kwa umeme. Hii maana yake ni nini? Saa za kufanyakazi katika nchi yetu wastani kwa mujibu wa sheria ni saa nane. Kwa hiyo, kwa siku tunapoteza wastani wa saa mbili au dakika 144, kwa wiki tunapoteza wastani wa saa 16 au dakika 1008, kwa mwezi tunapoteza saa ya kufanya kazi 40 au dakika 2,400. Maana yake ni kwamba tunapoteza kwanza mapato kwa *TANESCO* yenyewe lakini pia mapato kwa wananchi na kwa Serikali. Swali langu linakuja, kama tuna viwanda vikubwa 80 kwa nini tusiwe na Wilaya ya *TANESCO* katika Mji wa Mafinga kama ambavyo katika Wilaya ya Ilala, Wilaya ya Temeke, Wilaya ya Kinondoni wana Wilaya za *TANESCO* zaidi ya moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, toka asubuhi nimepokea simu na meseji nyingi sana kutoka kwa wananchi

wakiuliza kwamba wanashindwa kununua LUKU leo siku ya pili jambo ambalo linakosesha *TANESCO* mapato lakini pia shughuli za uzalishaji kwa wananchi kukosa umeme zinakuwa zimesimama. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la kwanza Mafinga ni mojawapo ya maeneo ambayo *TANESCO* inafanikiwa kwa asilimia kubwa kupeleka umeme wa uhakika, kwa sababu inayo *sub-station* ambayo ipo jirani kilometa kama 80 kutoka kwenye huo mji wenyewe eneo la Igowolo na umeme huo unatokea Iringa.

Pia tunayo *line* nyingine ndogo inayotoka Iringa moja kwa moja kupeleka umeme Mafinga. Kwa hiyo, Mji wa Mafinga unalishwa na *line* mbili za umeme, ikitoka moja inaunganishwa nyingine, ikitoka nyingine inaunganishwa hiyo moja. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Chumi aendelee kutuvumilia katika maboresho tunayoendelea kuyafanya kuhakikisha umeme unakuwa wa uhakika na kama ambavyo tumeshasema mara kwa mara eneo la Iringa, Mafinga, Mbeya na Bukoba tunaathari sana za kupatwa na radi kwa hiyo tunaendelea kurekebisha mifumo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili la LUKU, nikiri kwamba kwa siku mbili na leo itakuwa ni ya tatu tumekuwa tuna tatizo na tumepata shida kubwa sana kwenye mfumo wa kidigitali wa kununua na kuuza LUKU. Tunawahakikishia kwamba tunalishughulikia, tunazo *system* mbili; *system* moja imekufa, ilipata hitilafu kidogo na tayari tumeshapata itengenezwe na hiyo *system* nyingine iliyobakia inabeba mzigo mkubwa sana na hivyo inashindwa kuhudumia wateja wote kwa wakati. Tunaahidiwa na

wataalamu wetu kwamba kabla ya siku ya leo haijaisha tatizo hilo litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na kupitia *forum* hii, naomba niwaambie Watanzania wote kwamba ukifika katika ofisi za *TANESCO* unaweza ukanunua umeme. Shida tunayo kwenye ile *data base* au mfumo unaouza kupitia kwenye mifumo ya kibenki na mifumo ya simu, ile ndiyo imepata shida kidogo lakini ukifika Ofisi ya *TANESCO* unaweza ukanunua umeme. Naomba radhi kwa niaba ya wenzangu lakini tunawahakikishia kwamba leo kabla siku haijaisha tutajitahidi kuhakikisha huduma hiyo inarejea ili Watanzania waendeleo kupata huduma ya LUKU kama kawaida.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa usambazaji wa umeme kwa kutumia *REA* umekuwa ukitumia transfoma za KV 50 lakini Serikali kwa ujumla na kama Taifa tumekuwa tukihamasisha sana shughuli za uzalishaji. Je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kutumia umeme huu wa KV 50 wakati idadi ya watu na shughuli za uzalishaji zinaongezeka baadaye kuonekana kwamba umeme huu hautoshi. Kwa nini Serikali isianze sasa kubadilisha badala ya kuweka KV 50 ianze kwa maeneo kidogo kidogo kuweka KV 100? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunapeleka umeme tunaangalia na kuzingatia mahitaji ya wananchi walio katika

maeneo hayo. *Transformer* ya KV 50 ni *transformer* kubwa inaweza kuhudumia wateja zaidi ya 200 katika eneo moja. Kwa hiyo, kadri wateja wanavyoongezeka na sisi tutazidi kuboresha na kuongeza ukubwa wa *transformer* tunazoziweka katika maeneo husika.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mwongozo wa Spika

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga subiri kwanza. Sasa ni muda wa kutangaza wageni ambao wapo Bungeni.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni 35 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo ambao ni Dkt. Zainab Chaula -Katibu Mkuu; Dkt. Jim Yonazi - Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Onorius Njole - Mwenyekiti wa Bodi TTCL; Ndugu Waziri Kindamba - Mkurugenzi Mkuu TTCL; Dkt. Jonas Kilimba - Mwenyekiti wa Bodi TCRA; Dkt. Jabiri Bakari - Mkurugenzi Mkuu TCRA; Ndugu Gerald Matee - Mwenyekiti wa Bodi Mfuko wa Mawasiliano; Ndugu Justina - Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Mawasiliano na Ndugu Maorice Mbodo - PMG Posta. (*Makofi*)

Wageni wengine 36 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni wanafunzi kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilichopo Kigamboni Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Nevis Mbwire. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 25 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni WAWATA – Dekania Paulo wa Msalaba kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Stella Mavunde. Karibuni mmependeza na hizo nguo, mkija tena vaeni rangi nyingine, ile nyekundu. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni 35 wa Mheshimiwa Michael Mwakamo (Mb), ambao ni walimu 7 na wanafunzi 28 kutoka Shule ya Awali na Msingi Mikongeni iliyopo Kibaha Mkoa wa Pwani

wakiongozwa na Mkurugenzi wa Shule hiyo Ndugu Florah Lyakurwa. Karibuni watoto. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi (Mb), ambaye ni Mratibu wa *Tanzania Cooking Festival* na Mkurugenzi wa *Epics Catering* kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam Ndugu Secilia Muloki. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Jafari Chege (Mb), ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* wenyeji wa Jimbo la Rorya, Mkoani Mara, wakiongozwa na Ndugu Martina Atieno. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu (Mb), ambao ni wapiga kura wake kutoka Ikungi, Mkoa wa Singida, Ndugu Julius Marecho na Ndugu Getruda Swalehe. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Florent Kyombo (Mb), ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Misenyi, Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Ndugu Primus Joseph. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb), ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Mohamed Mwera. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga (Mb), ambaye ni mdogo wake kutoka Chuo cha Jordan, Mkoani Morogoro, Ndugu Suzan Aman. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Timothy Mnzava (Mb), ambao ni mdogo wake Ndugu Simon Mnzava na rafiki yake Ndugu Yohana Aloyce kutoka Korogwe Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika anawatangazia Wabunge wote na watumishi wote wa Bunge kitabu cha Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili kipo katika viwanja vya Bunge. Wabunge mnaombwa mtembelee eneo hilo na

wote mnunue kitabu hicho ili mjue kumbukumbu na taarifa rasmi na maisha ya Mzee Mwinyi ambaye aliishi akiwa Rais na Kiongozi Mkuu katika Taifa letu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuomba Mwongozo wa Kiti sawasawa na Kanuni ya 76 kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni leo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Michezo akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, swali namba 266 ambalo lilizungumzia namna gani Serikali inafanya mipango ili Timu ya Taifa ifanye vizuri katika michezo ya Kitaifa, Waziri akasema kwamba Simba wakati inacheza inakuwa Timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesimama kuomba mwongozo, je, Timu ya Taifa inakuwa imekufa? Hasa ukizingatia kwamba Timu ya Simba hivi karibuni imeiletea unyonge Taifa kwa kufungwa mabao manne. Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, umeshakaa chini au umesimama bado, endelea kukaa chini, Katibu. *(Kicheko)*

### **NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO A MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niombe hotuba yangu nzima kama ilivyowasilishwa Bungeni iingie na iwe kumbukumbu sahihi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nichukue nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako binafsi, Bunge lote na Familia ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Watanzania wote kwa kuondokewa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyefariki tarehe 17 Machi, 2021. Msiba huu ni pigo kubwa kwa Taifa letu kutokana na uongozi wake mahiri, uchapakazi na uzalendo uliotukuka kwa Taifa. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi, amina. Sisi kama Wizara tutamkumbuka kwa kuwa na maono ya kipekee kwa kuanzisha Wizara hii mpya ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari mnamo tarehe 5 Disemba, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali wakiwemo Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe (Kigoma) na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) kupitia Mkoa wa Manyara. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika ameandika historia kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke. Hii inadhihirisha mfumo thabiti wa kidemokrasia tulionao Tanzania wa kurithishana kwa amani madaraka kwa mujibu wa Katiba. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pasi na shaka ana uwezo mkubwa, ujuzi na uzoefu katika masuala ya uongozi Serikalini na katika siasa ambazo ni nyenzo muhimu zitakazomwezesha kuiongoza vyema nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa kwa kura zote na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Napenda pia kuwapongeza Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuhudumu katika Serikali ya Awamu ya Sita. Kwetu sote nafasi hizi tulizopewa na Watanzania ni deni kubwa, ambalo namna pekee ya kulilipa ni kwa kuwatumia wananchi kwa bidii na weledi mkubwa, Kazi na lendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, kwa hotuba yake ambayo imefafanua kwa kina utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali ya kuimarisha na kuboresha huduma za jamii kwa lengo la kupunguza kero za wananchi zinazotokana na umasikini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, nachukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, natoa shukrani zangu za dharti kwa familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuniwezesha kutekeleza majukumu kwa utulivu. Aidha, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kigamboni kwa kuniadini na kunichagua kwa kura za kishindo na kwa ushirikiano ambao wanaendelea kunipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Fungu 68 iliidhinishwa bajeti na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 15,654,466,000. Kati ya fedha hizo shilingi 2,196,528,000 ni kwa ajili ya mishahara; shilingi 2,457,938,000 ni za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 11 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya shilingi 9,321,425,513.78 zilipokelewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa Mapato, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Fungu 68 lilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 30. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Fungu 68 imekusanya jumla ya shilingi 26,276,724,992.50 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa

Mawasiliano *NICTBB* ambayo ni sawa na asilimia 87.5 ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 425,890,138,007. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Taasisi zimekusanya jumla ya shilingi 284,225,394,121.99 sawa na asilimia 66.9 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Moja, tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 yamefanyika na kubainisha maeneo yatakayojumuishwa katika Sera mpya ya Posta. Aidha, mapitio ya Sheria ya Shirika la Posta Tanzania ya Mwaka 1993 na Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *UCSAF* ya Mwaka 2006 yamefanyika na kubaini maeneo ya kufanyiwa marekebisho ili kuboresha utendaji wa Taasisi;

Pili, kusimamia utekelezaji wa huduma za Serikali kupitia eneo moja (Huduma Pamoja) kupitia miundombinu ya Shirika la Posta. Maandalizi ya Ofisi kwa ajili ya kutoa huduma yamekamiliika katika Ofisi za Posta Dodoma na Dar es Salaam ambapo huduma zitaanza kutolewa mwishoni mwa mwezi Juni, 2021. Ofisi za Arusha, Mbeya na Kijangwani – Zanzibar zitaanza kutoa huduma mwezi Agosti, 2021;

Tatu, mpango wa kupunguza gharama za huduma za mawasiliano kwa wananchi wa nchi za Afrika Mashariki wanapotembelea nchi wanachama ndani ya Jumuiya, *The East Africa Roaming Framework* umekamilika;

Nne, maandalizi ya kuanzisha chombo huru cha kusimamia, kuendesha na kuendeleza Mkongo wa Taifa yanaendelea; hatua inayofuata ni kupata vibali kutoka mamlaka husika;

Tano, maandalizi ya mradi wa Tanzania ya Kidijitali yamekamilika na unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Mradi huu unalenga kuleta mabadiliko ya kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya kijiditali ya kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza uchumi;

Sita, Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Usalama wa Mitandao wa Mwaka 2020/2021 – 2023/2024 unaolenga kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu matumizi salama ya mitandao. umeandaliwa.

Saba, mambo mengine yaliyotekelezwa na Wizara ni pamoja na Mkakati wa Taifa wa Mtandao wenye Kasi (*National Broadband Strategy*) ya mwaka 2021 - 2026 umeandaliwa kwa lengo la kuweka utaratibu utakaowezesha uwepo wa *internet* yenye kasi kubwa, ubora wenye viwango vya juu na gharama nafuu za huduma za mitandao, maudhui, programu za kompyuta, usalama wa mitandao kwa watumiaji;

Nane, Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Utatuzi wa Matumizi Mabaya ya Huduma na Bidhaa za Mawasiliano imeundwa, ambayo inajumuisha wadau mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya uhalifu wa mitandao. Kamati hii imeanza kufanya kazi mwezi Machi, 2021.

Tisa utambuzi wa Miundombinu Nyeti ya Taifa ya *TEHAMA, National Critical Infrastructure – NCI*, umefanyika na umeandaliwa mwongozo wa kuitambua na kuisimamia ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa miundombinu hiyo;

Kumi, Mwongozo wa ufikishaji wa miundombinu ya *TEHAMA* kwenye Shule za Serikali 20,269 na vituo vya afya na maeneo ya jamii 5,578 umeandaliwa. Mwongozo huu unalenga kufikisha huduma za mawasiliano kwenye taasisi hizo na utekelezaji wake utakuwa wa miaka 10 kuanzia mwaka 2021; na

Kumi na moja, mwongozo wa Usajili wa Wataalam wa *TEHAMA* nchini umeandaliwa, ambao umeweka utaratibu

madhubuti wa kuwezesha utambuzi na usajili wa wataalam wa *TEHAMA* ili kuhakikisha kuwa viwango stahiki vya taaluma ya *TEHAMA* vinafikiwa na kulindwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zilizo chini ya Wizara zimefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imefanikiwa kutambua miamala 2,860,988,609 ambapo kiasi cha 170,513,110,859,867 kilipita kwenye miamala ya simu. Tumeweza kuzuia mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na simu za Kimataifa ambapo jumla ya simu za ulaghai zipatazo 3,165 zilibainika na watuhumiwa walichukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika la Mawasiliano Tanzania *TTCL* limefanikiwa kuongeza idadi ya wateja kutoka wateja 701,262 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia wateja milioni 1,215,762 mwezi Aprili, 2021, kuongeza idadi ya watumiaji wa *T-PESA* kutoka 466,605 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia 835,931 mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania, *TPC* limefanikiwa kununua magari makubwa matano na pikipiki 50 kwa ajili ya kusafirisha mizigo ikiwemo barua, nyaraka, vifurushi na vipeto kufanya ukarabati na ubadilishaji wa mwonekano wa majengo matatu ya Posta katika Mikoa ya Mbeya, Lindi na Singida.

Mheshimiwa Spika, Tume ya *TEHAMA* imefanikiwa kuanzisha kanzidata ya wataalam wa *TEHAMA* ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 imesajili wataalam 415.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) imeendelea na zoezi la ufikishaji wa huduma ya mawasiliano vijijini ambapo mikataba ya kufikisha huduma za Mawasiliano katika Kata 61 zenye jumla ya Vijiji 173 imesainiwa. Aidha, kukamilika kwa miradi katika Kata hizo kunafanya huduma za mawasiliano

kufika katika Kata 1,057 zenye Vijiji 3,292 na wakazi zaidi ya milioni 12 ifikapo Oktoba, 2021; kuunganisha mtandao wa *internet* na kutoa vifaa vya *TEHAMA* ikiwemo kompyuta tano na *printer* moja kwa kila shule kwa shule za Umma 151; kutoa mafunzo ya *TEHAMA* kwa Walimu 601, kati yao Walimu 88 wanatoka Zanzibar na Walimu 513 wanatoka Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imetekeleza mradi wa kuongeza usikivu wa redio kwa kuhisha studio ya Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*) ambapo mfuko umefunga mfumo wa umeme na vifaa vya studio katika Studio ya *TBC* Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania, *TCRA CCC* kupitia Kamati za Watumiaji limehamasisha, limeshauri na kupokea maoni ya watumiaji 24,964 katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba ambapo Kamati zimeundwa. Aidha, Baraza limetoa elimu kwa watumiaji 1,686,000 kuhusu haki, wajibu, utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko na matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano *UCSAF, TCRA, TPC, TTCL*, Tume ya *TEHAMA* na *TCRA CCC* umefafanuliwa kwa undani kwenye ukurasa 15 hadi 32 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano; kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha Mwaka 2019, Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 7.2 mwaka 2019. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, asilimia 66 ya ardhi ya Tanzania (*Geographical Coverage*) inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani. Sekta hii huchangia katika

uchumi moja kwa moja na kupitia sekta nyingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za TCRA zinaonyesha kuwa, laini za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka shilingi 48,939,530 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia laini milioni 53,063,085 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Watumiaji wa *internet* waliongezeka kutoka 26,832,089 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia 29,071,817 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka 27,127,298 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia 32,720,180 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 20.6. Aidha, vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 193 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia vituo 200 mwezi Aprili, 2021 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 43 mwezi Julai, 2020 na kufikia vituo 50 mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeendelea kutekelezwa ambapo jumla ya Kilomita 409 zinaendelea kujengwa. Kilomita 72 zinajengwa kutoka Mangaka hadi Mtambaswala ili kuunganisha nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala. Kilomita 265 zinajengwa katika mzunguko wa Kaskazini, Kusini na Magharibi ili kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya Singida na Mbeya kupitia Itigi, Rungwa hadi Kambikatoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kilomita 72 za Mkongo zinajengwa ili kuunganisha watumiaji wa mwisho (*Last mile connectivity*) katika Ofisi za Serikali zilizopo Msalato, Mtumba na Kikombo Mkoani Dodoma. Vilevile, Mkongo wa Taifa wenye urefu wa Kilomita 105 kati ya Arusha na Namanga uliojengwa ardhini utahamishwa na kupitishwa kwenye nguzo za umeme wa TANESCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano utajumuisha pia ujenzi wa vituo vya kutolea

huduma za mawasiliano katika eneo la Mtambaswala pamoja na vituo vitatu vya kuongeza nguvu ya Mkongo wa Taifa. Vituo viwili viko maeneo ya Kiyombo na Rungwa Singida na kituo kimoja eneo la Lupa na Tingatinga Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tumeweza kuunganisha nchi saba kati ya nane zinazopakana na Tanzania kijlografia isipokuwa nchi moja ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *DRC*. Taratibu za kufanya upembuzi yakinifu zinaendelea ili kuwezesha kupata mahitaji ya kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi ya *DRC* kupitia chini ya maji ya Ziwa Tanganyika (*submarine cable*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi ni Mradi unaotoatarifa sahihi ya anapopatikana mwananchi na utambulisho wa matumizi ya eneo husika. Taarifa hizo zinarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma za Serikali na kijamii mahali ambapo mwananchi sambamba na kuwezesha biashara mtandao *e-Commerce*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 shughuli zifuatazo katika Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi zimetetelezwa: moja, kusimika nguzo zinazoonesha majina ya barabara, mitaa na njia na kubandika vibao vya namba za nyumba katika Jiji la Mwanza inaendelea kufanyika. Aidha, kazi ya ubandikaji wa vibao vya namba za nyumba inaendelea kufanyika katika Halmashauri 11 za Majiji ya Dodoma Kata saba na Tanga Kata tano; Manispaa za Ilemela Kata tatu, Shinyanga Kata nne, Morogoro Kata saba na Moshi Kata tisa; Wilaya za Chato Kata mbili, Chamwino Kata moja na Bahi Kata moja pamoja na Miji ya Geita Kata moja na Kibaha Kata tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani kwa maana ya *shapefiles* za Majiji ya Halmashauri tisa zimeandaliwa. Halmashauri hizo ni Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Kigamboni, Manispaa ya Temeke, Manispaa ya Ubungo, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha, Jiji la Mwanza, Jiji la Dodoma na Jiji la Mbeya. Programu tumizi *Mobile App*



ya kutumia simu za mkononi imeandaliwa ambayo itaongeza ufanisi katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi. Programu tumizi husika itawezesha kukusanya taarifa za barabara na mitaa, makazi na wakazi sambamba na kuonesha maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kukusanya taarifa za makazi na wakazi kwa kutumia programu tumizi inaendelea katika Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na Halmashauri. Maandalizi ya kukusanya taarifa katika Majiji ya Arusha na Tanga yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yaliyotekelezwa na Wizara kwenye mradi huu ni kuandaa mpango mkakati wa kuharakisha utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi kwa kipindi cha mwaka 2021 - 2025 umeandaliwa; Mafunzo ya *GIS, GPS, Database & Map Development* yametolewa kwa wataalam watano wa Wizara ili kuwawezesha kutekeleza mradi huo; Wataalam 36 wa Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mwanza na Tanga wamejengewa uwezo wa kutekeleza mradi; na Viongozi na watendaji 813 wa Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mwanza na Tanga wamejengewa uelewa kuhusu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Makadirio ya Mapato ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2021/2022; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Fungu 68 inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 50 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni jumla ya shilingi 216,384,551,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,984,770,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo shilingi 2,023,935,000 ni za Mishahara na Shilingi 2,960,835,000 ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, kiasi cha shilingi 211,399,781,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la *TEHAMA*, Wizara itasimamia utekelezaji na uendelezaji wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kujenga jumla ya Kilomita 1,880 za Mkongo katika maeneo Musoma – Simiyu - Shinyanga, Kilomita 304; Tabora -Uvinza, Kilomita 315; Manyoni – Mbeya, Kilomita 529; Babati – Dodoma, Kilomita 270; Chato - Bwanga, Kilomita 60; Isaka - Kahama - Kilomita 42; na Ifakara – Mlimba – Songea, Kilomita 360.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwezo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano utapanuliwa kutoka *Gigabit* 200 hadi kufikia ukubwa wa *Gigabit* 400. Vilevile, tutafanya ujenzi wa vituo 17 vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi kufikia katika ngazi za Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itasimamia utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali kwa kuhakikisha tunawezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda, Kimataifa na Kitaifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali (*Digital Economy*). Katika mradi huu tunatazamia kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa kituo kimoja kikubwa cha kukuza taaluma na ubunifu katika *TEHAMA* na vituo vitatu vitatu vidogo kwenye Majiji ya Mbeya, Mwanza na Arusha; Kuhakikisha usanifu wa mitambo na vifaa ili kuboresha na kujenga mtandao wa huduma za Serikali wenye usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha ununuzi wa *bandwidth* kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali, kununua vifaa na kuboresha Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi *data* unafanyika, kuhakikisha ujenzi na ukarabati wa vituo 10 vya Huduma za Jamii, ujenzi wa maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua vifaa vya *TEHAMA* katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zitakazofanyika kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidijitali ni pamoja na ujenzi wa minara ya mawasiliano 150 kwenye kata 150, ili kuwezesha huduma za *broadband* nchini unafanyika na kuhakikisha upanuzi na uboreshaji wa miundombinu iliyopo ya *broadband* inayomilikiwa na Serikali kwa maana ya *GovNET* unafanyika ili kuongeza ubora na umadhubuti wa huduma za Serikali mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mradi huu utafanya kazi ya ujenzi wa miundombinu ya saine za kielektroniki (*The National Public Key Infrastructure – NPKI*); Kutekeleza Mradi wa Huduma Pamoja (*One Stop Center*); na Kutekeleza ujenzi wa Mfumo wa Biashara Mtandao (*e-Commerce*) kupitia miundombinu ya Shirika la Posta na kujenga mfumo wa kijamii *social network* kwa ajili ya matumizi ya ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zitakazofanyika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika ngapi?

**MWENYEKITI:** Omba pesa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu iingie kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa shukrani kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishwa shilingi 216,384,551,000. Kati ya fedha hizo shilingi 4,984,770,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida; Sh.2,023,935,000 ni kwa ajili ya

mishahara na Sh.211,399,781,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA  
HABARI MHESHIMIWA. DKT. FAUSTINE NDUGULILE (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA  
2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2020/21. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la kumi na mbili. Aidha, tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya janga linaloendelea kusumbua dunia kwa sasa la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID -19). Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika kuhabarisha umma juu ya njia za kujikinga na ugonjwa huu pamoja na kupata huduma mbalimbali za kijamii na kibiashara kwa njia ya mitandao.

3. *Mheshimiwa Spika*, nichukue fursa hii kutoa pole kwako, Bunge na Watanzania wote kwa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyefariki tarehe 17 Machi, 2021.

Sisi kama Wizara tutamkumbuka kwa kuwa na maono ya kipekee kwa kuanzisha Wizara hii mpya ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tarehe 05 Disemba, 2020. Wizara hii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuifikisha Tanzania kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (*4th Industrial Revolution*) yanayoweza kwenye TEHAMA kama yalivyosomwa hapa kwenye Bunge lako Tukufu kwenye hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati wa kufungua rasmi Bunge la kumi na mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe 13 Novemba, 2020. Dhamira hii imeendelea kuisitizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwenye hotuba yake aliyoitoa wakati akihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali wakiwemo Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe (Kigoma) na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) kupitia Mkoa wa Manyara. Ninaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika ameandika historia kwenye ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke. Hii inadhihirisha mfumo thabiti wa kidemokrasia tulionao Tanzania wa kurithishana kwa amani madaraka kwa mujibu wa Katiba. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pasi na shaka ana uwezo mkubwa, ujuzi na uzoefu katika masuala ya uongozi Serikalini na katika siasa ambazo ni nyenzo muhimu zitakazomwezesha kuiongoza vyema nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa kwa kura zote na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7. **Mheshimiwa Spika**, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vilevile, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

8. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuhudumu katika Serikali ya Awamu ya Sita.

9. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa tena kutumikia nafasi hizo kwenye Bunge la kumi na mbili. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwenye nafasi hizo muhimu za kusimamia utekelezaji wa shughuli zinazopangwa na Serikali kwenye sekta na maeneo husika.

10. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na ya mwananchi mmoja mmoja kijamii na kiuchumi. Aidha, kwa namna ya pekee ninaomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Kigamboni kwa kunichagua tena kwenye Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020; bila kuisahau familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

11. **Mheshimiwa Spika**, ninachukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na **Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso (Mb)**, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati **Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb)**, Mbunge wa Same Mashariki. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Wizara. Ninapenda kullarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika Bajeti hii.

12. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru **Mheshimiwa Mhandisi Kundo A. Mathew (Mb.)**, Naibu Waziri; **Dkt. Zainab A. S. Chaula**, Katibu Mkuu na **Dkt. Jim Yonazi**, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara yangu, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia TEHAMA.

13. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia Taasisi Sita zilizogawanyika kwenye umahsusi wa udhibiti, mfuko, mashirika ya kibiashara na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); Tume ya Taifa ya TEHAMA (ICTC); na Baraza la Ushauri kwa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC). Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala mbalimbali ambayo taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zinatekeleza.

14. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni Taasisi ya umma liliyoanzishwa kwa sheria Na. 12 ya mwaka 2003 (*Tanzania Communications Regulatory Act No. 12 of 2003*) ambapo pamoja na mambo mengine, Mamlaka imekabidhiwa majukumu ya:-

- i) Kutoa leseni za watoa huduma za mawasiliano nchini;
- ii) Kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayakufuatwa;
- iii) Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa kama gharama za maunganisho kati ya mtandao mmoja na mwingine;
- iv) Kuweka viwango, kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazothibitiwa; na
- v) Kudhibiti viwango na bei ya jumla ya mawasiliano kati ya mitandao;
- vi) Kufuatilia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni Pamoja na;
  - a) Viwango vya uwekezaji;
  - b) Upatikanaji, ubora na viwango vya huduma;
  - c) Gharama za huduma; na
  - d) Ufanisi wa uzalishaji na usambazaji wa huduma.
- vii) Kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migogoro;
- viii) Kusambaza taarifa zinazohusu kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na
- ix) Kushauriana na mamlaka nyingine za udhibiti katika kutekeleza majukumu sawa na yale ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

15. **Mheshimiwa Spika**, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeanzishwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 (*Tanzania Communications Regulatory Act No.*



12 of 2003) Kifungu cha 37. Kulingana na Sheria iliyoanzisha Baraza, Kifungu cha 38 kinalipa Baraza majukumu yafuatayo:

- i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kushauriana na TCRA, Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano na watoa huduma.
- ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni kuhusu masuala ya msingi ya
- iii) Watumiaji wa huduma za mawasiliano;
- iv) Kuanzisha kamati za watumiaji katika ngazi za mikoa, wilaya na sekta na kushauriana na kamati hizo; na
- v) Kufanya mashauriano na wahusika katika sekta, Serikali na makundi mengine ya watumiaji wa huduma kuhusiana na masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma zinazosimamiwa kisheria.

16. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) ni Shirika la Umma lenye jukumu la kutoa huduma za mawasiliano kwa jamii na kusimamia uendeshaji wa Miundombinu ya Kimkakati kwa usalama wa nchi. Shirika lilianzishwa kupitia Sheria Na. 12 ya Bunge ya mwaka 2017 (*Tanzania Telecommunications Corporation Act, No. 12 of 2017*). Kwa mujibu wa sheria hiyo, Shirika la Mawasiliano Tanzania lina majukumu ya msingi yafuatayo: -

- i) Kuimarisha ulinzi na usalama wa huduma za mawasiliano ya simu nchini na utoaji wa huduma ya mawasiliano ya simu kibiashara na kiuchumi;
- ii) Kutoa huduma za mawasiliano ya simu kwa mujibu wa Sheria;
- iii) Kujenga na kuendesha miundombinu ya mawasiliano ya kimkakati kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana;

iv) Kutoa huduma ya miamala ya kifedha inayohusiana na mawasiliano ya simu;

v) Kuendesha mifumo na huduma ya mawasiliano ya simu ikiwemo mfumo wa TEHAMA ndani na nje ya nchi;

vi) Kutoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti na picha;

vii) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu TEHAMA kwenye mashirika, Taasisi za umma na kwa wajasiriamali; na

viii) Kukuza uwekezaji wa huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya nchi.

17. **Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 11 ya mwaka 2006 sura ya 422, kwa lengo la kupeleka na kufikisha huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo machache ya mijini na maeneo mengi yaliyo mbali vijijini yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa watoa huduma ya mawasiliano. Mwaka 2009 kanuni za Mfuko zilipitishwa na Mfuko kuanza kazi tarehe 1 Julai, 2009. Malengo ya Mfuko yaliyoainishwa na sheria ya uanzishwaji wake yamejikita katika maeneo yafuatayo:

i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

ii) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iii) Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iv) Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;

v) Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na

vi) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

18. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheria Na. 19 ya mwaka 1993 na lilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari, 1994 baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Baada ya kuvunjwa, iliundwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania kwa mgawanyo wa mali wa asilimia 70 kwa 30 mtawalia. Shirika la Posta linamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Shirika lina majukumu makuu manne kama ifuatavyo:-

i) Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya huduma za Posta katika sekta za viwanda, biashara na jamii kwa ujumla kwa ufanisi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii) Kutoa huduma za kutuma na kulipa fedha kwa njia ya hawala za Posta (*Money Order na Postal Order*), au kwa kutumia njia nyingine zinazoonekana zinafaa; na

iv) Kutoa huduma za Kaunta kwa ajili ya Shirika na Huduma za Serikali bila kuathiri majukumu mengine yaliyotajwa katika Sheria ya uanzishwaji wa Shirika.

19. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya TEHAMA ilianzishwa kwa Amri ya Rais kupitia Tangazo Namba 532 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Uanzishwaji wa Tume ya TEHAMA nchini ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2003 na maelekezo ya Baraza la Mawaziri yaliyotolewa Juni, 2012 kuhusu kuunda Tume ya Kitaifa ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano (TEHAMA) nchini. Kwa mujibu wa Amri iliyoanzisha Tume ya TEHAMA, majukumu yake ni pamoja na:-

- i) Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;
- ii) Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani ya TEHAMA;
- iii) Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;
- iv) Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na
- v) Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoainishwa na Sheria.

## **B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

### **Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano**

20. *Mheshimiwa Spika*, kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2019, Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi ya **asilimia 7.2** mwaka 2019. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, **asilimia 66** ya ardhi ya Tanzania (*Geographical Coverage*) inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani. Sekta hii huchangia katika uchumi moja kwa moja na kupitia sekta zingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia teknolojia ya habari.

21. *Mheshimiwa Spika*, takwimu za TCRA zinaonyesha kuwa laini za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka **48,939,530** mwaka 2020 hadi kufikia laini 53,063,085 mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 10.8**. Watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka **26,832,089** mwaka 2020 hadi kufikia **29,071,817** mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia**

8.3. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka **27,127,298** mwaka 2020 hadi kufikia **32,720,180** mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 20.6**. Aidha, vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo **193** mwaka 2020 hadi kufikia vituo **200** mwezi Aprili, 2021 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo **43** mwaka 2020 na kufikia vituo **50** mwezi Aprili, 2021.

### Ukusanyaji wa Mapato

22. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) ilikadiriya kukusanya jumla ya **Shilingi 30,000,000,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) imekusanya jumla ya **Shilingi 26,276,724,992.50** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) ambayo ni sawa na **asilimia 87.5** ya makadirio ya makusanyo.

### Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge Mwaka wa Fedha 2020/21

23. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) iliidhinishwa kutumia kiasi cha **Shilingi 15,654,466,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,654,466,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 11,000,000,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

24. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara imepokea na kutumia kiasi cha **Shilingi 4,711,497,069.55** kutoka Hazina, ambacho ni sawa na **asilimia 101.2** ya fedha zilizotengwa.

### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

25. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68)

imepokea jumla ya **Shilingi 4,609,928,444.23** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni **asilimia 41.9**.

## **Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

### **Eneo la Mawasiliano**

26. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika Eneo la Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:

i) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 yamefanyika ambapo tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo imekamilika na kubainisha maeneo yatakatayojumuishwa katika Sera mpya ya Posta;

ii) Mapitio ya Sheria ya Shirika la Posta Tanzania ya mwaka 1993 na Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ya mwaka 2006 yamefanyika na kubaini maeneo ya kufanyiwa marekebisho ili kuboresha utendaji wa Taasisi husika. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hizo na Kanuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yameandaliwa;

iii) Kusimamia utekelezaji wa huduma za Serikali kutolewa eneo moja (Huduma Pamoja) kupitia miundombinu ya Shirika la Posta. Maandalizi ya Ofisi kwa ajili ya kutoa huduma yamekamilika katika Ofisi za Posta Dodoma na Dar es Salaam ambapo huduma zitaanza kutolewa mwishoni mwa mwezi Juni, 2021. Ofisi za Arusha, Mbeya na Kijangwani – Zanzibar zitaanza kutoa huduma mwezi Agosti, 2021; iv) Rasimu ya Mkakati wa kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mawasiliano umeandaliwa; ambapo jumla ya **Shilingi Bilioni 1,094.82** zinahitajika kwa ajili ya kujenga minara katika kata **1,381** kwenye maeneo yote yenye makazi ambayo hayana huduma za mawasiliano. Hatua zinazoendelea ni pamoja na kufanya uhakiki wa maeneo husika sambamba na kufanya marekebisho ya Kanuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuongeza wigo wa fedha za utekelezaji wa mkakati husika;

v) Mpango wa kupunguza gharama za huduma za mawasiliano kwa wananchi wa nchi za Afrika Mashariki wanapotembelea nchi wanachama ndani ya Jumuiya (*EAC Roaming Framework*) umekamilika. Utekelezaji wa Mpango husika kwa hapa nchini utakuwa na faida zifuatazo:

a) kuchochea biashara ndani ya ukanda na kukuza sekta nyingine za kiuchumi;

b) kuvutia watumiaji wengi kuendelea kutumia huduma za nyumbani wakiwa nje ya nchi na hivyo kukuza kiasi cha mawasiliano nchini sambamba na mapato ya Serikali;

c) kudumisha utangamano na mahusiano ya kidiplomasia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;

vi) Tumeandaa na kusaini maeneo ya mashirikiano ya kukuza ubunifu katika TEHAMA kati ya Tanzania na nchi ya Estonia. Makubaliano haya yatawezesha kubadilishana utalaam, watalaam kujengewa uwezo pamoja na kuendeleza kampuni za ndani.

### **Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

27. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika Eneo la TEHAMA imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kubadilisha betri zilizokwisha muda wake wa matumizi na kununua betri mpya **2,048**, kuzifunga katika vituo **71** vya Mkongo wa Taifa ili kuhakikisha kuwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unakuwa wa uhakika na kupatikana wakati wote, pamoja na kufanya ukaguzi ili kuboresha uendeshaji wa Mkongo;

ii) Maandalizi ya kuanzisha chombo huru cha kusimamia, kuendesha na kuendeleza Mkongo wa Taifa yamekamilika, hatua inayofuata ni kupata vibali kutoka mamlaka husika;

iii) Ukaguzi wa miundombinu ya watumiaji wa mwisho waliounganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Mikongo mingine Wilayani (*Last Mile Connectivity*) ili kubaini na kuunganisha ofisi za Serikali ambazo hazijapata mawasiliano;

iv) Maandalizi ya mradi wa Tanzania ya Kidijitali yamekamilika na unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/22. Mradi huu unalenga kuleta mabadiliko ya kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya kijiditali ya kikanda na kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi;

v) Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Usalama wa Mitandao (2020/21 – 2023/24) unaolenga kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu matumizi salama ya mitandao umeandaliwa;

vi) Mkakati wa Taifa wa Mtandao wenye Kasi (*National Broadband Strategy 2021-2026*) umeandaliwa kwa lengo la kuweka utaratibu utakaowezesha uwepo wa intaneti yenye kasi kubwa, ubora wenye viwango vya juu na gharama nafuu za huduma za mitandao, maudhui, programu za kompyuta, usalama wa mitandao na watumiaji;

vii) Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Utatuzi wa Matumizi Mabaya ya Huduma na Bidhaa za Mawasiliano imeundwa, ambayo inajumuisha wadau mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya uhalifu wa mitandao. Kamati hii imeanza kufanya kazi mwezi Machi, 2021;

viii) Utambuzi wa Miundombinu Nyeti ya Taifa ya TEHAMA (*National Critical Infrastructure – NC1*) umefanyika na umeandaliwa mwongozo wa kuitambua na kuisimamia ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa miundombinu hiyo;

ix) Kukamilisha utengenezaji wa tovuti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yenye anwani **[www.mawasiliano.go.tz](http://www.mawasiliano.go.tz)** na kuwekwa taarifa muhimu zinazohusu Wizara;



x) Mwongozo wa ufikishaji wa miundombinu ya TEHAMA kwenye shule za Serikali **20,269** na vituo vya afya na maeneo ya jamii **5,578** umeandaliwa. Mwongozo huu unalenga kufikisha huduma za mawasiliano kwenye taasisi hizo na utekelezaji wake utakuwa wa miaka kumi (10) kwa kuanzia mwaka 2021; na

xi) Mwongozo wa Usajili wa Wataalam wa TEHAMA nchini umeandaliwa, ambao umeweka utaratibu madhubuti wa kuwezesha utambuzi na usajili wa wataalam wa TEHAMA ili kuhakikisha kuwa viwango stahiki vya taaluma ya TEHAMA vinafikiwa na kulindwa nchini.

### **Utekelezaji wa Masuala Mengine**

28. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

i) Kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26);

ii) Muundo wa Wizara umeandaliwa baada ya Sekta ya Mawasiliano kuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

iii) Kuhuishwa Miundo ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Shirika la Posta Tanzania; iv) Kukamilisha umiliki wa kiwanja cha Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Umoja huo, Jijini Arusha; na

iv) Kuondoa jukumu lilolokuwa linafanywa na Shirika la Posta Tanzania la kuwalipa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki.

### **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Miradi inayotekelezwa na Wizara ni Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliotengewa **Shilingi**

**8,000,000,000** na Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi wenye jumla ya **Shilingi 3,000,000,000**. **Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

30. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeendelea kutekelezwa ambapo jumla ya **Kilomita 409** zinaendelea kujengwa katika Mwaka wa Fedha 2020/21. **Kilomita 72** zinajengwa kutoka Mangaka hadi Mtambaswala ili kuunganisha nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala. **Kilomita 265** zinajengwa kwenye mzunguko wa Kaskazini, Kusini na Magharibi ili kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya Singida na Mbeya kupitia Itigi, Rungwa hadi Kambikatoto. Aidha, **Kilomita 72** za Mkongo zinajengwa ili kuunganisha watumiaji wa mwisho (*Lastmile connectivity*) katika Ofisi za Serikali zilizopo Msalato, Mtumba na Kikombo mkoani Dodoma. Vilevile, Mkongo wa Taifa wenye urefu wa **Kilomita 105** kati ya Arusha na Namanga uliojengwa ardhini utahamishwa na kupitishwa kwenye nguzo za umeme wa TANESCO.

31. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano utahusisha pia ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za mawasiliano katika eneo la Mtambaswala pamoja na vituo vitatu vya kuongeza nguvu ya Mkongo wa Taifa. Vituo viwili viko maeneo ya Kiyombo na Rungwa (Singida) na kituo kimoja eneo la Lupa Tingatinga (Mbeya).

32. **Mheshimiwa Spika**, hadi sasa tumeweza kuunganisha nchi saba kati ya nane zinazopakana na Tanzania kijiografia isipokuwa nchi moja ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Taratibu za kufanya upembuzi yakinifu zinaendelea ili kuwezesha kupata mahitaji ya kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi ya DRC kwa kupita chini ya maji ya Ziwa Tanganyika (*submarine cable*).

### **Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi**

33. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi ni Mradi unaotoa taarifa sahihi ya anapopatikana mwananchi na utambulisho wa matumizi ya eneo husika.

Taarifa hizo zinarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma za Serikali na kijamii mahali alipo mwananchi sambamba na kuwezesha biashara mtandao (*e-Commerce*). Katika Mwaka wa Fedha 2020/21 shughuli zifuatazo katika Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi zimetetelezwa

i) Kazi ya kusimika nguzo zinazoonesha majina ya barabara, mitaa na njia na kubandika vibao vya namba za nyumba katika Jiji la Mwanza inaendelea kufanyika. Aidha, kazi ya ubandikaji wa vibao vya namba za nyumba inaendelea kufanyika katika Halmashauri 11 za Majiji ya Dodoma (Kata 7) na Tanga (kata 5); Manispaa za Ilmela (kata 3), Shinyanga (kata 4), Morogoro (kata 7) na Moshi (kata 9); Wilaya za Chato (kata 2), Chamwino (kata 1) na Bahi (kata 1) pamoja na Miji ya Geita (kata 1) na Kibaha (kata 3);

ii) Ramani (*shape files*) za Majiji ya Halmashauri tisa (9) zimeandaliwa. Halmashauri hizo ni Jiji la Dar es salaam, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Kigamboni, Manispaa ya Temeke, Manispaa ya Ubungo, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha, Jiji la Mwanza, Jiji la Dodoma na Jiji la Mbeya;

iii) Programu tumizi (*Mobile App*) ya kutumia simu za mkononi imeandaliwa ambayo itaongeza ufanisi katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi. Programu tumizi husika itawezesha kukusanya taarifa za barabara na mitaa, makazi na wakazi sambamba na kuonesha maeneo husika;

iv) Kazi ya kukusanya taarifa za makazi na wakazi kwa kutumia programu tumizi (*Mobile App*) inaendelea katika Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na Halmashauri. Maandalizi ya kukusanya taarifa katika majiji ya Arusha na Tanga yanaendelea;

v) Mkakati wa kuharakisha utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi kwa kipindi cha mwaka 2021-2025 umeandaliwa; vi) Mafunzo ya GIS, GPS, *Database & Map Development* yametolewa kwa wataalam watano (5) wa Wizara ili kuwawezesha kutekeleza mradi;

vi) Wataalam 36 wa Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mwanza na Tanga wamejengewa uwezo wa kutekeleza mradi; na

vii) Viongozi na watendaji **813** wa Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mwanza na Tanga wamejengewa uelewa kuhusu mradi.

### **Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

34. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 425,890,138,007**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Taasisi zimekusanya jumla ya **Shilingi 284,825,394,121.99** sawa na asilimia 66.9 ya lengo.

35. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

### **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

36. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 144,287,198,711**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Mamlaka ilifanikiwa kukusanya **Shilingi 129,701,867,649** sawa na **asilimia 89.9** ya makadirio ya mwaka. Vyanzo vya mapato ya Mamlaka ni pamoja na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (asilimia moja ya pato ghafi ya watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo kutokana na mtambo wa *Teletraffic Management System (TTMS)*.

37. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia Mfumo wa *Teletraffic Management System (TTMS)* wenye uwezo wa kubaini takwimu mbalimbali zinazopita katika mitandao ya mawasiliano nchini. Mfumo huu unaiwezesha Serikali kupata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano.

38. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2021, Mamlaka ya Mawasiliano kupitia mfumo wa TTMS imefanya yafuatayo:-

i) Kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao, ambapo jumla ya miamala **2,860,988,609** ilifanyika kupitia mitandao ya simu na kiasi cha **Shilingi 170,513,110,859,867** kilipita kwenye miamala ya simu katika kipindi hicho;

ii) Kuzuia mianya ya upotevu wa mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazolingia hapa nchini ambapo jumla ya simu za ulaghai zipatazo **3,165** zilibainika. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilifanya kaguzi nane (**8**) kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Songwe na kuwezesha kukamata vifaa vya uchepushaji wa mawasiliano ya simu za kimataifa kumi (10) na kukamata watu kumi na tatu (13) waliokuwa wakijihusisha na uchepushaji huo. Wahalifu wote walifikishwa kwenye vyombo vya sheria na kesi zao zinaendelea kusikilizwa mahakamani.

iii) Mfumo wa TTMS umewezesha Serikali kupata mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazolingia na kuishia hapa nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 4,203,129,015.05** kiliwasilishwa Hazina. Vilevile, jumla ya **Shilingi 1,401,043,005.02** zilibakia TCRA kwa ajili ya kuendesha na kuboresha Mfumo;

iv) Mfumo umewezesha kuzuia matumizi ya simu zilizoripotiwa kuibiwa, kupotea, kufanya ulaghai au kuharibika pamoja na kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango. Jumla ya simu **943,554** zikiwemo sisizo na viwango na zenye namba tambulishi zilizonakiliwa (*Duplicate International Mobile Equipment Identity - Duplicate IMEIs*) zimebainika na kufungiwa.

39. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuendesha na kuboresha kanzidata ya usajili wa laini za simu kwa njia ya kibiometria nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, jumla ya laini za simu

zilizosajiliwa kibiometria ni **51,108,886**; laini za simu ambazo zimesajiliwa kwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi na kitambulisho cha Mpiga Kura ni **1,954,199**, hivyo kufanya jumla ya laini ambazo zimeunganishwa na mtandao kufikia **53,063,085**. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya laini za simu **8,436,805** zimesajiliwa ambapo ni ongezeko la asilimia **18.9** kutoka laini **44,626,280**.

40. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kukabiliana na changamoto zinazotokana na ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hapa nchini. Mamlaka ya Mawasiliano kwa kutumia *National Computer Emergency Response Team (TZ-CERT)* imeendelea kukabiliana na majanga yatokanayo na Kompyuta na mifumo ya Mawasiliano. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 Serikali kupitia TCRA imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kutoa mafunzo juu ya usalama wa mifumo kwa wasimamizi wa mifumo kutoka taasisi mbalimbali nchini. Pia, imefanya tathmini ya hatari na matishio ya kiusalama ya mifumo ya kompyuta na mtandao kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyopo dhidi ya mashambulio ya mtandao (*cyber-attacks*) ambapo tahadhari za usalama (*security alert*) **278**; mashauri (*security advisories*) 416 na taarifa kwa umma (*public notice*) nne (4) za kiusalama zilitolewa ili hatua stahiki ziweze kuchukulia kuimarisha usalama wa mtandao na mifumo; na

ii) Kutoa mafunzo kwa washiriki **432** wa taasisi mbalimbali juu ya usalama wa mifumo na miundombinu (*ICT systems security, Network & Systems monitoring*) usalama wa majina ya kikoa yaani *Domain Name System (DNS)* na *Domain Name System Security Extension (DNSSEC)* na mafunzo kwa vitendo juu ya ufanyaji tathmini ya hatari na matishio ya kiusalama ya mifumo. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano imetoa mafunzo ya elimu ya usalama mtandaoni kwa taasisi **17** za umma ambapo jumla ya wafanyakazi **2,204** walihudhuria mafunzo hayo.

41. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na jukumu la kukagua na kuhakiki ubora wa viwango vya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki hapa nchini kwa lengo la kulinda usalama na afya za wananchi. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi kufikia Aprili, 2021 jumla ya maombi **618** yamepokelewa kwa ajili ya uhakiki wa ubora na usalama wa matumizi ya vifaa vya kielektroniki. Kati ya hayo, maombi **445** yamekaguliwa na kukidhi vigezo vya ubora na usalama kwa matumizi, maombi **155** yako kwenye hatua za mwisho za ukaguzi na maombi **20** yamekataliwa.

42. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea kuhakikisha uwepo wa rasilimali zinazowezesha mawasiliano ya simu, intaneti, redio na runinga. Rasilimali hizi ni pamoja na masafa, namba na viko. Usimamizi mzuri wa rasilimali hizi umewezesha kuhakikisha kuwa hakuna mwingiliano katika huduma na kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Usimamizi wa rasilimali hizi umetokana na:-

i) Uwepo wa nyenzo za kisasa pamoja na Sera, Sheria na Kanuni zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya nchi hivyo kuwezesha upangaji mzuri wa rasilimali za mawasiliano; na

ii) Upangaji na usimamizi mzuri wa rasilimali za mawasiliano (masafa na namba), umewezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano pamoja na huduma za pesa mtandao. Mamlaka ya Mawasiliano hupanga na kutoa namba zinazotumika katika mawasiliano pamoja na namba fupi (short codes) zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha.

43. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuhimiza matumizi ya kikoa cha kitaifa cha *dot tz (country code Top Level Domain - cc-TLD)* ambacho ni rasilimali muhimu ya Taifa kwenye mawasiliano ya intaneti kama ilivyo namba +255 kwenye

mawasiliano. Mamlaka ya Mawasiliano inapanga na kuratibu matumizi ya kikoa hiki nchini kwa ajili ya kutumika kwenye anwani za kielektroniki kwenye mawasiliano ya intaneti mfano tovuti au barua pepe. Anwani zenye kikoa cha kitaifa zinasaidia:-

i) Kutoa utambulisho wa kitanzania kwenye mtandao (*cyber space*);

ii) Kuongeza uhakika na usalama kwenye matumizi ya mtandao;

iii) Masuala ya kibiashara ya kikoa cha kitaifa yanatatuliwa na sheria zetu tofauti na vikoa vingine kama "*dot com*"; na

iv) Kupatikana kirahisi kwenye search engines kama *Google*.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 anwani za kikoa cha kitaifa **2,042** zimesajiliwa na hivyo kufanya jumla ya anwani za kikoa kuongeze ka kutoka **19,776** mwezi Julai, **2020** na kufikia anwani za kikoa **21,818** mwezi Aprili, 2021.

45. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) kwa kutoa elimu juu ya sheria, haki na wajibu wa mtumiaji, uhakiki wa usajili wa laini za simu za mkononi, wajibu wa mtumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao na kufanikisha ufumbuzi wa malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma za Mawasiliano.

46. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeweka utaratibu mahsus wa kushughulikia malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma. Vile vile, mamlaka ya Mawasiliano inaendelea kutoa elimu juu ya wajibu na haki za watumiaji na watoa huduma za mawasiliano. Kuanzia Julai, 2020 hadi kufikia Aprili, 2021, Mamlaka ilikuwa imepokea na kushughulikia jumla ya malalamiko **508**.



47. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia sheria na kuboresha mfumo wa utoaji leseni ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kutoa leseni za kimtandao. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya Leseni **1,572** zimetolewa. Leseni ambazo zimetolewa zinajumuisha leseni za mawasiliano ya redio (*radio communication stations*) **123**, leseni za maudhui ya redio na ya televisheni **20**, leseni ya maudhui mtandao **151**, leseni za madaraja mbalimbali (*class licences*) **1,274**, leseni za huduma za mawasiliano (*application service licences*) **4**.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ambazo zimeendelea kufanyika ni pamoja na ukaguzi wa matumizi ya masafa ili kuhakikisha kuwa yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Zoezi hili linafanyika kuhakikisha watoa huduma wa mawasiliano wamezingatia matumizi ya masafa ya mawasiliano (*radio frequency*) kulingana na leseni walizopewa. Hili linafanyika kulingana na upangaji masafa wa Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Simu Duniani (*International Telecommunications Union*).

49. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kufanya tathmini ya gharama za huduma za mawasiliano pamoja na kuwashirikisha wadau muhimu ili iweze kuchukua hatua stahiki zinazolenga kuhakikisha kuwa mahitaji ya wadau wa pande zote (Serikali, watoa huduma na watumiaji wa huduma) yanafikiwa kupitia huduma husika.

## **Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

### **(a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Pan African Postal Union (PAPU House)**

50. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeanza ujenzi wa Jengo la Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union) (PAPU House) jijini

Arusha lenye ghorofa 16. Ujenzi huu unakadiriwa kugharimu **Shilingi 39,706,626,131.05**. Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania (**asilimia 40**) na Umoja wa Posta Afrika (**asilimia 60**). Jengo hili litatumika kama Makao Makuu ya Shirika la Posta la Afrika na Ofisi za Kanda ya Kaskazini za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022.

#### **(b) Mradi wa vifaa vya TEHAMA Mashuleni**

51. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa kufadhili vifaa vya TEHAMA mashuleni ili kuwezesha wanafunzi na walimu kutumia mifumo ya TEHAMA kupata taarifa za masomo kwenye tovuti mbalimbali duniani. Kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, TCRA imenunua vifaa vya TEHAMA kwenye shule mbili (2) zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni Kompyuta **23**, Printa **moja** yenye uwezo wa kuchapisha maandishi ya nukta nundu. Shule hizi ni Sekondari ya Moshi (Kilimanjaro) na Sekondari ya Mabira (Kagera).

#### **(c) Mradi wa kutoa Elimu kwa Umma**

52. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa kuelimisha wananchi masu ala yanayohusiana na Sekta ya Mawasiliano kupitia vipindi vya redio na runinga. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 TCRA imerusha vipindi **832** vya Elimu kwa Umma.

#### **Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

53. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Shirika lilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 199,225,826,248**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 Shirika lilifanikiwa kukusanya **Shilingi 101,703,349,616.25** sawa na **asilimia 51** ya makadirio ya mwaka kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

54. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanya upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili (*Core Network Systems*), Usafirishaji wa Data (*Transmission/Transport Networks*) na mawasiliano ya Simu za Mkononi (*Radio Access Network*). Hatua hii imewezesha Shirika kuongeza uwezo wake katika kutoa huduma.

55. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanikiwa kuongeza wateja kutoka wateja **701,262** mwezi Julai, 2020 hadi kufikia wateja **1,215,762** mwezi Aprili, 2021. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 45.2** ya lengo na hivyo kulifanya Shirika kumiliki asilimia 2 ya soko la mawasiliano. Aidha, Shirika linatarajia kufikisha wateja **1,839,905** ifikapo mwezi Juni, 2021.

56. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kuimarisha mkakati wa uuzaji na usambazaji wa muda wa maongezi. Sambamba na maduka yaliyopo katika ofisi za Shirika la Mawasiliano nchi nzima, Shirika limeendelea kuboresha upatikanaji wa muda wa maongezi kwa:-

i) Kuongeza idadi ya wasambazaji wa vocha kutoka **6,836** mwezi Julai, 2020 hadi kufikia wasambazaji **7,414** mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 8.5**;

ii) Kuwaelimisha na kuwaunganisha wateja wake na huduma ya T-PESA ili waweze kununua muda wa maongezi kwa njia ya kielektroniki kupitia T-PESA na benki pindi wanapohitaji kununua muda wa maongezi bila kufika ofisi za Shirika au Wakala; na

iii) Shirika limeingia makubaliano na Shirika la Posta kwa ajili ya kutoa huduma za uwakala mkuu wa T-PESA, usambazaji wa vocha na usajili wa wateja wapya wa TTCL. Hivyo, huduma za TTCL zinapatikana kila palipo na ofisi za Shirika la Posta

57. **Mheshimiwa Spika**, Shirika linaendelea kufanya maboresho ili kuhakikisha huduma linazotoa zinakidhi viwango kwa kuboresha mitambo na kuongeza vituo vya huduma kwa wateja. Kwa upande wa huduma kwa wateja

maboresho haya ni kama ifuatavyo: kuhakikisha kituo cha huduma kwa wateja (*call center*) kinakuwa thabiti na kupatikana ndani ya muda stahiki; T-PESA imeanzisha namba maalum ya kupiga bure (*toll free number*) **0800 110095** kwa ajili ya kuwahudumia Mawakala wake ili kupunguza msongamano na kuchelewesha kupata huduma kwa wakati; kuongeza vituo vya huduma kwa wateja (*customer service centers*) katika mikoa na wilaya ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kote nchini kwa ukaribu zaidi.

58. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limebuni huduma ya T-HAKIKI inayoweza kuthibitisha ubora wa mbegu na viuatilifu. Huduma hii inalenga kuwasaidia wakulima kubaini mbegu na viuatilifu visivyokidhi viwango au vilivyopitwa na muda wa matumizi. Huduma hii ni bure na inatumiwa na wakulima, taasisi za udhibiti ubora wa pembejeo za kilimo na wauzaji wa mbegu na kemikali za kilimo. Hivyo, watumiaji wote wa simu za mkononi waliosajiliwa nchini wanaweza kuhakiki ubora wa pembejeo kupitia namba **\*148\*52#**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 huduma imekuwa na watumiaji **12,291**. Shirika linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kutumia huduma hii.

59. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kutoa huduma za data kwa wateja wakubwa, wa kati na wadogo. Vilevile, Shirika linatoa huduma ya njia ya mawasiliano (*capacity service*) na huduma ya maunganisho (*interconnect*) nje ya nchi ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 limefanikiwa kutanua wigo wa huduma kwa wateja 5 ambao ni Airtel Malawi, Bharti Airtel ya Uingereza, MTN Global, Apelby na AT&T ya Marekani. Juhudi zinaendelea ili kupata wateja zaidi.

60. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kusimamia na kuende sha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano likiwa na vituo **27** vinavyotoa huduma za matengenezo ya kiufundi kupitia kwa wataalam wa Shirika pamoja na vituo **39** vinavyounganisha huduma za wateja waliopo ndani na nje ya nchi sita (6) za Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Kenya na Uganda kupitia vituo vilivyopo mipakani.

61. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kuendesha Kampuni Tanzu ya TTCL Pesa (T-PESA) ambapo watumiaji wa huduma za T-PESA wameongezeka kutoka wateja **466,605** mwezi Julai, 2020 hadi kufikia wateja **835,931** mwezi Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia **79**. Kwa upande wa mawakala ambao wanafanya miamala, wameongezeka kutoka mawakala **2,300** mwezi Julai, 2020 hadi kufikia mawakala **3,200** mwezi Aprili, 2021. Wateja na mawakala hawa wamekamilisha taratibu zote za kiusajili kwa mujibu wa Sheria. Aidha, T-PESA imeunganishwa kwenye Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG), mifumo ya ki-benki ya CRDB, NMB, NBC, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na watoa huduma za mawasiliano ili kumwezesha mteja kufanya malipo mbalimbali kwa kupitia T-PESA.

#### **Kituo cha Data cha Taifa (*National Internet Data Centre - NIDC*)**

62. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC) kimeanzishwa mwaka 2015 ikiwa ni sehemu ya mradi wa Mkongo wa Taifa na kina hadhi ya daraja la tatu (*tier 3*) kwenye viwango vya kimataifa. Huduma zinazotolewa na kituo ni upangishaji wa vifaa (*collocation*), upangishaji wa nafasi kwenye mashine (*virtual servers*), upangishaji wa mashine kubwa (*dedicated servers*), kutunza data kwa matumizi ya baadae (*storage and backups*), kutengeneza mifumo na huduma za kuweka tovuti za wateja zipatikane kwenye wavuti ulimwengu (*web hosting*).

63. **Mheshimiwa Spika**, Kituo kimefanikiwa kuunganisha wateja **160** ambao kinaendelea kuwahudumia toka kuanzishwa kwake, kati ya hao wateja **89** ni Taasisi na Idara za Serikali na wateja **71** ni taasisi au kampuni binafsi. Idadi hii ya wateja imepelekea kukusanya mapato ya kiasi cha **Shilingi 2,239,484,755.01** kuanzia Julai, 2020 hadi tarehe 30 Aprili, 2021.

64. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Kuhifadhi Data (NIDC) kwa kushirikiana na T-PESA kimeanzisha kadi ya malipo maalum ijulikanayo kama N-CARD inayotumiwa na wateja waliosajiliwa na mitandao yote ya simu ili kuwawezesha

watumiaji kulipia bidhaa na huduma mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 mfumo wa N-CARD una jumla ya wateja **224,106** wanaotumia kadi za N-CARD kuingia viwanja vya mpira na kwenye maonesho ya biashara na kulipia nauli za vivuko.

### **Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania**

65. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limekamilisha upanuzi wa mifumo mikuu ya mawasiliano (*Core Network Capacity Upgrade*) na uboreshaji wa vituo vya huduma vya 3G au 4G maeneo ya mijini (*3G/4G Radio Access Network Capacity Upgrade*). Miradi hii imewezesha Shirika kuongeza uwezo wa kuunganisha wateja wa 2G, 3G na 4G na kuboresha huduma za 3G/4G.

66. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limekamilisha usimikaji wa mfumo wa ankara za malipo (*billing system*) ambao unaongeza uwezo wa kuhifadhi taarifa za usajili wa wateja, kuwezesha usimamizi wa mawakala, kutengeneza na kuuza vocha na utengenezaji wa bidhaa na huduma kutokana na makundi ya wateja. Mfumo huu umeboresha utoaji huduma kwa wateja kwa kuwawezesha kuwa na huduma binafsi (*self service*) kupitia tovuti ya Shirika na umewezesha maingiliano (integration) ya mifumo ya ndani ya Shirika pamoja na mifumo ya nje inayoliwezesha Shirika kufanya biashara.

67. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limekamilisha mradi wa upanuzi wa Mkongo kwenda kwenye Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere - Rufiji. Mradi huu umeboresha huduma za mawasiliano kwenye eneo la mradi.

### **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

68. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Mfuko ulikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 32,802,183,379**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Mfuko ulifanikiwa kukusanya **Shilingi 28,698.931,101**. sawa na **asilimia 87.4** ya makadirio ya mwaka kutoka katika vyanzo vyake vinne vya mapato,

ambavyo ni ruzuku toka Serikalini, tozo ya huduma, mchango toka TCRA na wadau wa maendeleo.

### **Miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini**

69. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano katika Mwaka wa Fedha 2020/21, imeendelea na zoezi la ufikishaji wa huduma ya mawasiliano vijijini ambapo mikataba ya kufikisha huduma za Mawasiliano ifikapo mwezi Oktoba, 2021 katika kata **61** zenye jumla ya vijiji **173** imesainiwa. Aidha, kukamilika kwa miradi katika kata hizo kunafanya huduma za mawasiliano kufika katika kata **1,057** zenye vijiji **3,292** na wakazi zaidi ya **milioni 12**.

70. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mitatu (3) ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini. Miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea ni pamoja na mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano vijijini katika maeneo ya mipakani na Kanda Maalum Awamu ya Tano. Mradi huu una kata **33** zenye vijiji **53** na wakazi wapatao **368,000** na unatekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Kata **2** kati ya kata **33** tayari zimefikishiwa huduma ya mawasiliano na kata **31** zilizobaki zinatarajiwa kufikishiwa mawasiliano ifikapo mwezi Septemba, 2021.

71. *Mheshimiwa Spika*, mradi mwingine tunaoendelea kutekeleza ni wa kufikisha huduma za mawasiliano vijijini Awamu ya Tatu ambao una jumla ya kata **177** zenye vijiji **373** na wakazi wapatao **1,836,000**. Aidha, kata **117** zimekwisha fikishiwa huduma za mawasiliano na kata **60** zilizobakia zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2021.

72. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unaendelea na utekelezaji wa Mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano vijijini Awamu ya Nne wenye kata **252** na vijiji **555**. Kata **63** zenye vijiji **197** na wakazi wapatao **790,000** zimekwisha pata huduma za mawasiliano na kata zilizobakia zinatarajia kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2021.

73. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuwasimamia wakandarasi ili wakamilishe miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika vijiji vyote vilivyobaki.

**b) Mradi wa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha shule na mtandao wa intaneti**

74. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetekeleza mradi wa kuunganisha mtandao wa intaneti na kutoa vifaa vya TEHAMA kwa shule za umma **151**. Vifaa vilivyotolewa kwa kila shule ni kompyuta 5 na printa 1. Mfuko umetekeleza mradi huu kwa ushirikiano na kampuni ya simu ya Vodacom kupitia shirika lake la Vodacom Foundation. Aidha, Serikali inaendelea kuunganisha shule nyingine **100** za umma na mtandao wa intaneti na kuzipatia kompyuta 5 na printa 1 kila shule.

**c) Kituo cha “Call Centre” Zanzibar**

75. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mfuko inatekeleza mradi wa kujenga kituo cha “call center” Zanzibar, ambacho kitakuwa mahsusi kwa wananchi wa Zanzibar kutoa taarifa za matukio ikiwa ni pamoja na taarifa za maafa kama vile moto na magonjwa ya milipuko. Kituo hicho kitatumia Mfumo ambao utaruhusu wananchi kupiga simu hadi kufikia **500** kwa wakati mmoja na hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kuweza kutoa taarifa za majanga au maafa wakati wowote. Mradi huu unatekelezwa na Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2021.

**d) Mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu**

76. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imetekeleza mradi wa kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa **Walimu 601**, kati yao **Walimu 88** wanatoka Zanzibar na **Walimu 513** wanatoka Tanzania Bara. Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Disemba, 2020 katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT). Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea Walimu uwezo wa kutatua changamoto ndogondogo za kiufundi katika vifaa vya TEHAMA vikiwemo printa na kompyuta.



**e) Mradi wa Tiba Mtandao**

77. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuwezesha mradi wa Tiba Mtandao ambapo Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Mifupa MOI zimeunganishwa na hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro kwa njia ya mtandao. Mradi huu unalenga kuwawezesha wagonjwa kutoka katika hospitali za pembezoni kupata huduma za kibingwa kutoka katika hospitali za taifa. Uunganishwaji unaendelea kwa hospitali za rufaa za Ruvuma, Tanga na Katavi. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni, 2021.

**f) Ujenzi wa Studio ya TBC Dodoma**

78. *Mheshimiwa Spika*, usikivu wa redio ni jukumu ambalo pia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umekasimiwa ili kuhakikisha Watanzania walioko katika maeneo yote wanaweza kupata usikivu wa redio kutoka nchini kwao. Serikali imetekeleza mradi wa kuhuisha studio ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) iliyoko Dodoma kazi zilizofanyika ni pamoja na ufungwaji wa mifumo ya umeme pamoja na kufunga vifaa vya studio. Kazi iliyobaki ni kufanya majaribio ili kupima utendaji kazi wa studio kabla ya kuanza kazi rasmi. Mradi huu unatarajiwa kuzinduliwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2021.

**g) Uboreshaji wa Usikivu wa Matangazo ya TBC Redio Kisaki, Morogoro**

79. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imetekeleza mradi wa kuboresha usikivu wa matangazo ya redio ya TBC katika eneo la mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere kwa kujenga kituo cha kurushia matangazo ya redio katika Mkoa wa Morogoro eneo la Kisaki. Kituo kinatarajiwa kuwashwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2021.

**h) Uboreshaji wa Matangazo ya TBC katika maeneo ya Mipakani**

80. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imetekeleza mradi wa kuboresha matangazo ya redio ya Taifa ya TBC katika

maeneo ya wilaya za mipakani na yenye usikivu hafifu wa redio. Maeneo hayo yaliconufaika na mradi huu ni pamoja na Ngara katika Mkoa wa Kagera, Mlimba katika mkoa wa Morogoro, Kyela katika mkoa wa Mbeya, Ludewa katika mkoa wa Njombe na Ruangwa katika mkoa wa Lindi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

### **Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

81. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Shirika lilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 45,099,221,247**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Shirika lilifanikiwa kukusanya **Shilingi 24,604,394,870** sawa na **asilimia 54.6** ya makadirio ya mwaka kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni usafirishaji wa barua, Usafirishaji wa nyaraka kwa njia ya haraka (EMS), fedha na uwakala, biashara mtandao pamoja na miliki.

82. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Shirika limefanikiwa kununua magari makubwa matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 30 kila moja na pikipiki hamsini (50) kwa ajili ya kusafirishia mizigo ikiwemo barua, nyaraka, vifurushi na vipeto.

83. ***Mheshimiwa Spika***, katika uboreshaji wa utoaji wa huduma Shirika limefanikiwa kufanya ukarabati na ubadilishaji wa muonekano wa majengo matatu (3) ya Posta kuu za Mikoa ya Mbeya, Lindi na Singida ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa lengo la kuvutia wateja.

84. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, Shirika limefanikiwa kutengeneza mfumo wa *Posta Management Information System (PMIS)* ambao umeunganishwa katika ofisi zote zinazotoa huduma za Posta za msingi. Mfumo huu unawezesha mteja kufuatilia mlolongo wa usafirishaji wa barua, nyaraka, vifurushi na vipeto.

85. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limeunganisha Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Posta (*Posta Revenue Collection*

*System*) na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuwezesha kutumia vifaa vya kielektroniki vya kufanyia mauzo (*Point of Sale - POS*) katika maeneo ya kutolea huduma za Posta.

86. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kutoa huduma za Posta Mlangoni katika maeneo yenye miundombinu ya Anwani za Makazi na Postikodi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Geita, Pwani pamoja na Zanzibar. Shirika pia linatoa huduma ya Posta Mlangoni kwa mahakama zote za Tanzania Bara.

87. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limekasimiwa jukumu la kusimamia na kuendesha vituo vya Huduma Pamoja kupitia mradi wa Tanzania ya kidigitali. Hadi kufikia mwezi Juni, 2021 vituo viwili vitaanza kutoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma kwa kutoa huduma zifuatazo;

- a) Cheti cha kuzaliwa - RITA;
- b) Hati ya kusafiria (*Passsport*) - UHAMIAJI;
- c) Kitambulisho cha Taifa - NIDA;
- d) Usaji wa kampuni za Biashara - BRELA;
- e) Namba ya Mlipa Kodi (TIN) - TRA;
- f) Leseni za Biashara za Halmashauri - Halmashauri ya Ilala, Kigamboni, Kinondoni na Temeke;
- g) Bima ya afya - NHIF; na
- h) Taarifa za pensheni ya uzeeni – PSSSF na NSSF.

### **Tume ya TEHAMA (ICTC)**

88. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Tume ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,232,897,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Tume ilifanikiwa kukusanya **Shilingi**

**317,590,260.74** sawa na asilimia 25.7 ya makadirio ya mwaka kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mgao kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ada za usajili wa Wataalam wa TEHAMA na wadau na washirika wa maendeleo.

89. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka Fedha 2020/21, Wizara imetoa Mwongozo wa Kusajili Wataalam wa TEHAMA kwa lengo la kuwatambua na kuwaendeleza. Usajili wa wataalam wa TEHAMA ulizinduliwa rasmi tarehe 7 Oktoba, 2020 ambapo tukio hilo lilienda sambamba na kukabidhiwa vyeti vya usajili wataalam wa TEHAMA **100**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya wataalam wa TEHAMA waliokuwa wamesajiliwa ni **415** sawa na **asilimia 52** ya lengo la kusajili wataalam **800** kwa mwaka.

90. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Tume ya TEHAMA imeandaa na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA katika maeneo yenye upungufu wa utaalam wa TEHAMA. Tume imeratibu na kuwezesha mafunzo ya usimamizi miradi ya TEHAMA kwa wataalam wa TEHAMA hamsini (50) yaliyofanyika Bagamoyo mwezi Aprili, 2021. Mafunzo haya yamewapatia ujuzi wataalam wa TEHAMA katika kusimamia kwa ufanisi miradi ya TEHAMA katika maeneo wanayofanyia kazi.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika eneo la utafiti, Tume imefanya tathmini ya kubaini maeneo ya ujuzi wa taaluma ya TEHAMA unaohitajika nchini (*ICT Skills gap analysis*). Utafiti umebaini kwamba maeneo ya ujuzi wa TEHAMA yanayohitajika zaidi nchini ni *“Big Data Analytics, Cloud Computing Management and Security, Cyber Security, Systems and Software development na Evolving Digital Technologies”*. Utafiti huu umeiwezesha Tume ya TEHAMA kutengeneza Muundo wa kuendeleza ujuzi wa TEHAMA nchini unaotambua makundi matatu ya ujuzi ambayo ni ujuzi wa msingi, ujuzi wa kati wa kidijitali na ujuzi wa juu wa kidijitali. Kadhalika, Mfumo unawianisha ujuzi wa TEHAMA na maeneo ya kazi katika soko la ajira. Mfumo huu unaiwezesha Wizara kupitia Tume kutambua viwango na ubora wa ujuzi unaotolewa na kupatikana nchini.

92. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na maendeleo ya TEHAMA yaliyopelekea kuimarika kwa biashara mtandao (*e-commerce*) duniani, Tume ya TEHAMA katika mwaka huu wa fedha imefanya tathmini ya kubaini fursa za TEHAMA kwa maendeleo ya sekta ndogo ya Posta ili inufaike na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya nchi.

93. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuendeleza TEHAMA nchini, Tume imeendelea kuratibu na kuwezesha yafuatayo:

i) Kuandaa Kongamano la Nne la mwaka la TEHAMA nchini (*4th Tanzania Annual ICT Conference - TAIC*) lililofanyika mwezi Oktoba, 2020 na kuhudhuriwa na washiriki 640 kutoka taasisi 116 za sekta ya umma na binafsi. Kupitia kongamano hilo, watalaam wa TEHAMA wameendelea kujengewa uwezo, kufanya maonesho ya huduma za TEHAMA zinazoendana na mapinduzi ya nne ya Viwanda (*4th Industrial Revolution*) na kujadili kuhusu fursa na changamoto kuelekea mapinduzi ya nne ya viwanda;

ii) Wizara kupitia Tume ya TEHAMA iliandaa Jukwaa la Pili la Usalama wa Mitandao ambalo lilifanyika mwezi Februari, 2021 na kuhudhuriwa na washiriki 206. Washiriki walijengewa uwezo wa mbinu mpya za kitaalam za kukabiliana na matishio ya usalama wa mitandao; na

iii) Tume ya TEHAMA kupitia programu ya kuendeleza wabunifu TEHAMA inayoitwa Softcenter kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia maendeleo ya Mitaji (*UN Capital Development Fund*) na Shirika la *Digital Opportunity Trust (DOT)* imewezesha mkutano wa wadau wa ubunifu wa TEHAMA 170. Mkutano huu uliazimia kuwa Serikali iwatambue na kuanzisha kanzidata yenye taarifa zao ili kuweza kuwaendeleza na kulinda kazi za wabunifu chipukizi katika TEHAMA. Utengenezaji wa kanzidata umeshaanza na itazinduliwa tarehe 18 Juni, 2021.

94. **Mheshimiwa Spika**, kupitia kituo cha kuendeleza kampuni chipukizi cha Softcenter, Tume imesajili miradi miwili (2) ya wajasiriamali ambayo ni: Mradi wa mfumo wa TEHAMA wa

elimu kwa njia ya mtandao, Mradi wa kufundishia, kujifunzia na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi katika shule za Sekondari. Aidha, Tume imeanza maandalizi ya mradi wa ujenzi wa kituo cha kuendeleza utaalum wa TEHAMA (*National Center for ICT Research and Professionals Development*).

### **Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania (TCRA CCC)**

95. *Mheshimiwa Spika*, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano. Chanzo kikuu cha mapato ya Baraza ni ruzuku kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Baraza limepokea **Shilingi 300,000,000** sawa na **asilimia 75** ya ruzuku toka TCRA.

96. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Baraza limeendelea kuhamasisha na kuchukua maoni ya watumiaji wa huduma za mawasiliano. Baraza kupitia Kamati za Watumiaji za mikoa katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba limehamasisha, limeshauriana na kupokea maoni kwa watumiaji **14,964**. Aidha, katika maadhimisho ya Nanenane Kamati za Watumiaji katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Mbeya na Mjini Magharibi zilihamasisha watumiaji **10,000** kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano. Wawakilishi wa watumiaji kutoka makundi ya watu wenye ulemavu, wajasiriamali, wanawake, vijana na waandishi wa vyombo vya habari walishirikishwa.

97. *Mheshimiwa Spika*, Baraza kupitia vyombo vya habari ikiwemo; redio, magazeti, blogu, runinga mtandao, tovuti na kurasa zake za mitandao ya kijamii limeendelea kutoa elimu na kuhamasisha pamoja na kupokea maoni kutoka kwa watumiaji. Aidha, kwa kutumia video fupifupi zinazorushwa katika mabasi yaendayo mikoani na katika vyombo vya usafiri wa majini vya Azam watumiaji **1,686,000** wamepata elimu juu ya haki, wajibu, utaratibu wa kuwasilisha malalamiko, na

matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

### **C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

#### **Makadirio ya Mapato ya Wizara**

98. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 50,000,000,000** ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

#### **Malengo ya Bajeti ya Wizara**

##### **Eneo la Mawasiliano**

99. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

i) Kukamilisha kazi ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta na maandalizi ya Mkakati wake wa Utekelezaji;

ii) Kukamilisha maboresho ya Sheria ya Shirika la Posta Tanzania ya mwaka 1993, Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 na Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ya mwaka 2006 na Kanuni zake;

iii) Kuandaa Mkakati mpya wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016 wa Mwaka 2022 hadi 2024; iv) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watoa huduma za mawasiliano ya Simu na Posta;

v) Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa Sekta Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

vi) Kuboresha upatikanaji huduma za mawasiliano ya simu zenye intaneti ya kasi (*broadband*) na huduma za Posta ili kufikia wananchi wote;

vii) Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha vifaa vya TEHAMA;

viii) Kuandaa ramani ya kidijitali kwa ajili ya usafirishaji na ufuatiliaji (*Digital Delivery Map*);

ix) Kutekeleza mradi wa Tanzania ya Kidijitali ambao unatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia, ambapo shughuli zifuatazo zitatekelezwa;

a) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Huduma Pamoja (*One Stop Center*);

b) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Biashara Mtandao (*e-Commerce*) kupitia miundombinu ya Shirika la Posta; na

c) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa *ICT Innovation and Softcenter*.

## **Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

100. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatarajia kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i) Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kufikia maeneo ya Wilayani kwa jumla ya Kilomita 1,880; ambapo Ofisi za Halmashauri 17 pamoja na Taasisi nyingine zitaunganishwa na miundombinu ya mtandao wa kasi (*broadband infrastructures*);

ii) Kupanua uwezo wa mkongo kutoka Gigabit 200 (200G) hadi Gigabit 400 (400G);

iii) Kuratibu ukamilishaji wa utungwaji wa Sheria ya TEHAMA na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (*Personal Data Protection Act*);

iv) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;



v) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao (*National Cyber Security Strategy*);

vi) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mtandao wa TEHAMA wenye kasi (*National Broadband Strategy*); vii) Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Wakala wa kusimamia, kuendesha na kuendeleza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

vii) Kuandaa mkakati wa kujenga uwezo kwa wataalamu kwenye maeneo ya TEHAMA yenye uhaba wa ujuzi nchini;

ix) Kuratibu ujenzi na uboreshaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA nchini (*National IT Systems*) na kuunda na kusimamia Mifumo ya TEHAMA ndani ya Wizara; na

x) Kuweka utaratibu wa kuwezesha upatikanaji wa huduma za intaneti kwa gharama nafuu katika maeneo ya huduma za kijamii.

## **Miradi Itakayotekelezwa na Wizara**

### **I: Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

101. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano itaendelea kufanyika kwa lengo la kupanua uwezo wa Mkongo wa Taifa kutoka Gigabit 200 (200G) na kufikia ukubwa wa Gigabit 400 (400G). Aidha, Serikali itajenga jumla ya Kilomita 1,880 za Mkongo katika maeneo Musoma-Simiyu-Shinyanga (Kilomita 304), Tabora-Uvinza (Kilomita 315), Manyoni-Mbeya (Kilomita 529), Babati-Dodoma (Kilomita 270), Chato-Bwanga (Kilomita 60), Isaka-Kahama (Kilomita 42) na Ifakara-Mlimba-Songea (Kilomita 360). Mradi huu utajumuisha ujenzi wa Vituo vipya **17** vya kutolea huduma za Mkongo ili kuogeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi kufikisha ngazi za Wilaya nchini.

102. **Mheshimiwa Spika**, shughuli nyingine zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu ni:

- i) Kusimamia utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali ambao unajumuisha utekelezaji wa miradi midogo midogo ya Taasisi za Serikali kwa kufanya maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kufikisha huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa Wananchi.
- ii) Kusimamia matumizi ya kidigitali na ujenzi wa miundombinu ya Mkongo kwa watumiaji wa mwisho (*last mile connectivity*) kwenye Vituo vya Afya, Ofisi za Serikali na Shule zote nchini;
- iii) Kusimamia Ujenzi wa Miundombinu ya sainsi za kielektroniki (*National Public Key Infrastructure - (NPKI)*);
- iv) Kufanya tathmini na kujenga mfumo wa kijamii (*social network*) kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi;
- v) Kujenga uwezo kwa wataalamu kwenye maeneo ya TEHAMA yenye upungufu wa utaalam;
- vi) Kuwezesha utendaji kazi wa Kamati za kiufundi kwa ajili ya usimamizi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa; na
- vii) Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni.

## **II: Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi**

103. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 45,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi katika Halmashauri **17**. Halmashauri hizo ni pamoja na Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha, Jiji la Mwanza, Jiji la Dodoma na Jiji la Mbeya; Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Kigamboni, Manispaa ya Temeke, Manispaa ya Ubungo, Manispaa ya Bukoba, Manispaa ya Mtwara Mikindani, Manispaa ya Tabora, Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mjini, Halmashauri ya Magharibi "B", Halmashauri ya Chakechake na Halmashauri ya Wete. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na Kuweka muundombinu wa mfumo wa anwani za makazi na postikodi, kukusanya taarifa za barabara, nyumba na mitaa na kutengeneza na kuhuisha ramani.

104. **Mheshimiwa Spika**, shughuli nyingine zitakazotekelezwa katika Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi ni:

i) Kuhabarisha na kuhamasisha umma kuhusu umuhimu, manufaa na matumizi ya mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi; ii) Kujenga uwezo kwa viongozi na wataalam nchini kwa kuwapatia mafunzo kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi;

iii) Kuwezesha utungwaji wa sera, sheria ndogo na miongozo itakayowezesha utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi;

iv) Kuboresha kanzidata na programu za TEHAMA za Mfumo ambazo zitawezesha kuharakisha na kurahisisha utekelezaji na matumizi ya Mfumo; na

v) Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa Mfumo.

### **III: Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania)**

105. **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unalenga kuleta mabadiliko ya Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali (*Digital Economy*). Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo (SMEs na SMMEs); kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya Serikali na waliopo nje ya Serikali; na kuongeza uwezo wa utoaji wa Huduma za Serikali kwa kuwezesha uwepo wa Intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya Serikali ili kumnufaisha Mwananchi.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 25,000,000,000 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kujenga kituo kimoja cha kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitatu (3) kwenye majiji ya Mbeya,

Mwanza na Arusha; ii) Kuwezesha usanifu wa mitambo na vifaa ili kuboresha na kujenga mtandao wa huduma za Serikali wenye usalama zaidi;

iii) Kuwezesha ununuzi wa *bandwidth* kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali;

iv) Kununua vifaa na kuboresha Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (NIDC);

v) Kufanya ujenzi na ukarabati wa vituo 10 vya Huduma Jamii;

vi) Kujenga mfumo wa kitaifa utakaorahisha ukusanyaji wa takwimu za TEHAMA;

vii) Kujenga, Kupanua na kuboresha miundombinu iliyopo ya broadband inayomilikiwa na Serikali (GovNET);

viii) Kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua (*refurbishment*) ya vifaa vya TEHAMA katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza; ix) Kujenga minara ya mawasiliano 150 kwenye kata 150 ili kuwezesha huduma za *broadband* nchini;

x) Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali za TEHAMA;

xi) Kujenga uwezo kwa wataalam 50 wa TEHAMA nchini; na

xii) Kufanya usanifu na kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

### **Mipango ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

107. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zimekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 424,412,283,968.65** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Mchanganuo wa makusanyo na shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

108. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 150,067,415,286.65** ambazo zitatokana vyanzo mbalimbali vikiwemo ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (asilimia 1 ya pato ghafi ya watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo kutokana na mtambo wa TTMS.

109. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ukaguzi wa ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinatolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na kwa kuzingatia masharti ya leseni;

ii) Kujenga maabara ya kukagua na kuhakiki viwango vya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki hapa nchini;

iii) Kupima na kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kutoa huduma za kiudhibiti kwa usahihi zaidi;

iv) Kufuatilia, kujibu na kuripoti matukio ya usalama wa mtandao wa kompyuta ili kupunguza mashambulizi;

v) Kufuatilia na kudhibiti gharama za vifurushi, promosheni na ofa maalum zinazotolewa na watoa huduma ili kulinda maslahi ya watumiaji;

vi) Kuendelea kusimamia utendaji wa mfumo wa TTMS na mifumo unganishi, ikiwemo Mfumo wa Uhakiki wa Mapato ya Mawasiliano ya Simu (TRAS), vii) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi za PAPU na ofisi za Kanda ya Kaskazini ya TCRA (TCRA – PAPU House) na kuanza ujenzi wa ofisi za TCRA za Kanda ya Kati, Dodoma kwa kuweka mitambo na mifumo ya udhibiti ili kupunguza gharama za kupanga majengo kwa ajili ya ofisi;

viii) Kusimamia na kuboresha kanzidata ya Anwani za Makazi na Postikodi;

ix) Kuendelea kudhibiti ulaghai katika mitandao ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka kwa miamala ya simu za kimataifa zinazolingia hapa nchini kutoka nje (*international incoming traffic*);

x) Kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao; na

xi) Kukuza na kuhakikisha usalama wa miundombinu ya mawasiliano na matumizi.

### **Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

110. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 198,040,680,322** kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

111. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika la Mawasiliano Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuendelea na upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili (*Core Network Systems*), Usafirishaji wa *Data (Transmission/Transport Networks)* na mawasiliano ya Simu za Mkononi (*Radio Access Network*);

ii) Kuongeza idadi ya wateja wa huduma za mawasiliano (simu na data) kutoka wateja **1,215,762** waliopo na kufikia wateja **1,770,071** ifikapo mwezi Juni, 2022;

iii) Kuiongezea uwezo Idara ya Biashara,Utafiti na Masoko na kuimarisha kitengo cha makusanyo kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi kama ilivyoainishwa kwenye muundo wa Shirika;

- iv) Kuboresha mbinu za kuuza na kusambaza muda wa maongezi na kuhakikisha huduma za muda wa maongezi zinawafikia watumiaji wa mtandao wa TTCL katika ngazi zote;
- v) Kuendelea kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (NIDC);
- vi) Kuendelea kuendesha kampuni tanzu ya TTCL Pesa (T-PESA) kwa kutekeleza yafuatayo;
  - a) Kuongeza idadi ya mawakala wa T-PESA kutoka **11,402** hadi kufikia mawakala **18,000** ifikapo Juni, 2022;
  - b) Kuongeza wigo wa watumiaji wa T-PESA kutoka watumiaji **835,931** hadi watumiaji **1,500,000** ifikapo Juni 2022; na
  - c) Kutanua wigo wa uwakala wa kuuza muda wa maongezi, matumizi ya N-CARD na huduma za tiketi mtandao kwa kushirikiana na wadau.

#### **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

112. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 33,435,331,960** kutoka katika vyanzo vyake vinne vya mapato, ambavyo ni Ruzuku toka Serikali Kuu, tozo ya huduma, mchango toka TCRA na wadau wa maendeleo.

113. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umepanga kutekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara nchini kwa lengo la kuyajumuisha katika miradi ya Mfuko;
- ii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kufikisha mawasiliano ya simu katika kata 1,057 ili kuona huduma iliyokusudiwa inawafikia wananchi katika viwango vinavyokubalika;

- iii) Kuunganisha shule 150 za Serikali kwenye mtandao wa intaneti na kuzipatia vifaa vya TEHAMA;
- iv) Kuzipatia Shule 10 za wanafunzi wenye mahitaji maalum vifaa maalum vya TEHAMA vya kujifunzia;
- v) Kuboresha usikivu wa matangazo ya redio katika maeneo ya mipakani;
- vi) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 650 kutoka katika shule zilionufaika na vifaa vya TEHAMA kutoka katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote;
- vii) Kutathmini na kutoa ruzuku ya kuboresha miundombinu ya umeme mkubwa (phase three) katika vilima kwa ajili ya kuwawezesha watoa huduma wa ving'amuzi vya matangazo ya kidigitali ya runinga (MUX Operator) katika mikoa ya Babati (Gitsmi), Shinyanga (Kilulu) na Mbeya (Kyela);
- viii) Kutekeleza mradi wa kuanzisha kituo kimoja cha TEHAMA katika wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar;

### **Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

114. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 40,761,234,400** kutokana na biashara za usafirishaji wa barua, usafirishaji wa nyaraka kwa njia ya haraka (EMS), fedha na uwakala, biashara mtandao pamoja na miliki.

115. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

- i) Ununuzi wa vyombo vya usafirishaji (*delivery van 13, pickups 7 na pikipiki 80*) kwa ajili ya shughuli za usafirishaji na usambazaji wa barua, vifurushi na vipeto pamoja na usafirishaji wa sampuli za maabara nchi nzima;
- ii) Kuboresha utoaji huduma na muonekano wa Ofisi kwa kukarabati na kuweka samani katika Ofisi Kuu za Mikoa tisa (9) ya Mwanza, Tanga, Mbeya, Singida, Lindi, Katavi, Kigoma,



Geita na Mjini Magharibi pamoja na Ofisi za Wilaya tano (5) za Chato, Ifakara, Mbozi, Temeke na Kinondoni;

iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya Shirika la Posta kwa kuhakikisha mfumo wa utoaji huduma za Posta yaani *Posta Management Information System (PMIS)* unatoa huduma zote zilizokusudiwa pamoja na kusomana na mifumo mingine ya malipo na utoaji wa taarifa mbalimbali za ufanisi. PMIS ni mfumo wenye huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji huduma za kaunta kwa wateja, huduma za utumaji barua na pia ina mfumo wa ufuatiliaji barua;

iv) Kukamilisha utengenezaji wa programu tumizi (*application*) ya Posta Kiganjani na kuhakikisha huduma zote za Posta zinapatikana katika mfumo kwa njia ya kielektroniki. Posta kiganjani ni mfumo unaowezesha wateja wa Posta kupata huduma kupitia simu ya mkononi. Huduma hizi ziko katika mfumo wa PMIS na Programu ya Smartposta ambazo zimeunganishwa ili kuweza kutoa huduma mbalimbali za kiposta;

v) Kuanzisha kituo cha kutolea huduma za Posta katika Mji wa Serikali Mtumba-Dodoma; vi) Kuanzisha maduka sita (6) ya kununua na kuuza fedha za kigeni (*Bureau De Change*) katika ofisi za posta za Ilala, Muhimbili, Mutukula, Sirari, Kahama na Geita, sambamba na hilo Shirika limeendelea kuimarisha maduka 26 yaliyopo kwa kuboresha mfumo wa utoaji huduma;

vii) Kupanua wigo wa huduma za usafirishaji wa sampuli za maabara kutoka Mikoa 18 ya sasa na kutoa huduma katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

viii) Kuimarisha huduma za masoko na utafiti (*marketing and research*) kwa ajili ya kupata fursa za biashara kitaifa na kimataifa na kuzitumia fursa hizo katika kukuza biashara za Posta; na

ix) Kuendelea kusimamia na kuendesha vituo vya Huduma Pamoja kupitia mradi wa Tanzania ya kidijitali katika majiji ya Mwanza, Arusha, Tanga na Mbeya.

## Tume ya TEHAMA (ICTC)

116. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume ya TEHAMA inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 2,107,622,000** kutoka vyanzo vya ndani, mgao wa Matumizi Mengineyo (OC) na wadau wa maendeleo.

117. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume ya TEHAMA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kuendelea kusajili wataalam wapya 900 wa TEHAMA na kutambua mafunzo ya TEHAMA kwa ajili ya kuendeleza ujuzi na utaalam wa TEHAMA nchini;

ii) Kuandaa na kutekeleza Agenda ya Tafiti za TEHAMA;

iii) Kutengeneza Mfumo wa Kuratibu na Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (*ICT Innovation Development Framework*) na kuendelea kanzidata ya wabunifu na watafiti wa TEHAMA nchini;

iv) Kuendelea kuratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA katika maeneo ya kitaalam ya TEHAMA;

v) Kuendelea kufanya utafiti wa kupima viashiria vya Jamii Habari; na

vi) Kutekeleza Mradi wa ujenzi wa kituo cha kuendeleza ujuzi, ubunifu na bidhaa za TEHAMA nchini.

## Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA – CCC)

118. *Mheshimiwa Spika*, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA - CCC) kwa mwaka 2021/22 ni kama zifuatazo:

i) Kuendelea kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kushirikiana na Taasisi za umma na binafsi;

ii) Kupokea maoni kutoka kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano pamoja na Kamati za Watumiaji Mikoani na kuziwasilisha kwa taasisi husika ili kuboresha ufanisi na kupunguza changamoto zinazowakabili watumiaji;

iii) Kuandaa na kuendesha vipindi na programu za elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, machapisho, mitandao ya kijamii, tovuti na makala za video (*documentaries*) kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu masuala muhimu ya mtumiaji pamoja na fursa mbalimbali katika sekta ya mawasiliano;

iv) Kukamilisha uandaaji wa programu tumizi (*mobile app*) itakayoongeza fursa za kuwafikia watumiaji wengi zaidi kwa ajili ya kutoa elimu na kupokea maoni; na

v) Kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Watumiaji katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

#### D. SHUKRANI

119. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kwa upekee niweze kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Mawasiliano. Washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Afd).

120. **Mheshimiwa Spika**, ningependa kuchukua fursa hii kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Mawasiliano

inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati wa juu ifikapo mwaka 2025.

**E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

121. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 216,384,551,000.00** kwa mchangano ufuatao:-

i) Kiasi cha **Shilingi 4,984,770,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 2,023,935,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 2,960,835,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

ii) Kiasi cha **Shilingi 211,399,781,000.00** kinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 185,000,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 26,399,781,000.00** ni Fedha za Nje.

122. *Mheshimiwa Spika*, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni <http://www.mawasiliano.go.tz>.

123. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja lilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante na hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba yake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, mama yetu Mama Malecela. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa

kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kwa mujibu wa kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wafedha wa 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri utakaotolewa katika Taarifa hii ni kutokana na majukumu ya Kamati kama yalivyoainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, kifungu cha 6(8) cha Nyongeza ya Nane ambayo imeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2021/2022; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi 11,000,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya Miradi miwili ambayo ni Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano shilingi 8,000,000,000.00 na Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi shilingi 3,000,000,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti: Kamati ilifanya ziara kuanzia tarehe 12 hadi 16 Machi, 2021 katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Hata hivyo, miradi iliyotembelewa yote ipo katika Mkoa wa Dar es Salaam ambayo ni Ujenzi wa Mkongo wa Taifa ambao unasimamiwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) kwa ajili ya kupatikana taarifa ya mfumo wa kusimamia na kuratibu mawasiliano ya simu, ambao kwa kiasi kikubwa umefanikisha kukusanya fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyobainika katika ziara; katika usimamizi wa mkongo ambao umekasimiwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TTCL), Kamati imebaini changamoto ambayo ni ya muda sasa ya kutokuwepo kwa fungu la fedha ya uendeshaji na usimamizi wa mkongo na hivyo kusababisha TTCL kutumia fedha zake za mapato ya ndani kwa ajili ya mkongo pasipo kurejeshewa, jambo linaloathiri utendaji wa TTCL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hiyo hadi kufikia mwezi Disemba, 2020, Shirika la Mawasiliano Tanzania linaidai Wizara jumla ya Dola za Kimarekani 68,309,414.30 ambazo ni: Madai ya ada ya usimamizi wa uendeshaji; Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) iliyolipwa na Shirika kwa ajili ya Mkongo; Gharama za upangishaji wa vifaa; Malipo ya gharama za matengenezo; Bima ya vifaa vya Mkongo; na Pango la ofisi ya Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kutokuwepo mwongozo au makubaliano ya mikataba kati ya Shirika na Wizara kuhusu majukumu na maeneo ya uwajibikaji kwa pande zote mbili na uharibifu wa miundombinu unaotokana na mmonyoko wa udongo pamoja na miundombinu ya Mkongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu mfumo wa kusimamia na kuratibu mawasiliano ya simu; Kamati imebaini fadia ya mfumo huu ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kupata takwimu za mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani na nje ya nchi;

(ii) Kuhakiki mapato yote ya watoa huduma ya Mawasiliano nchini;

(iii) Kupata takwimu zinazohusiana na matumizi ya huduma za mawasiliano (simu za sauti, matumizi ya *data* na jumbe fupi);

(iv) Kugundua mawasiliano ya simu za ulaghai;

(v) Kutambua takwimu za ada za miamala ya fedha mtandaoni;

(vi) Kusimamia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano na hivyo kuboresha viwango vya huduma hizo;

(vii) Kutambua taarifa za laini za simu na namba tambulishi za kifaa cha mawasiliano;

(viii) Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizopakiliwa;

(ix) Kuwasilisha kwa Serikali mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazolingia na kuishia hapa nchini; na

(x) Kusimamia kanzidata ya taarifa za usajili wa simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tangu Mfumo huu ulipoanza kufanya kazi 2013, hadi Novemba, 2020, jumla ya Sh.403,774,208,412.24 zimekusanywa na watoa huduma kama mapato kupitia simu za kimataifa zinazolingia hapa nchini.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021, hadi kufika mwezi Februari, 2021, mapato kutokana na mtambo wa *TTMS* ni Sh.7,472,659,089.76. Kamati imebaini ongezeko la Sh.197,318,511.32 sawa na ongezeko la asilimia tatu la makusanyo ya mapato ukilinganisha na makusanyo yaliyopita kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa ujumla mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa sheria ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasiliano duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2020/2021; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara

ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Sh.30,000,000,000.00 ambapo hadi mwezi Februari, 2021 zimekusanywa bilioni 68.22 ya makadirio ya makusanyo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika/Taasisi zilizo chini ya Wizara hii zilipanga kukusanya jumla ya Sh.425,890,138,007.00 kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyvo katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya Mashirika yameendelea kuwa na makusanyo madogo ikilinganishwa na Taasisi zingine. Mashirika yenye makusanyo madogo ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) ambalo lilikusanya kiasi cha shilingi 68,043,738,328.91 sawa na asilimia 34.1 na Shirika la Posta Tanzania ambalo lilikusanya kiasi cha shilingi 18,667,096,428.00 sawa na asilimia 41 ya makadirio ya makusanyo yaliyopaswa kukusanywa kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yaliyofanya vizuri katika makusanyo kwa mwaka 2020/2021 ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) ambayo imekusanya kiasi cha shilingi 117,520,800,598.56 sawa na asilimia 81.5 na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambao ulikusanya kiasi cha shilingi 24,469,097,483.00 sawa na asilimia 78.6 hadi tarehe 28, Februari 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya *TEHAMA* ilikadiriwa kutumia Sh.1,232,897,000, lakini hadi kufikia 28 Februari, 2021, matumizi yalikuwa ni shilingi 186,448,499.96 ya makadirio sawa na asilimia 15.1. Fedha iliyopokelewa kutoka Serikalini kwa kipindi hicho ni kiasi cha shilingi milioni 226,448,499.96. Kwa ujumla ni muhimu kwa Serikali kuchukuwa hatua za kuimarisha mashirika yake ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za mandeleo; kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi 11,000,000,000.00 kama mchanganuo wa jedwali unavyoonesha.



Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hali ya utolewaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Mawasiliano si ya kuridhisha kwani hadi Kamati inakutana na Wizara mwezi Machi ya kila mwaka fedha hutolewa kwa kiasi kidogo kisichovuka asilimia 50. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha unaoisha 2020/2021 fedha zilizotolewa ni asilimia 19 tu ya fedha zote za miradi ya maendeleo zilizoidhinisha. Hali hii ya fedha kutolewa kwa kiasi kidogo imeathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 50,000,000,000.00. Fedha hizi zinatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi 20,000,000,000.00 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Mashirika yalio chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yanakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 787,229,091,796.39. Kamati imebaini ongezeko la Sh.361,338,953,789.39 ambalo ni sawa na asilimia 85 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo linatokana na ongezeko la Makadirio ya mwaka 2021/2022 kwa Mashirika ambayo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Posta, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Tume ya TEHAMA kama inavyoonyeshwa katika jedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imetenga shilingi 4,984,770,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 2.3 ya fedha zote zilizotengwa kwa Wizara ya Mawasiliano kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka shilingi 4,654,466,000.00 za mwaka 2020/2021 hadi shilingi 4,984,770,000.00 ambalo ni ongezeko la shilingi 330,304,000.00 sawa na asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Fedha za Miradi ya Maendeleo; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa shilingi 211,399,781,000. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jedwali Na.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2021/2022 zimepanda kutoka shilingi 11,000,000,000.00 hadi kufikia shilingi 211,399,781,000.00 ambapo zimeongezeka shilingi 200,399,781,000.00 sawa na ongezeko la asilimia 1922.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini, ongezeko hili limetokana na Serikali kuongeza fedha za maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu iliyotekelezwa na Wizara na mabadiliko yaliyofanywa na Serikali kwa Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 68; Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuongeza bajeti wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwani Wizara hii ni nyeti sana na ina mchango mkubwa katika pato la Taifa. Aidha, ongezeko hili linaonyesha Serikali imetambua na kuthamini umuhimu wa Wizara hii ambayo ina jukumu kubwa la kusimamia mambo ya mawasiliano ya Teknolojia ya Habari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); soko la mawasiliano ya simu na intaneti limekuwa kwa kasi kati ya mwaka 2015 hadi 2021. Ukuaji huu unatokana na uwekezaji unaofanywa katika miundombinu ya mawasiliano, sera,

sheria na mazingira mazuri na mfumo unaohusisha wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya laini za simu inakuwa kwa asilimia saba, simu za sauti zinaongezeka kwa asilimia nane na matumizi ya data yanaongezeka kwa kwa asilimia 25 na mapato yanaongezeka kwa asilimia tatu kwa mwaka. Hii ni tofauti na hali ya uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano ambao umeshuka kutoka shilingi bilioni 1,123 kwa mwaka 2015 hadi Shilingi bilioni 491 kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya nne yenye bei ndogo ya *data* kwa Afrika ikiongozwa na Sudan, Somalia na Ghana, pia ni nchi yenye bei ndogo za *data* ikilinganishwa na nchi zote za *EAC* na *SADC*. Pamoja na kuwa na bei ndogo ya *data*, bado ina asilimia kubwa ya kodi zinazotowwa kwenye huduma za mawasiliano ikilinganishwa na Nchi za Afrika Mashariki na *SADC*. Imebainika kuwa ukubwa wa asilimia ya kodi zinazotowwa kwenye huduma za mawasiliano unasababishwa na malipo ya *excise duty* ambapo ni asilimia 17 tofauti na Nchi zingine za Afrika Mashariki na *SADC* (Mfano, kodi ya *excise duty* kwa Kenya ni asilimia 15, Uganda asilimia 12, Burundi asilimia 12 na Rwanda asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Serikali ikaangalia kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano kwani mawasiliano ni huduma muhimu na wezeshi kwa sekta nyingine. Kuwepo kwa kodi kubwa kunaweza kusababisha kupunguza matumizi ya huduma na kupunguza uwezo wa wawekezaji kupanua huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Anuani ya Makazi; utekelezaji wa mradi huu unahusisha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – *TCRA*) ikishirikiana na Wizara nyingine zinazohusika na Mradi huu wa Anuani ya Makazi na Misimbo ya Posta ambazo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka kuanzishwa kwa mradi huu Kamati imekuwa hairidhishwi na utekelezaji wake kutokana na changamoto ya mradi kutengewa kiasi kidogo cha fedha na zimekuwa hazitolewi kwa wakati, jambo ambalo limekuwa likiathiri utekelezaji wa mradi huu. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi 3,000,000,000 fedha za ndani ambapo hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2021 jumla ya shilingi 1,212,827,106.65 zilipokelewa, sawa na asilimia 40 ya fedha zote zilizotengwa kwa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu umetengewa shilingi 45,000,000,000.00. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuongeza bajeti ya mradi huu kwa ongezeko la shilingi 42,000,000,000.00 sawa na ongezeko la asilimia 1,400. Ongezeko hili ni kubwa na linatoa taswira halisi ya dhamira ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*); lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ni kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara ambapo usambazaji wa mawasiliano unafanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya Simu kama vile Tigo, Vodacom na Halotel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kusambaza mawasiliano nchini, mfuko umekamilisha kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 55 zenye vijiji 169 na wakazi 679,000 kati ya kata 252 za mradi awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya mawasiliano kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya mipakani mwa nchi ambapo maeneo mengi yamekuwa yakiingiliana mawasiliano ya simu kwa kiasi kikubwa na nchi Jirani, jambo linaloongeza gharama ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, changamoto nyingine zinazoukabili Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ni

uhaba wa fedha, watoa huduma kutokamilisha kwa wakati miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano kwa mujibu wa mikataba na mapungufu ya kisheria yanayotoa mwanya kwa watoa huduma na wadau mbalimbali kutowajibika kwa mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Simu Tanzania (TTCL); licha ya kuwepo na juhudi mbalimbali zinazofanywa kuhakikisha TTCL inamudu ushindani wa kibiashara na kuzidi kuimarika, hali ya utendaji wa shirika hili bado si ya kuridhisha kwani bado shirika linakabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo wa uwekezaji usiyoendana na mabadiliko ya teknolojia na kushindwa kukabiliana na ushindani wa soko la mawasiliano. Changamoto zingine zinazolikabili Shirika la Mawasiliano Tanzania ni pamoja na: - (Makofi)

(a) Mtaji mdogo kwa ajili ya uwekezaji na kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayokwenda sanjari na kasi ya uwekezaji;

(b) Madeni ya zamani ambayo yanatokana na kutumia huduma mbalimbali ambayo mengi yao shirika linaidai Serikali na taasisi zake ambapo hadi Januari, 2021 kiasi cha shilingi bilioni 20.1 zinadaiwa; (Makofi)

(c) Sheria ya Manunuzi kdwa mashirika ya Umma ambayo inaleta urasimu unaokinzana na ushindani wa kibiashara; (Makofi)

(d) Kutokuwepo kwa fungu la fedha za uendeshaji na usimamizi wa Mkongo na kusababisha TTCL kutumia fedha zake za mapato ya ndani kwa ajili ya Mkongo pasipo kurejeshewa, jambo linaloathiri utendaji wa TTCL kwani hadi Desemba 2020, shirika linaidai Wizara jumla ya Dola za Kimarekani 68,309,414.30; (Makofi)

(e) Uharibifu na ukataji wa miundombinu ya Mkongo unaotokana na shughuli za binadamu, hujuma, na shughuli za maendeleo kama ujenzi na upanuzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Serikali ina nia ya kufanya shirika hili liweze kujiendesha kwa tija na kumudu ushindani, ni vema changamoto hizi zikatatuliwa kwa haraka ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia pamoja na ukuaji wa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa Kamati na kuliondoa Shirika la Posta Tanzania katika orodha ya mashirika yaliyokuwa yanasubiri kurekebisha. Hii ni hatua nzuri ambayo itasaidia shirika hili kutumia rasilimali zilizo kufanya uwekezaji kwa lengo la kijiendesha kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hiyo nzuri, shirika hili limeendelea kukabiliwa na changamoto ya kuwa na mtaji hasi. Shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani uliopo na changamoto ya soko katika Sekta ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shirika limeelemewa na mzigu wa deni la kodi la muda mrefu la jumla ya shilingi 26,879,572,393.00 kutokana na kushindwa kuwasilisha kodi na riba mbalimbali kwa wakati kati ya mwaka 2007 na mwaka 2016. Deni hili linajumuisha shilingi 14,840,500,956.00 deni la msingi na shilingi 12,039,071,437.00 tozo ya adhabu na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni deni la wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki ambapo hadi mwezi Februari, 2021 shirika limelipa kiasi cha shilingi bilioni 7.9. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwani imechukua jukumu la kulipa deni hilo ambapo hadi mwezi Machi, 2020, imelipa jumla ya shilingi bilioni 11.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwani sekta hii ni ya muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi na hata kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika na fedha za bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka 2021/2022 kwani bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 1,282 ukilinganisha na Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kuacha fedha angalau asilimia 40 ya makausanyo ya mashirika yake ili yaweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) Kamati ina shauri ufuatao: -

(i) Serikali iendelee kudhibiti gharama za mitandao ya simu kwani gharama za baadhi ya mitandao na vifurushi zipo juu ukilinganisha na uwezo wa wananchi wengi katika kumudu gharama hizo;

(ii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iendelee kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo *NIDA*, Idara ya Uhamiaji, Watoa Huduma, Jeshi la Polisi pamoja na Baraza la Walaji la *TCRA* ili kuhakikisha kuwa watumiaji wa simu za mkononi ambao bado hawajasajiliwa wanasajiliwa kwa mujibu wa sheria;

(iii) Serikali kupitia *TCRA* iendelee kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na mitandao ya uhalifu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani (Jeshi la polisi); na

(iv) Serikali ihakikishe ving'amuzi vyote nchini vinaonesha angalau *channels* nne za ndani ambazo ni za

bure ili kupunguza gharama kwa wananchi kununua ving'amuzi zaidi ya kimoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Kamati inashauri; -

(i) Serikali ipitie upya taratibu za uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufanya maboresho yatakayoondoa changamoto ya Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL kusimamia na kuendesha Mkongo wakati mapato yatokanayo na Mkongo huelekezwa Wizarani, jambo linaloathiri mizania ya hesabu ya TTCL.

Vilevile, Serikali kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(ii) Kwa kuwa moja ya changamoto zinazoikabili TTCL ni ukosefu wa fedha za kutosha kufanya uwekezaji unaotakiwa, Serikali iendeele kusaidia Shirika la TTCL mpaka litakapoweza kujiendesha kibiashara na hatimae kumudu ushindani katika soko, hii ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa TTCL kuweza kupata mkopo wa gharama nafuu;

(iii) Serikali iweke mkazo kwa vyombo vyake vyote kulipa madeni yanayodaiwa na TTCL ambayo hadi mwezi Machi, 2021 yameripotwa kufika shilingi bilioni 14.8;

(iv) Serikali iangalie namna itakavyoweza kusaidia TTCL kwenye Sheria za Manunuzi ili ziweze kubadilika ili TTCL iweze kwenda kasi na kushindana na makampuni mingine ya mawasiliano; na

(v) Serikali isimamie maboresho katika Kitengo cha Huduma kwa Wateja kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania ili kuendana na mahitaji ya soko la ushindani na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Anuani za Makazi na Postikodi: -



(i) Kwa kuzingatia kuwa Mwaka huu wa Fedha 2021/2022, Serikali imeongeza fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu kutoka shilingi bilioni 3 hadi bilioni 45, sawa na ongezeko la silimia 1500, Serikali sasa ihakikishe fedha hizi zinatolewa zote na kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu katika maeneo yaliyokusudiwa kwani mradi huu utarahisisha upatikanaji, utoaji na ufikishaji wa huduma mbalimbali;

(ii) Ili Mradi wa Anuani za Makazi uweze kutekelezeka kwa haraka na ufanisi, Wizara zinazohusika na mradi huu ikiwemo Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, TAMISEMI, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zikae pamoja na kuona namna nzuri ya kuharakisha utekelezaji wa mradi huu kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

(iii) Ili mradi huu uwe wa kisasa na kuenda na wakati, ni vema wataalam wa mradi huu wakajifunze katika nchi zingine na kuona namna nchi hizo zilivyofanikisha na kuweka mfumo huu; na

(iv) Serikali za mitaa kuhakikisha zinatoa elimu ya kutosha na zinalinda miundombinu ya mradi huu dhidi ya wahalifu wanaochukuwa chuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Pamoja na Serikali kurejesha kiasi cha shilingi bilioni 11.1 kwa Shirika la Posta ambazo zililipwa kwa ajili ya madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inasisitiza Serikali iendelee kulipa fedha zilizobaki ambazo ni jumla ya shilingi bilioni 7.9;

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kulisaidia Shirika la Posta kwa kufuta deni la kodi la muda mrefu la jumla ya shilingi bilioni 27 ambalo shirika linadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na kushindwa kuwasilisha kodi na riba mbalimbali kwa wakati;

(iii) Kwa kuwa moja ya changamoto zinazolikabili Shirika la Posta ni kutokuwa na mtaji wa kutosha, ni muhimu sasa Serikali kulisaidia shirika hili mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na hatimae kumudu ushindani katika soko;

(iv) Shirika la Posta lipewe jukumu la kusimamia usafirishaji wa vifurushi vyote ikiwa ni pamoja na kutoa vibali kwa wasafirishaji wengine; na

(v) Shirika la Posta lipewe kusimamia na kujenga miundombinu ya Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta kwa kuwa kihalisia Posta ndiye atakaekuwa mtumiaji mkubwa wa miundombinu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kamati inaendelea kutoa maoni na ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iweke mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya milimani ambapo upatikanaji wa mawasiliano umekuwa ni changamoto. Vilevile maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kupata taarifa za nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Sekta ya Mawasiliano ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani sekta hii huwezesha sekta nyingine zote kuweza kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Spika, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini na kuwezesha Bunge kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ANNE K. MALECELA – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza michango; tunaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi, ajiandae Mheshimiwa Antipas Mgungusi, ajiandae Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mzungumzaji wa kwanza katika Wizara hii ya Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa imani ambayo Wabunge wamekuwa nayo juu yako na kukurudisha katika kiti cha enzi, na ninaamini kwamba utatuombea dua na siku ya Jumamosi mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, lakini pia nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Andrea Mathew Kundo pamoja na Katibu Mkuu, Dkt. Chaula, lakini pia na Naibu

Katibu Mkuu Jim Yonazi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii bado ni mpya kwa maana ya kuundwa hivi karibuni lakini mambo ambayo inafanya ni mambo ya siku nyingi. Na Wizara hii imeundwa mahususi kabisa kuja kuwasaidia Watanzania na hususan vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi katika ukurasa wa 96, imezungumzia suala la uwekezaji na kuwezesha mashirika kimitaji na kimenejimenti. Kwa bahati nzuri sana menejimenti iliyopo sasa chini ya Mtendaji Mkuu wa *TTCL* Waziri Kindamba, anafanya kazi nzuri sana, na kama Serikali ikimpa ushirikiano tunaotaraji ambao umeelekezwa katika ilani wa uwezesaji wa kiuchumi na kimenejimenti, maana yake shirika hili litakwenda mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa kama ambavyo mmesikia ripoti ya Kamati hapa inaonesha kwamba madeni makubwa ambayo *TTCL* anadai yamesababishwa na Serikali. Kwa hiyo, Serikali yenyewe imekuwa sasa ndio muuaji wa mashirika yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo katika eneo hili hatutakubali kwa sababu tumekukabidhi *tools* za kusimamia Wizara hii kupitia ilani ya chama, kwa hiyo chama tutakuuliza; tumekupa ukaue shirika au ufanye shirika lifanye kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG*, takribani bilioni 40 zinadaiwa kupitia Mkongo wa Taifa. Kamati hapa imeeleza kwamba na yenyewe inaona takribani dola milioni 68 za Mkongo wa Taifa ni deni kutoka *TTCL*. Kwa hiyo, tunaomba sana kwamba eneo hili tulisimamie vizuri ili shirika hili liweze kushindana na mashirika binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe hatujaweka mtaji wowote mkubwa kwa kipindi cha takribani miaka kumi

mpaka kumi na mbili wakati kampuni hizi binafsi karibia kila mwaka zinaweka mtaji wa dola 100,000 mpaka 150,000. Katika hali ya kawaida hatuwezi kufanya Shirika hili lishindane. Kwa kweli tunaomba sana Shirika hili lijengewe uwezo, uwezo wa *management* upo na tunaridhika nao lakini uwezo wa mtaji ndiyo jukumu la Serikali hasa kupitia madeni ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi makampuni binafsi hayaweki dola laki moja wanaweka dola milioni mia moja kila mwaka. (*Makofi*)

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa sahihisho hilo, sasa nadhani Mheshimiwa Ndugulile amekaa kwa kutulia pale unaweza ukaona kwamba makampuni binafsi wanaweka dola milioni mia moja sisi miaka 12 mpaka 15 hatujaweka chochote. Hata hicho wanachozalisha tunaendelea kukivuna, madeni yale ambayo Serikali inazalisha hatuyalipi. Kwa hiyo, tunaomba suala hili lishughulikiwe na jioni hapa kwenye shilingi tunakuandaa kabisa uwe tayari vinginevyo leo utaondoka bila mshahara hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni kwamba Shirika hili tunataka liwezeshe kimenejimenti kwa maana kwamba liwe huru kibiashara. Yapo mashirika kama haya kwenye nchi za wenzetu, kwa mfano, kuna *Deutsche Telecom* Ujerumani, *China Telecom*, *Telecom Egypt*, *Telecom Namibia*, ni Mashirika ya Umma lakini yanajiendesha kibiashara moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huku tunakoendesha sana kwa kisiasa hivi ndiyo maana wakati mwingine sasa tunayanyang'anya hata mitaji ya kujiendesha na kuyafafanisha na makampuni binafsi, hii siyo sawa. Kwa kuwa vijana tuliowakabidhi wana uwezo wa kuliendesha kimenejimenti ni lazima tulipe sasa kazi ya ziada na tupate shirika ambalo linakuwa la matokeo, *result oriented*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni *TCRA*. Hapa napo kuna shida, sisi

kama Taifa ni lazima tutangaze utamaduni wetu kimataifa na hili eneo zile *TV* za kulipia (*Pay TV*) zinafanya kazi nzuri sana, lakini zinazuliwa kuweka matangazo katika zile *channel* zao ambazo zipo katika *Pay TV*. Kwa mfano, *Azam Media* kupitia *Cinema Zetu* ambapo wote tunafahamu kwamba tasnia ya *Bongo Movie* na *Bongo Flewa* wanaitumia sana ku-*promote* muziki wao, hawaruhusiwi kuweka matangazo wala kuwa na wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pay TV* ndiyo *TV* pekee ambazo zinaonekana ndani na nje ya nchi kwa maana kwamba zinakuwa katika ving'amuzi vya ndani na vya nje, kule ndiyo utamaduni wetu unaweza ukaonekana. Utamaduni huu ukionekana kupitia wadhamini na matangazo maana yake uzalishaji wa hizi sinema utakuwa bora zaidi na vijana wengi watapata ajira ya kutosha hapa na matokeo yake na Serikali nayo itapata kodi kupitia matangazo na udhamini. Sasa Serikali inakwama wapi kuziruhusu hizi *Pay TV* kuweka matangazo na wadhamini? Hii siyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TV* kama ya Wasafi, kijana mdogo yule anajaribu kukua, lakini tunamuwekea vizingiti vya namna hii, tunatarajia tuwe na Wasafi nyingi, ni watu wangapi wameajiriwa ndani ya Wasafi *Media*. Unapowanyima fursa ya kuweka matangazo na kuwa na wadhamini atatokaje huyu kwenda kuzalisha vijana wengine watengeneze maudhui mazuri ili yauzike kimataifa na sisi utamaduni wetu uzidi kukua huko lakini mwisho wa siku Serikali mtapata kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *Azam Media* ndiyo inaonyesha mpira katika Ukanda huu wa Kusini mwa Afrika inashindana na *TV* nyingi za Kimataifa *DSTV*, *GTV* na nyinginezo, lakini ile ni sifa ya Watanzania. Mwaka huu wameweka uwekezaji mkubwa, nadhani tutatangaziwa hivi karibuni kupitia ligi ya *VODACOM* mkataba wa miaka kumi shilingi bilioni 190, haijawaji kutokea. Hiki ni chombo cha Watanzania, hizi ni bidhaa za Watanzania lazima tufaharike nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapowawezesha hawa ndiyo wanaongezeka akina Baraka Mpenja kule ambapo wanapata ajira, akina Ally Kamula watapata ajira tutakuwa nao, lakini wakina Gift Macha watapa ajira tutakuwa nao. Sasa *TCRA* hili eneo la kwenye *Pay TV* matangazo na udhamini tatizo lenu ni nini? Mbona Serikali wakati mwingine mnakuwa na wivu ambao hauna sababu? Kwa sababu kwa kupitia matangazo na huo udhamini tutapata kodi na tukipata kodi ndiyo tutazidi kutanua hii tasnia na itakuwa kubwa zaidi, itaajiri vijana wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba katika ukuaji wa pato la Taifa ina sehemu kubwa sana ya mchango wa sanaa, sasa sanaa yetu itakuwa tu endapo itakuwa inaonekana katika ving' amuzi vya kimataifa na vya ndani kwa sababu sasa ndani tumejitosheleza twende nje, tuwaruhusu hawa waweke matangazo. Utalii wetu pia tutautangaza kupitia hizo *Pay TV* tukiweka matangazo pale Nigeria, Ivory Coast na kila mahali wataona. Tunalalamika hapa kwamba hatutangazi utalii wetu tunaweza tukautangaza kupitia *Pay TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu kwa siku ya leo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shangazi, umezungumza mambo muhimu sana hasa haya masuala ya matangazo. Ni kweli kwenye kipindi hiki sasa cha *digital externalization*, ni lazima Serikali muachane na vitu vingine. Mwendokasi mabasi nyie, michezo nyie, kila kitu nyie, acheni hivi vitu, acheni watu wajimwage sasa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Antipas na Mheshimiwa Jerry Silaa ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote, naomba uniruhusu niweze kutoa shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya TAMISEMI ingawa siyo Wizara hii, lakini waliweza ku-*attend* dharura ya Malinyi

ya mafuriko ya maji yaliyoathiri barabara zetu. Fedha zimetolewa, sasa wakandarasi wapo *site* wanatatua tatizo Wanamalinyi watakuwa na amani hawataathirika tena na masuala ya mvua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii nina mambo mawili au matat. La kwanza, Jimbo langu la Malinyi lina changamoto ya mawasiliano, sehemu kubwa ya jimbo huwezi kupatikana, karibia asilimia thelathini au arobaini ya Jimbo ndiyo wanapatikana hewani, lakini zaidi ya asilimia sitini, sabini hakuna mtandao *voice* na *data* ndiyo kabisa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi ninavyozungumza Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkurugenzi hazipatikani kwa maana huwezi kumpata mtu hewani akiwa kwenye Ofisi hizo mpaka jioni wakirudi mtaani ndiyo unaweza wakapatikana. Kwa hiyo, naona Wizara inanisikiliza naomba walichukulie hili jambo kwa udharura watu Malinyi waweze kusaidika tuweze kupata mawasiliano kama maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia changamoto ya *cyber-crimes* kwa maana ya wizi wa mtandao umeendelea kuwepo. Mnakumbuka tulifanya usajili wa *line* kwa njia ya vidole ili kuweza kudhibiti changamoto hii, lakini mpaka leo hii bado watu wanafanya utapeli na namba ambazo zinatumika kufanya utapeli bado zinapatikana hewani mpaka hivi ambavyo ninazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi ni muhanga wa jambo hili, watu wame-*forge* akaunti kwenye mitandao ya *facebook* wanawatapeli watu kuna masuala ya ajira mtume nauli na kadhalika ili ufanyiwe mipango, namba ambazo zinatolewa watu wanapiga bado zipo hewani na watu wanaendelea kutapeliwa fedha. Nimefanya majaribio kadhaa rasmi kwa maana ya kuripoti Polisi miaka miwili iliyopita, tumeandika barua, nimepewa *RB* naambiwa watu wa *cyber* wanafuatilia lakini mpaka leo wanaendelea kutapeliwa na tunachafuliwa heshima zetu. Sasa mimi ni



kiongozi nina *access* ya kusema, sijui watu wangapi kwenye nchi hii wanakumbana na adha ya namna hii na hawezi kusema. Kwa hiyo, naomba Wizara ilichukulie jambo hili *serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni suala la mawasiliano ya simu katika vivutio vya utalii kwenye *National Parks, Game Reserve* na maeneo mengine. Kwa mfano, Hifadhi kama ya Mlima Kilimanjaro tuna watalii wengi wanapanda lakini asilimia 90 ya mlima ule mawasiliano hakuna. Watangazaji wazuri wa utalii ni watalii wenyewe, watalii wa ndani na watalii wa nje, watu wanapanda milima wanapenda ku-*share experience* yao moja kwa moja, watume picha kwenye mitandao, wafanye *live video calls* kuwahamasisha wengine lakini jambo hili haliwezekani kwa maana ya kwamba *network* hakuna kabisa mlimani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu Mheshimiwa Waziri alichukue hili washirikiane na Wizara ambayo ni mlaji ya Maliasili wahakikishe Mlima Kilimanjaro ambacho ni kivutio chetu kikubwa mawasiliano yawepo muda wote hasa ya *data*. Jambo hili linaendelea hata kwenye hifadhi zingine Ruaha, Ngorongoro maeneo mengine ya misitu yote yana changamoto kubwa za *network*. Kwa hiyo, naomba suala hili lichukuliwe kwa uzito kusaidia watalii kui-*enjoy* na kuwashawishi wenzao kwa kuona kwenye mitandao uzuri wa vivutio vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo changamoto pia ya doria, askari wetu ambao wapo porini wanafanya doria kulinda maliasili za nchi yetu, wanakutana na changamoto kubwa ya mawasiliano. Siyo mara zote *radio call* zinafanya kazi vizuri lakini mawasiliano ya simu yanaweza kuwa rahisi kuhakikisha watu waliopo kule porini wanafanya kazi vizuri, wanatoa taarifa kwa wakati, muda mwingine ni rahisi hata ku-*track* majangili, mambo ya kuviziana ni ya kizamani sana lakini *technology* ndiyo inafanya kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wizara inanisikia walichukue jambo hili, hata majangili ambao wapo porini

wanapanga mipango unaweza ukawa-*track* kupitia *technology*. Maeneo makubwa ambayo yanaathari ya ujangili hayapatikani kwa simu tunatumia tu *radio call*. Kwa hiyo, naomba Serikali ilichukue suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo mchango wangu ni huu, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry Silaa ajiandae Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kugundua mchango wa sekta ya TEKNOHAMA katika uchumi wa Taifa letu. Kwa kuunda Wizara hii, ni matumaini yetu sasa kwamba Serikali itatengeneza utaratibu mzuri ili sekta hii iweze kutoa mchango chanya kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri ameanisha takwimu za watumiaji ambao mpaka hivi tunavyozungumza wanatumia *line* za simu. Mpaka kufikia anasoma hotuba hapa leo wapo watumiaji 53,063,000 wanaotumia *line* za simu. Kuna Watanzania 29,071,000 wanaotumia mtandao wa *internet* lakini zaidi ya Watanzania 32,000,000 wanatumia miamala ya fedha kwa maana ya fedha za kwenye simu. Ukiangalia takwimu zote hizi za mamilioni utagundua kwamba tayari Tanzania ipo na wenzetu wa duniani, kwamba sasa tumehama toka kwenye mifumo tuliyoizoea (*traditional systems*) kwenda kwenye mifumo ya kimtandao kwa maana ya *online systems*, tutakutana kwenye bajeti kuu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi tunavyozungumza wenzetu wa Mamlaka ya Mapato wanao Watanzania wenye *Tax Identification Number* kwa maana

ya *TIN Number* milioni mbili na laki tano. Ukiangalia takwimu hizi za *online* na takwimu zetu zile tulizozioea za makaratasi, utakubaliana na mimi kwamba tayari dunia imehama na ni wajibu wetu kama Watanzania kuwekeza nguvu kubwa zaidi ya kutumia *advancement* hii ya teknolojia kuendesha uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza, tumeona kwenye *Finance Act* nyingi kwamba wenzetu wa Serikali wanatumia takwimu hizi za wingi wa watumiaji wa simu, *internet*, mitandao ya fedha kwenye simu kama ndiyo mtaji na kuweka makodi mengi ambayo yanawaumiza watanzania. Wanasahau kwamba takwimu hizi zinapaswa kutumika kama *platform* ya kutengeneza *system* nzuri zaidi ya kuwa kwanza na tija kwenye matumizi yenyewe ya mitandao, lakini pili kama kuna ukusanyaji wa mapato, kukusanya mapato stahiki kwa wale ambao wamebeba ama wale ambao ndiyo *online platform prayers* kwa maana wale ambao ndiyo hasa wamiliki wa mitandao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Ufaransa ndiyo walikuwa wa kwanza (*pioneers*) wa kuanzisha Kodi ya Mitandao, kwa maana ya *Digital Service Tax (DST)*. Waliseti asilimia tatu, kwa mtu yeyote anayefanya biashara ya mtandao lakini biashara hiyo inafanyika na wananchi wa Ufaransa. Tukisema watu hawa ni watu kama *YouTube, Facebook, Instagram, Amazon* na watu wote wale ambao ndiyo wenye biashara zao za mtandao. Wenzetu wakenya kwenye *Finance Act* ya mwaka 2019 wame-introduce *Digital Service Tax*.. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nayasema haya kwa sababu tutakuja kukutana kwenye Bajeti Kuu ya Taifa kuiomba na kuishauri Serikali kuanza kuondoa fikra kwenye kumbana Mtanzania wa kawaida anayetumia mtandao na kupeleka fikra kwenda kuwabana wale wanaopata pesa kupitia mtandao. Tukitumia takwimu hizi vizuri na tukiweza kutengeneza mifumo mizuri ya kuhakikisha biashara zinazofanyika duniani kupitia mitandao ambazo wateja na

watumiaji wake ni wananchi wetu wa Tanzania hawa tunaowataja milioni 53, milioni 29, milioni 32 tuna uwezo kwanza kumsaidia Mtanzania kupata mawasiliano mazuri zaidi lakini kuiongezea Serikali mapato bila kumuumiza Mtanzania wa kawaida anayetumia mtandao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza *content* nyingi za habari zinapita kupitia mitandao. Hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani michango wanayoitoa, kazi wanazozifanya asilimia 90 zinapita kwenye mitandao na siyo kwenye *traditional media systems*. Hapa tunapozungumza TCRA waje watuambie wakati tunahitimisha hotuba hii ya bajeti, hatuna *aggregator* wa YouTube ndani ya nchi yetu, wote hawa unaowasikia wanaotusaidia na sisi, ukisikia Millard Ayo YouTube Channel wanafanya *aggregation* yao ya *content* wanayoi-air kwenye *online platforms* kupitia nchi nyingine. Wapo wanaofanya Kenya, Afrika ya Kusini na wapo wengine vijana wa Kitanzania wanaofanya Marekani na hata kulipwa inabidi walipwe kwa *accounts* za Marekani. Hii si tu inatupunguzia mapato lakini inatengeneza urasimu mkubwa kwa vijana wetu ambao wangeweza kupata tija kubwa zaidi kwenye sekta hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili, nizungumzie maeneo ya *Pay TV*. Zipo leseni TCRA wanazitoa za *Pay TV* ambapo moja kati ya *TV* hizi ni kama Wasafi. Moja kati ya masharti wanayopewa kwanza hawaruhusiwi kutoa *any live coverage including coverage* za matamasha yao ya muziki wanayoifanya. Leo tuna vijana wasanii wanafanya kazi kubwa, wametoa ajira kwa vijana wengi, lakini matamasha hata ya kwao yenyewe wanashindwa kuyaonyesha *live* kwa masharti wanayopewa na TCRA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu pekee kinachoruhusiwa kuonyeshwa *live* ni mpira wa miguu. Sasa wakati tunaendelea kuenzi mpira kama ajira kwa vijana tukumbuke vilevile na tasnia ya sanaa ya muziki na yenyewe ni ajira kwa vijana wetu. Inapoonyeshwa *live Pay TV* zinazoonekana kwenye

mitandao ya *DSTV* zinaonekana Afrika na dunia nzima, wataitangaza nchi yetu na tija tutaiona hata kwenye utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotengeneza masharti haya tuangalie Wizara hii kwa suala mtambuka kwa maana inagusa maeneo yote ya uchumi wa Taifa hili. Tunapokuwa na mifumo ambayo utekelezaji wake unabana fursa badala ya kutanua fursa tunawaumiza wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho niungane na wewe na wachangiaji waliotangulia na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ni shirika letu la *TTCL*, kama kweli Serikali inataka kufanya biashara ifanye biashara. Hatuwezi kuwa na Shirika ambalo fedha haziendi, tumechukua deni la Mkongo tumepelekea Shirika kulipa tabu, sisi wenyewe Serikali ni wateja wa Shirika hatulipi madeni yetu, naomba tuweze kutengeneza *seriousness* katika kusaidia Shirika letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine itafika wakati tatalichukulia hili suala hili kidogo *personal* kwa sababu tushukuru Serikali tunaye Mkurugenzi kijana na masuala ya TEKNOHAMA haya huwezi kuyatofautisha sana na vijana hata mtaalam wangu Mheshimiwa Getere angekuwepo angesema, ni masuala ambayo yanaendana na vijana. Sasa tumuunge mkono, tusiwe sisi wenyewe Serikali tunataka tufanye biashara, lakini sisi wenyewe tukidaiwa madeni hatulipi, sisi wenyewe hatuwekezi na ndiyo wa kwanza kuwasema kwamba hawatekelezi majukumu yao ipasavyo. Kwa hiyo, Waziri utusaidie na useme humu Bungeni maana mengine inawezekana na wewe yapo nje ya uwezo wako kwa maana ya Wizara yako inatakiwa iwezeshe, Wabunge tulisaidie Shirika letu la *TTCL* liweze kupewa uwekezaji wa kutosha liweze kushindana kwenye ushindani wa kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia tena kwamba tunavyotengeneza masharti yanayosimamia tasnia hii ya mitandao, basi tutengeneze masharti ambayo yanaendana na masuala mengine ya kidunia.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Silaa. Nilitegemea vile vile ungesema wateja wa *TTCL* ni milioni 1,100,000 tu, wakati makampuni mengine *private* ni milioni 15.6. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndungulile uko hapa, ili nao wawe na wateja milioni 15, wanahitaji uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza niungane na mzungumzaji aliyepita kuhusiana na mchango wa teknolojia na ukuaji wa teknohama katika ulimwengu. Pia, sisi kama Taifa, kama sehemu katika ulimwengu miongoni mwa washiriki katika maendeleo makubwa sana ya sayansi na teknolojia, hatuwezi kuishi kama kisiwa. Kwa hiyo, ni lazima kama nchi kwa pamoja tukubaliane kwamba tunapozungumza uchumi wa kidijitali, *digital economy* kwanza siyo *terminology* mpya, siyo neno jipya, pia siyo *myth*, yaani ni kitu ambacho kinaishi na kinafanyika kwa sababu nchi za wenzetu duniani sasa hivi wanazungumza kuhusu *digital economy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia *digital economy* au uchumi wa kidijitali, hatuwezi kumaliza bila kuzungumzia miundombinu. Kwa hiyo, tunapongeza jitihada kwa sababu kimsingi sisi kama nchi mkiangalia hata namna ya utekelezaji wa mambo yetu, bado tuko kwenye makabrasha sana. Ndiyo maana hata Bunge hili ni miaka michache tu iliyopita ndiyo tumeingia kwenye teknolojia, hata tunatumia vishikwambi sasa hivi. Tuna mabunge mawili nafikiri ndiyo tumeanza kutumia vishikwambi. Kwa hiyo, maana yake ni lazima pia tukubali kwamba tulikuwa *somewhere behind* kwa sababu dunia ilishakwenda huko

ambako sisi *tuna-struggle* kwenda ama tuko sasa hivi tunapambana kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napongeza kwa namna yao Wizara na Serikali kwa upande fulani wamejitahidi sana, kwa sababu mpaka sasa hivi wameshaunganisha Makao Makuu ya Mikoa 26 na Wilaya 42. Wamejitahidi, tunakwenda kwa maana ya *connectivity*, kwenye miundombinu ya kusaidia Watanzania kufikiwa na huduma za kimtandao. Pamoja na hayo, bado tuna changamoto kubwa sana, kwa sababu wananchi asilimia 68 maeneo wanayoishi wana uwezo wa kupata huduma za mtandao (*internet*), lakini ni asilimia 26 tu ndio ambao wanaweza kufikia (*access*) kupata huduma ya mtandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mpaka uwe na simu janja ndiyo unaweza ukatumia *internet*. Kwa hiyo, ni asilimia 26 tu. Wakati Serikali inajaribu kuweka miundombinu na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya kimtandao, bado wananchi wetu sisi kufikia kumiliki vifaa vyenye uwezo wa *ku-access internet*, bado ni asilimia ndogo sana. Kwa hiyo, hii inatuelekeza kwamba hata tunavyozungumza *digital economy* bado kuna sehemu tuko nyuma. Kwa sababu ili tuweze *ku-access digital economy* ni lazima wananchi wetu wawe wana vifaa vyenye uwezo wa kutumia hizo *internet* ambazo tunazizungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anafahamu kwamba simu janja gharama yake ni kubwa mno. Kwa hiyo, wananchi wengi unakuta wana simu ndogo tu ya kutumia, lakini kupata kifaa au kupata simu ambayo inaweza kumpa *access* ya kuweza kutumia *internet*, wengi bado hawana uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara na Serikali kwa namna yao waangalie namna gani wanaweza wakapunguza gharama ya vifaa hivi vyenye uwezo wa *ku-access internet* ili wananchi wetu wengi waweze *ku-access internet*, waweze kupata taarifa nyingi sana ambazo zinapatikana kwenye mitandao na faida kubwa

inayopatikana kwenye suala zima la *digital economy*.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata wale ambao wana vifaa vyenye uwezo wa *ku-access internet*, bado kuna gharama kubwa sana za *data* ambazo zinasababisha hata Serikali ikose mapato kwenye kiwango ambacho ilitahili kupata. Mpaka sasa kuna ongezeko kubwa sana la matumizi ya *data* asilimia 35, lakini Serikali inapata asilimia 16 tu kwenye pato la Taifa kutokana na matumizi ya *data*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba najua kuna Tume inaitwa Tume ya TEHAMA, nafikiri miongoni mwa jukumu ambalo naweza kushauri, waongezewe, wapewe uwezekano wa *ku-regulate*, kuhakikisha kwamba makampuni ya simu yenye kupewa jukumu na TTCL kwa ajili ya kusaidia wananchi kupata *internet*, waweze *ku-regulate*. Kwa sababu unaweza kujuliza kwa nini *data* ni asilimia 35, lakini asilimia 16 tu ndiyo tunayochangia kwenye pato la Taifa. Maana yake kuna tofauti katika utoaji wa huduma za *data*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake ile Tume sasa ya TEHAMA itusaidie kuwa na *segment at least* ya kushauri na kuangalia namna wanaweza *ku-regulate* ili bei zisiwe tofauti sana. Kwa sababu, pamoja na kwamba ni huduma, tunajua pia wanafanya biashara, lakini isifike hatua kwamba wanawaumiza wananchi, wanashindwa *ku-access*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nami nina *direct interest* kwenye upande wa vijana, kwa sababu, ni ukweli usiopingika kwamba watumiaji wengi wa mitandao ni vijana. Mheshimiwa Jenista Mhagama anajua tatizo kubwa la ajira nchini, pengine vijana wengi wangukuwa na uwezo wa *ku-access internet* kwenye vifaa pamoja na *data*, wangukuwa na uwezo mkubwa pia hata wa kujiajiri. Nitakwenda moja kwa moja kwenye namna ambavyo kama Taifa, kama vijana tunaweza kupunguza tatizo la ajira na kusaidia vijana wetu kwenye kujiajiri na tukaishi kwa vitendo katika *digital economy*. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu sasa hivi anafuatilia kwenye mitandao anaona kuna *debate* kubwa kuhusiana na namna ambavyo wasanii wetu wanatengeneza pesa kwenye *viewers you tube*. Tunaishi kwenye ulimwengu ambao ni tofauti sana, inawezekana vitu vingine watu wakashangaa kabisa. Ukiwa na *viewers* milioni moja katika *YouTube* una uwezo wa kupata *USD 5,000*. *That is money* na hauhitaji *subscribers*; unahitaji *u-post content You Tube* ili watu *waka-view content* yako ili *you tube* waweke matangazo kwenye *channel* yako upate pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vijana wengi sasa hivi hawaelewi hiki kitu ndio maana mpaka sasa hivi *wana-discuss* kwamba, inawezekana kweli watu wanatengeneza *viewers YouTube*; kwamba *Diamond* katoa nyimbo siku mbili tu ina *viewers* milioni 10! *That is money, that is money*. Yaani hiyo ni pesa, kwasababu, *YouTube* wanaweka matangazo yao kwenye ile *video*. Wakishaweka hayo matangazo yao, wewe wanakulipa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 kuna kijana mdogo wa miaka saba anaitwa *Riyans' Toys Review*, *ana-post* midoli; ndio alikuwa anaongoza *YouTube*, analipwa milioni 22 *USD*. Sasa hivi nafikiri ana miaka 12 ama 10 hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna *Jeffry Star* analipwa dola milioni 200 *net worth* yake na alikuwa *ame-bankrupt* kabisa. Huyu *content* yake anatangaza bidhaa za urembo. *Actually* ni mwanaume, lakini anafanya mambo ya *entertainments*. Kwa hiyo, ana bidhaa za *make up*, anaimba *music*. Kwa hiyo, *ana-post YouTube* halafu anatangeneza *subscribers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *robots* wanatengeneza *subscribers YouTube*. Wale *subscribers* wanakusaidia kuita watu *waka-view content* yako *YouTube*. *Waki-view content* yako *YouTube* wewe unapata pesa kwa sababu *YouTube* wanaweka matangazo kwenye *account* yako na *you get paid*, lakini kuna *procedure* za kufuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wa Kitanzania hawajui kwamba *you can get paid by just posting your content*. Hata Wizara ya Maliasili na Utalii...

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa tu mzungumzaji kwamba anachosema ni kweli asilimia 100. Wasanii wetu wa Tanzania hawajui *ku-monetize*, kugeuza *viewers* wao kupata fedha, matokeo yao wanafanyiwa na Wakenya. Kwa hiyo, fedha zinaenda Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa tu mzungumzaji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Nusrat, taarifa hiyo umeipokea?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea. Tuseme tu kwenye hilo, hata Kiswahili, Wanaijeria wananunua *online* vitabu vya kufundisha a, e, i, o, u Dar es Salaam kwa shilingi 500/= wanaenda kufundisha watu Kiswahili *YouTube* na *they get paid for that*, nasi tumezaliwa na Kiswahili na tunakuwa nacho na tunakiangalia. *We don't know how to get money on it.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe kama changamoto; kwanza kwenye uwasilishaji wa juzi wa *TCRA*, Mheshimiwa Waziri na watu wako wa *TCRA* kweli mmeleta wasilisho zuri. Kwenye *issue* ya maudhui, pamoja na *capacity building* mnahitaji kufanya *capacity building* kwa vijana wengi ili tuache sasa, tutoke kwenye *ku-complain* watu waende waweke *content*. Kwa sababu, hawa waliotengeneza hizi pesa kwanza wengi ni watu ambao

hawana hata kazi rasmi, ni watu wanaoishi tu nyumbani, unahitaji tu kuwa *full time YouTube*, unahitaji tu kuwa na kitu cha *ku-post*, kwa sababu *money is the reward after solving somebody's problem. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tajiri namba mbili anayelipwa pesa nyingi *YouTube, ana-post video games*, yeye ndio anacheza *games*; zile *play station, anaji-record reaction* yake wakati anacheza na *ana-post* na watu wanakuwa *inspired*, wanakwenda *ku-view*. Sasa hiyo ni pesa. Watu wa utalii wanahitaji kutangaza utalii. Sisi kama nchi tunahitaji kutangaza, lakini sijui kama Wizara ya Utalii wana *YouTube Channel. We need YouTube Channel for that.* Tunahitaji kuwa na *YouTube Channel* kutangaza nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Nusrat kwa mchango wake mzuri kwa vijana wetu, lakini nimwambie tu kwamba kwa hapa Tanzania mwanamuziki Nassib Abdul Diamond Platnum analipwa kuanzia kati ya dola 75,000 mpaka 100,000 kupitia *YouTube. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Nusrat, taarifa hiyo.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa maana ya nia njema ila namshauri pia Mheshimiwa Shangazi akaangalie vizuri kwa sababu hii ni *updated* na Diamond hayuko kwenye *list*. Hata hivyo *is a good thing*, kwa sababu kama anaweza *aka-hit viewers* wengi kwenye muda mfupi sana, maana hiyo ni *opportunity* kubwa sana.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Ehe, taarifa.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Nusrat ni sahihi kabisa. *Regulator* wa *YouTube* yuko Kenya, kwa hiyo, anatumia hoja kwamba tunapoteza mapato mengi kwa sababu *regulator* wa *YouTube* Tanzania kwa hao wanaolipwa yuko Kenya. Kwa hiyo, tunatakiwa tuwe na *regulator* wetu sisi hapa Tanzania. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Nusrat na Mheshimiwa Waziri, umelisia hilo? Endelea Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru maana yake kama Wizara wanaona sasa kuna kazi ya kufanya. Lazima tuweke nguvu, tuweke teknolojia, tuweke utaalum, watu wakafanye tafiti watuletee ili tuone namna gani tutatengeneza pesa. Siyo tu kuweka miundombinu, tukajenge minara, hatuwezi kuishia kuzungumza minara, lazima tuzungumze tunanufaika vipi na hivi vitu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, ili hivi vitu vyote tufanikiwe kwa sababu tunazungumza faida tutakayoipata baada ya miundombinu kukaa sawa, hatuwezi pia kuacha *kuwa-recognise TTCL* ambao mpaka sasa hivi wanadai Wizara Dola za Kimarekani milioni 68. Kwa kweli mnawakwamisha sana *TTCL*, kwa sababu tunawategemea, ndiyo wanaosimamia, wanatumia mapato yao ya ndani kuendesha mfumo mzima na kuhakikisha kwamba Mkongo wa Taifa unafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunategemea hawa ndio wafike, kwa sababu tunaweza tukawa tuna *ideas* nzuri kweli watu wanapewa mafunzo waende *waka-monetize*

*YouTube Channels* zao wapate pesa, lakini kama hatuna *connectivity*, hatuna miundombinu na hawana *access* ya kutumia *internet* bado tutakuwa tuko nyuma sana, bado tutakuwa tuna *lag behind*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja la mwisho, pamoja na kwamba tumeweka kwenye *data* kwamba watu inabidi walipe ili kununua *data wa-access internet*, lakini kama Wizara tunaomba mwangalie upya kwenye machapisho ya kielimu na kwenye *document* za Kiserikali, hebu waondoe *cost za downloading*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanahitaji kupata *information*. Sasa ili *ni-download* kitabu ambacho kitanisaidia kupata maarifa ambacho pengine mwalimu anaenda kufundishia au mwanafunzi anajifundishia; wanafunzi wa vyuo vikuu mnajua, kuna *amount* unapata darasani na kuna *amount* unaenda kutafuta mwenyewe. Wako kwenye *internet* wanatafuta *materials*. Sasa kuna vitu vya msingi kama hivyo ambavyo tunaomba mwondoe *downloading cost* ili waweze *ku-access* kwa sababu ni muhimu kwao. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Ndungulile ili tuwasaidie zaidi, Serikali lazima ifanye *score-audit* kwenye *software infrastructure development index*, ndio haya yote mtaweza *kuya-catch on* aliyosema Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Nusrat pamoja na Mheshimiwa Shangazi.

Tunakwenda kwa Mheshimiwa Kapinga na Mheshimiwa Mwakasaka, atafuatia na Mheshimiwa Mbarawa ajiandae. (Makofi)

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa sasa hivi Tanzania na dunia nzima tumesimama katikati ya mabadiliko makubwa ya teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa yamebadilisha yataendelea kubadilisha namna tunavyoishi, namna tunavyofanya kazi na namna tunavyoshirikiana na watu

wengine. Huko tunakoelekea, kwa namna ambavyo mabadiliko ya teknolojia yanatokea, haina shaka kwamba kwa ujumla maisha yetu yatabadilika kwa kasi ambayo tusiyoitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunakumbuka, tukiangalia hapa tulipo na tulipotoka, mapinduzi ya kwanza ya viwanda namna ambavyo yalikuwa yanaendeshwa, yalikuwa yanatumia njia ya maji pamoja na mvuke, yaani *waterna steam power*. Mapinduzi ya pili *yali-advance* kidogo yakawa yanatumia *electronic power*, mapinduzi ya tatu yakaenda yakawa yanatumia *electronics and information technology*. Hapa tulipo sasa hivi *yame-advance* kiasi cha kwamba tunatumia mchanganyiko wa nguvu kazi yaani za mikono, kidijitali na mbinu za kibaiolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya ili niweze kueleweka kwamba hapa tulipo tuko katika nyakati ambazo hazijawahi kutokea katika historia ya dunia na mabadiliko yanayoenda sasa hivi kwa kasi ambayo yanatokea haijawahi kuwa *recorded* toka dunia imeanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema pia ili tuone umuhimu wa kuwekeza katika masuala ya teknolojia, sayansi pamoja na uvumbuzi, lakini hatutaweza kufanikiwa kwa sababu masuala yote yanayohusiana na sayansi, teknolojia, uvumbuzi, mawasiliano na habari hayajawekwa pamoja katika nchi yetu, yaani yameparanganyika. Yapo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lakini masuala ya *information* na *communication* na *ICT* yako kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu kama tunavyofahamu ni dubwana kubwa namna hii, masuala ya sayansi na teknolojia, hayawezi kuendelezwa pale kwa kasi ambayo sisi tunaitaka na ndiyo maana leo hii nataka nishauri Serikali yangu sikivu. Wakati umefika sasa *tu-centralize* masuala yote yanayohusiana na sayansi, teknolojia, uvumbuzi, habari na mawasiliano kwenye sehemu moja. Sehemu sahihi ni Wizara hii ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kwa nini *tu-centralize* leo? Ni kwa sababu tunapaswa kujisuka upya ili tuweze kwenda na kasi ambayo dunia inaenda. Lazima tukae kwenye mstari ambao *the rest of the world* wapo. Leo hii tulipokaa hapa nchi 24 duniani zimeshaweka makubaliano ya kumaliza matumizi ya mafuta ya petroli kuanzia mwaka 2025, ina maana watakuwa wanatumia magari ya umeme ama magari ya gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tulitakiwa tuwe tuna mkakati wa kutuwezesha sisi kuungana na dunia kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwekeza kwa wataalam ambao wanaweza kubadilisha mifumo yetu ya magari kwenda kwenye mifumo ya magari aina ya umeme na gesi. Haya yote hayawezekani kwa sababu mambo yote haya yamekuwa *decentralized*. Hakuna sehemu moja ambapo tunaweza tukajisuka kama nchi na kwenda katika kasi ambayo dunia yote inaenda leo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni rai yangu kwa Serikali ya chama change, ni wakati umefika *tu-centralize* sayansi, teknolojia, uvumbuzi, mawasiliano na habari kwenda kwenye Wizara hii ili yaweze kufanyiwa kazi kwa kasi ambayo sisi tungeitamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia kwa mfano leo, kuna nchi kadha wa kadha zinanufaika na *startup program* za vijana kwa sababu wamejisuka na *system* yote imekuwa *centralized*. Leo *South Africa* wanaingiza takribani *1.3 trillion* kwa *startup program* 10 tu za vijana. *Imagine* pesa ambayo Serikali yao inapata kama wana *startup programs* 100. Kenya tu hapo wamewekeza kwenye *startup programs* na wanapata zaidi ya *USD* milioni karibia 300 kwa *program* 10 tu. Sisi tunaweza kufanya haya; *startup programs* chini ya *COSTECH* hazijipambanui zaidi kiuchumi kwa sababu hazijaweza kusukwa ipasavyo kwa mifumo ambayo tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema vijana wa Taifa hili watapata ajira zile milioni nane kwa urahisi kama

tukiwekeza kwenye masuala ya teknolojia na hizi *startup programs*. Kwa sababu *startup programs* 10 tu zina uwezo wa kuajiri mpaka vijana 1,000. Sasa *imagine* una *startup program* 100. Ndio maana naendelea kuisisitiza, ni wakati umefika kujisuka upya masuala yote yanayohusiana na sayansi, teknolojia na uvumbuzi yawe *centralized* hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya *ICT* iko chini ya Wizara ya Mawasiliano lakini Sera ya Sayansi na Teknolojia, tena ya siku nyingi, iko Wizara ya Elimu. Sera ya Uvumbuzi mpaka leo mwaka 2021 hatuna Sera ya *Innovation* kwenye Taifa letu. Ndiyo maana nazungumzia habari ya *ku-centralize* masuala haya ili yaweze kufanyiwa kazi katika sehemu moja na tuweze kupiga kasi. *Trust me not*, ikifika 2025 hapa tutatafutana kwa sababu dunia inaenda kwenye kasi ambayo haijawa *recorded* sehemu yoyote ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye masuala yanayohusiana na *ma-bundle*. Kumekuwa kuna malalamiko kwa walaji wengi kwamba *ma-bundle* wanayotumia yanaenda kwa kasi mno. Inawezekana ikawa ni matumizi, lakini kuna tatizo sehemu. Wizara ilielekeza haya makampuni ya simu yaweze kuweka mita zinazoonyesha utumiaji wa *ma-bundle*, lakini tatizo linakuja kwenye *speed* ya *ma-bundle* ambayo tunauziwa. Hizi zinaitwa *MPDS* hazijawekwa wazi. Kuna makampuni wanatutoa *speed* ya 3 - 5 *MPDS*, lakini sasa *ma-bundle* tunayouziwa, leo *Vodacom* akinipa mimi *bundle* la 2GB na *Tigo* akinipa *bundle* la 2GB inawezekana la *Vodacom* likaisha kabla ya *Tigo* kwa sababu haijawekwa kwamba *bundle* la 2GB ambalo ninapewa inabidi liwe la *speed* gani, *MPDS* ngapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana watumiaji wa mtandao mmoja wanalalamika kuliko watumiaji wa mtandao mwingine, kwa sababu hatuna hata kipimo na hatuwezi *ku-trap* matumizi ya mitandao yetu. Ndiyo maana leo unaweza ukanunua 2GB ikaisha. Ni haki kwa Mtanzania kulalamika kwamba *bundle* langu linaisha kama upepo, kwa sababu hatuambiwi *speed* ya *ma-bundle* tunayotumia ni *MPDS*



ngapi; na ni vigezo gani vinatumika? Kwa hiyo, labda ifike kipindi tuuziwe *ma-bundle* kwa mantiki ya *speed* basi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaambiwa Watanzania ni nchi ya nne kwa *ma-bundle* rahisi Afrika; lakini sasa kama *bundle* langu nanunua kwa bei rahisi napewa *GB1* sawa, baada ya saa moja, nanunua tena *GB1*, hiyo ni rahisi *in terms of quantity or in terms of speed*? Kwa hiyo, ifike mahali sasa Wizara ituangalie hapa; kuna jambo hapa kwenye masuala ya *ma-bundle*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wangu wa pili naomba nizungumzie kuhusu masuala ya matumizi ya *internet*. Naipongeza Serikali, watumiaji wa *internet* wameongezeka mpaka kufikia milioni 29, lakini nachelea kusema kwamba watumiaji hawa kwa kiasi kikubwa ni watumiaji wa mijini. Sisi kule kwetu Mbinga Kata 29 na vijiji 117 hatuna *internet*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani vijiji vyote 117 tunahangaika, mpaka tufike mjini ndiyo tuweze hata kutuma *document* ama kufungua *document* kwenye simu. Naomba Waziri wakati anakuja hapa, atueleze sisi wananchi wa Mbinga Vijijini ni lini tutatuliwa matatizo yetu ya *internet*? Leo hii kata zote 29 na vijiji 117, jamani naomba Waziri atuambie sisi wananchi wa Mbinga Vijijini tutafanyaje? Maana sasa tunakosa cha kufanya. Tunaomba tuangaliwe tupate na sisi *3G* kwa sababu vijana wengi wako kule vijijini, siyo kwamba vijijini hamna vijana ambao wamesoma. Wanataka kuuza kahawa zao kwenye mitandao, wanataka kuuza unga wao kwenye mitandao, tuletewe na sisi kule ili tusije kufanya kazi mjini tukae kule kule kwetu tuuze biashara zetu kule kule tulipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunafahamu kwamba mawasiliano ya simu ndiyo maisha siku hizi, lakini kata saba hata kupiga simu huwezi. Kata hizo, naomba niweke kwa *record*; Kitura, Kipololo, Ngima, Mhongozi, Ukata, Amanimakoro, Kihangimauka; na hapa Mheshimiwa Waziri

nataka nikupe taarifa nitashika shilingi, naomba utuambie ni lini kata hizi zitapata mawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mpaka sasa hivi michango imekuja kitaalam nawapongeza sana. Mheshimiwa Waziri kuna makampuni mliwapa leseni kwenda vijijini wameingia mitini. Wote wamekimbillia mijini, *this the time* ku-empower TTCL wakachukue wakai-cover Tanzania nzima. Ninavyosema kuhusu *program*, kuna program za IOT (*Internet Of Things*). COSTECH walianza vijana walipeleka Bandarini ku-monitor na kuhesabu zile *container* zinazolingia na kutoka kwa mtandao, *very simple* hata wewe ukikaa hapo unaweza ukaitazama *movement* za ma-*container*, lakini hakuna mtu anayewasikiliza.

Tuendeleo Mheshimiwa Mwakasaka ajiandae Mheshimiwa Profesa Makame M. Mbarawa.

Waheshimiwa, nami ndio nachangia maana nilikuwa nichangie leo, sasa ndio nachangia kabisa hapa. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka. halafu Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Mawasiliano. Wenzangu wamechangia zaidi kwenye maeneo mengi ambayo ni mazuri lakini mimi nitachangia katika maeneokama matatu. Kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa namna ilivyoweza kudhibiti hasa wizi unaotokana na fedha ambazo zimekuwa zikiibiwa kwenye simu za kimataifa. Naipongeza sana Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wizara imeweza kudhibiti kwa kiwango kikubwa wizi unaotokana na mitandao. Wizi wa ndani kwa sasa hivi umeongezeka kwa

kiasi kikubwa na kwa sababu kuna *TCRA* vile vitengo vya *Cibber crime* vina uwezo wa ku-*tress*hawa wezi. Kwa sababu sasa hivi mtu anakuibia kama alivyosema mchangiaji nadhani alikuwa ni wa pili. Watu wanaiba kwa kutumia mitandao na zile simu zinajulikana na wale watu wanaendelea kutumia zile simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikisikia Tigo wamepiga wameniambia hapa ni *customer service* huwa nakata pale pale sisikilizi chochote, kwa sababu mimi ni mmoja wa wahanga. Nilipigiwa *customer service* ya Tigo walivyoniambia tu ni *customer service* nikawaambia kwamba nitawaaminije kama ni ninyi? Wakanipa *data* zangu zote ambazo nimefanya ile miamala ya mwisho. Kwa hiyo nikawaambia hakuna shida, wakaniambia tumekuongeza kutoka kutuma shilingi 3,000,000 sasa utatuma shilingi 5,000,000 kuna ujumbe unakuja hapo utabonyeza *okay*. Ujumbe kweli ulikuja nilipo bonyeza *okay* nikaambiwa nimetuma shilingi 711,000 na kila kilichopo nikabaki na *zero balance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninavyoamini ni kwamba inawezekana hawa wengine pia ni watumishi wa mitandao hii au ni wale ambao wanafundisha wenzao namna ya kutuibia. Wasiwasi wangu ni kwamba inaweza ikafika mahali kwa *advancement* hii ya watu wa mitandao, unaweza ukajikuta hujafanya *transaction* yoyote lakini huko tunakokwenda unaweza ukajikuta unaangalia *balance* yako kwenye simu hakuna senti tano. Kwa hiyo naishauri Wizara awa wenzetu upande wa polisi ambao tunaambiwa kwamba ndio tuwe tunaripoti tunapotapeliwa, wawe karibu sana na watu wa *TCRA* ili waweze ku-*trace* hizo namba ambazo zinafanya wizi huo wa kimtandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine hili ni la kiusalama mimi na kerwa sana, unapiga simu yako na hili ni mitandao karibu yote. Unapiga simu, kabla haijaanza kuita wewe unapewa matangazo, simu yako inaunganishwa, bonyeza sijui, *hash* sijui, yanaanza matangazo halafu simu ndio inaita. Sasa mimi najiuliza kama ulikuwa unapiga simu ya *emergency* labda mtu kavamiwa labda na majambazi,

anapiga simu ili labda Polisi wapokee ile simu, yanaanza matangazao yao ambayo sisi hatujawaomba kama tunataka hayo matangazo kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wewe wakati unasikiliza matangazo yale, unaweza ukapata hasara, kwa nini wasiendeleo na matangazo yao kwa mitindo mingine, lakini mteja yeye akipiga ile simu iite moja kwa moja kuliko kuikawiza kwa sababu ya mambo ya kiusalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Minara ya Simu; miji inaendelea sana, kwa mfano mimi nime-experience kitu kimoja na ni wengi hapa Dodoma na sasa muda mrefu kunakuwa na shida ya simu zetu wenyewe *either* kupiga au hata kupatikana. Nahisi ni *conjunction* ya mitambo yenyewe, yaani kwa maana ya minara. Wakati mji kama Dodoma haujawa Jiji, minara ilikuwa ni hiyo hiyo iliyopo na kama imeongezeka ni michache sana. Sasa matokeo yake kunakuwa na foleni kubwa sana ya simu na meseji. Unaweza ukatuma meseji leo ikawa *delivered* kesho. Pia unapopiga simu kunakuwa na shida ya kupatikana kwa simu. Kwa hiyo, nawaomba Wizara waweze kuongeza minara hii ya simu ili mawasiliano yaweze kuwa mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba sana Ndugu yangu Waziri Ndugulile, jiografia ya Tabora anajua, kwa mfano, Jimbo langu la Tabora Mjini linaitwa mjini tu, lakini lina vijiji 41. Vijiji vingi havina mawasiliano ya simu, ukienda kwa mfano, Kata za Ndevelwa, Uyui, Kabila, Ntarikwa, Tumbi hizo ni kata za nje, ukienda lkomwa ambayo inapakana na Nzega kule mawasiliano ya simu ni magumu sana. Hata hivyo, pale pale mjini eneo la Kipalapala ambapo halizidi kilometa mbili, kuna shida ya mtandao wa simu.

Kwa hiyo naomba ndugu yangu Ndugulile atufikirie kupeleka minara mingine ya simu katika maeneo yale ili mawasiliano yaweze kuwa mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita hasa kwenye eneo la miundombinu kwa sababu kubwa kama tunazungumzia *digital economy*, kama tunazungumzia maudhui, kama tunazungumzia chochote kile kwenye sekta hii ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano jambo muhimu ni miundombinu sahihi. Ndio sababu Serikali yetu iliamua kujenga miundombinu sahihi, miundombinu mahiri, miundombinu ya uhakika kwa kuhakikisha kwamba Watanzania hawa wanapata huduma safi na salama ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kwanza kwenye sekta hii eneo la Mkongo wa Taifa. Kama unavyofahamu na Watanzania wote wanavyoelewa kwamba Serikali yetu imewekeza kwenye Mkongo wa Taifa mabilioni ya fedha. Mpaka sasa hivi tumejenga takriban kilometa 7,450 ambazo zimeunganisha mikoa yote ya Tanzania pamoja na nchi jirani, kwa maana inaunganisha nchi yetu na nchi za nje. Tunafanya vizuri na nchi yetu sasa imekuwa kituo mahiri kwa ajili ya muunganisho wa sekta ya mawasiliano. Pia tumeona taasisi nyingi za Serikali tunatumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna eneo ambalo bado hatujafanya vizuri. Eneo hili ni eneo la elimu mtandao, matibabu mtandao, biashara mtandao, kilimo mtandao na kadhalika. Watu wengi hapa wanazungumzia kuhusu maudhui, maudhui yanapatikana hasa kama tunakwenda kwenye elimu mtandao kwa sababu tunasomesha vijana wengi, tunawapa nafasi nyingi, matokeo yake vijana hawa wanaweza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hatujafanya vizuri kwenye maeneo haya, kwanza, ni kwa sababu *bundle* yenye kasi kubwa *high speed internet bandwidth* ipo bei juu. Pili, kumekuwa na shida ya *excess network, last mile connectivity*. Maeneo mengi ya mjini yanayo *internet* lakini ukitoka nje ya miji kuna shida, tumefika kwenye wilaya lakini bado kuna shida ya *connectivity*. Tatu, kunatakiwa taasisi maalum ambayo itasimamia mkongo kwa uwezo mzuri zaidi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunaishauri *TTCL* ambayo ndiyo shirika letu la mawasiliano likishiriana na Wizara iweze kutoa *bandwidth* hasa kwa Vyuo Vikuu na hospitali kwa bei nafuu ili kuwawezesha watu hao kufanya elimu mtandao, waweze kufanya matibabu mtandao na kadhalika. Naamini tukifanya hivyo tutaweza kutumia mkongo wetu vizuri na utaleta faida kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Sasa hivi wakati mwingi tunatuma mkongo kwa ajili ya simu, kupeleka meseji huku na kule, kupeleka picha huku na kule lakini hatujautumia ipasavyo hasa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuchangia ni kuhusu miundombinu ya *data center*. Pale Kijitonyama tumejenga mfumo wa kisasa wa *data center*. *Data center* ile ni ya kisasa, nathubutu kusema kwamba katika Afrika ya Mashariki ndio *data center* kubwa na ndiyo yenye uwezo wa kisasa. Ina kiwango kinachoitwa *tier-3* ambayo inatambulika kimataifa. Hata hivyo, bahati mbaya sana, taasisi chache hasa sekta binafsi zimejiunga na mfumo ule. Nachukua fursa hii kuiomba Wizara itumie muda mwingi kuhamasisha watu wengi waweze kujunga na taasisi ile au *data center* ile. Kwa sababu watu wengi wakijiunga na *data center* ile tutapata fedha zaidi, tutaweza kupata *hub grade*, tutaweza kufanya mambo mengi na Watanzania watafaidika zaidi na mfumo ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya *data* ni biashara muhimu sana duniani na kila nchi inafanya biashara ya *data*, lakini hapa kwetu bado hatujachangamkia sana fursa ile na

Serikali imewekeza shilingi nyingi karibuni, kama sikosei Dola za Kimarekani milioni 91 zimewekezwa pale kwa ajili ya kujenga *data center*. Kwa hiyo naomba sana Wizara, naomba sana *TTCL* na wadau wote waitumie fursa ile kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Pia ile *data center*iko pale tu Kijitonyama lakini ipo haja ya kujenga na maeneo mengine kwa mfano hapa Dodoma na Zanzibar kwa sababu lazima tuwe na *backup*. Ikitokea la kutokea leo pale Kijitonyama tutapoteza *data* nyingi ambalo hilo litakuwa siyo jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo naomba wizara ifanye jambo hili na iweze kuchangamkia, waweze kujenga *data center* moja hapa Dodoma, nafikiri mpango huo ulikuwepo na vile vile waweze kujenga *data center* nyingine huko Zanzibar. Tukifanya hivyo *data* zitakuwa salama na nchi yetu inaweza kufanya biashara kubwa ya *data*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *PKI - Public Infrastructure*, hili ni jambo kubwa sana na Wizara wanalifahamu na wamejipanga, naomba waongeze kasi ya kutengeza jambo, kwa sababu mfumo huu ni muhimu sana hasa kwenye usalama wa miala tunayofanya. Kama unavyojua sasa kila mtu sasa hivi ananunua vitu kupitia kwenye mitandao, ananunua vitu kupitia kwenye simu, lakini usalama wa miamala hiyo bado ni shida. Kwa hiyo, tukianzisha mfumo huu wa *PKI*, naamini kwamba sasa tutajipanga vizuri na tutaweza kufanya kazi vizuri na nchi yetu itafaidika katika teknolojia hii ya habari na utangazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, sasa naomba kuunga mkono hoja na nafikiri tunaendelea vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwaifunga, ajiandae Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya

Wizara hii ya Mawasiliano. Kwanza nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge na leo umekalia kiti hicho. Naomba Mwenyezi Mungu akuongoze uendelee kuwa na hekima kama ilivyokuwa hapo awali tuendelee kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya masuala ya ma-*bundle*. Wananchi wengi sana wamekuwa wakilalamikia wizi mkubwa unaofanywa katika ma-*bundle*. Unapoweka *bundle* unapewa *expire date*, unaambiwa kwamba hii utatumia kwa mwezi mmoja, utatumia kwa wiki moja, utatumia kwa siku moja, lakini unaweza usitumie kwa mwezi mmoja, lakini inapofika ule wakati wanakufyeka inabidi uweke fedha nyingine sasa fedha hizi zinakwenda wapi? Tungeomba sana Wizara ya Mawasiliano waangalie jambo hili, limekuwa likipigiwa kelele sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichofanya wamerudisha vifurushi vile ambavyo gharama ambazo zilikuwa hapo zamani. lakini, bado kuna hitaji kubwa sana la wananchi kutumia vifurushi hivi, lakini gharama hizi zinaonekana ni kubwa hasa kwa wananchi wa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anawasilisha hapa amezungumzia kuhusiana na masuala mazima ya kesi za wahalifu wa mitandaoni. Mheshimiwa Waziri hajatuambia mpaka sasa, ni kesi ngapi mpaka sasa zimeshatolewa maamuzi. Kwanza zipo ngapi, lakini ni ngapi mpaka sasa zimeshatolewa maamuzi. Pia ni adhabu gani zinazochukuliwa kwa watu hawa wanaohusishwa na uhalifu wa mitandaoni. Labda wakisema wazi pengine haya mambo yanaweza yakapungua kulingana na adhabu ambazo zinatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya *TCRA* kufungia Vyombo vya Habari bila kuwaita na kuwasikiliza. Tunataka kujua, haki iko wapi kama unamfungia mtu bila kumsikiliza. Malalamiko yamekuwa makuwa hasa kwa hawa wanaotumia mitandao ambao



vyombo vyao vya habari viko mitandaoni. Wanafungiwa sana bila hata kuitwa na kusikilizwa na wao waweze kujieleza. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali iwe inafanya utaratibu wa kuwaita wale wanaowafungia, wawasikilize, wakishawasikiliza ndiyo waweze kufanya maamuzi kuliko kuwaumiza kama ambavyo wanafanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ufungaji pia wa vyombo vya habari kama magazeti na magazeti haya yamekuwa yakichaguliwa, yapi yafungiwe na mengine yasifungiwe. Sasa tungetaka kujua, Serikali ituambie ni utaratibu upi au ni maudhui gani yanayotakiwa kwenye gazeti yaandikwe ndiyo gazeti lifungiwe na gazeti hili lisifungiwe. Kwa sababu unaona kuna magazeti mengine yanaandika vitu vya ajabu lakini utashangaa magazeti haya hayafungiwi, yanafungiwa magazeti mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba tufahamu na tujue haya magazeti yanayofungiwa, yanafungiwa kwa makosa yapi na haya ambayo yanaendelea kuwepo na tunayaona mitaani yakiandika vhabari za ajabu, yenyewe yanakuwa na uhalali gani wa kuendelea kuwepo kwenye tasnia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nishauri kidogo Serikali kuhusiana na suala zima la ruzuku. Ningeishauri Serikali iondoe mpango wa kutoa ruzuku kwa watoa huduma za *internet* ili kupunguza gharama za upakuaji wa mada ama machapisho ama vitabu. Tunafahamu kabisa sasa hivi hata wanafunzi wanapewa masomo yao katika mitandao. Sasa wanapokuja kwenye suala la kupakua unakuta kwamba gharama inakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, nashauri Serikali ingejitahidi kutoa ruzuku ili basi wanafunzi hawa na hata maeneo mengine ya watu wa Serikalini ambao wanafanya machapisho mbalimbali ziweze kuwa hazina gharama zozote, yaani iondolewe kabisa na iweze kuwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka Mkoa wa Tabora. Moja kati ya Mikoa ambayo ina changamoto kubwa sana ya mawasiliano, unaweza ukajikuta umetembea hatua

chache tu huwezi kupata mawasiliano. Amezungumza hapa Mbunge wa Tabora Mjini lakini naomba niongezee. Jimbo la Tabora Mjini lina Kata 29, katika kata hizi 29, Kata 12 ni Kata za Vijijini. Unapokwenda kwenye Kata hizi, ukitoka tu kwenye kata ya mjini ukaingia kwenye kata ya vijijini mawasiliano yanakata kabisa. Kwa hiyo, hata kama unakuwa na changamoto yoyote ambayo umeiacha huku mjini, mtu anapokutafuta huwezi kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Wizara iangalie maeneo haya iweze kutupelekea minara ili wananchi wale na wao waweze kupata huduma ya mawasiliano. Kwa sababu, inafika mahali mtu anapotaka kupata mawasiliano lazima apande kwenye eneo la mwinuko...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ya pili hiyo, ahsante na mwinuko.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa. Jiandae Mheshimiwa Joseph Tadayo.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Rais wa Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassan wakati anawaapisha Mawaziri katika hotuba yake alisema haya maneno, naomba ninukuu. *'Competitiveness ya TTCL* iangaliwe vizuri kwa sababu hili ndilo shirika letu na tunategemea lishindane na mashirika mengine ya *private sector*. Kwa hiyo, *competitiveness* hiyo ikoje? Tuangalie vizuri tutoe nini, tuache nini, turekebishe ndani ya TTCL ili shirika lisimame vizuri'. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia nukuu hii ina maana nzito na kubwa sana katika mustakabali wa

maendeleo pamoja na ushindani wa Shirika letu la *TTCL*. Imesemwa hapa na baadhi wa Wabunge kwamba kila mwaka mashirika binafsi ama mashirika shindani na *TTCL* yanawekeza kati ya milioni 100 dola mpaka milioni 150. Lakini, shirika letu la *TTCL* linawekeza sifuri. Halafu tunategemea hapa uwepo ushindani ama uwepo ufanisi wa biashara katika shirika letu hili la *TTCL* na mashirika haya mengine shindani ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* shirika *giant* kama *Vodacom* kila mwaka linawekeza milioni 100 lakini kashirika ketu ka-*dwarf* kanawekeza sifuri. Kwa hiyo, hapa ule ushindani tunaoutafuta hatuwezi kuupata. Imesemwa hapa teknolojia inakua kila leo na inakua kwa kasi kubwa sana. Kwa maana hiyo, tunapozungumzia teknolojia uwekezaji wake unahitaji fedha nyingi na unahitaji fedha ya kutosha. Sasa tunaambiwa Shirika letu la *TTCL* ndani ya miaka 10 halijawahi kufanya huo uwekezaji. Mara ya mwisho shirika hili liliwekeza mwaka 2001. Sasa tuangalie kutoka mwaka 2001 mpaka leo 2021 hapa katikati teknolojia ime-*change* kwa kasi na kiasi gani. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesisitiza tena, akina *Vodacom* wanawekeza kiasi kikubwa lakini sisi ndani ya miaka 10 mfululizo tumewekeza sifuri, sifuri. Sasa kwa kuwa sasa hivi Tanzania tumekuwa tunaelewa sana masuala ya mpira hapo ukifanya ulinganifu yaani uichukue ndondo *cup* iende ikacheza kule Barcelona. Ama uichukue Simba iende ikacheze na Arsenal. Juzi wamecheza na Kaiza wamefungwa goli nne, sasa pata picha iende ikacheze na Barcelona, majibu na matokeo hapa wote tunayo kwamba itachezea kipigo cha mbwa koko. Kwa hiyo, ninatoa mfano huu kujaribu kuonesha kwamba Arsenal ndiyo *giant* hawa *Vodacom* halafu Simba ndiyo hii ndondo *cup* ninayotolea mfano. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama hakika hatuwezi kupata tija inayotafutwa. Kwa hiyo ushauri wangu kwa Serikali, Serikali toeni mtaji ipeni *TTCL*. Malalamiko yote yanayolalamikiwa hapa na pia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ilisema kwamba wawekezaji binafsi wanawekeza

sehemu zenye mvuto wa kibiashara. Kule ndani ndani, *interior* wenyewe huwa hawawekezi, ni shughuli yetu Serikali kuwekeza. Kwa sababu hiyo, tuna kila sababu Serikali kuipatia mtaji *TTCL* ili iweze kuwekeza kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili *TTCL* iweze kusimama, mtaji wake wa awali tu inahitaji bilioni 800 za Kitanzania, huo ni uwekezaji wa awali wa mwanzoni kabisa. Inawezekana kwamba fedha hizi zinaonekana kuwa nyingi kwa sababu tunazo huduma muhimu za kijamii kama afya, elimu na maji pengine sasa Serikali inapata ugumu na ukakasi kupeleka fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini tusiwaruhusu sasa waende wakakope? Kwa muda mrefu nikiwa mjumbe wa hii Kamati, ushauri tuliokuwa tunaishauri Serikali iruhusuni *TTCL* iende ikakope *concession loan*, mkopo wa gharama na masharti nafuu ili iweze kuwekeza ifanye kazi shindani na kazi yenye tija kama ambavyo tayari imeshatangukiwa kusemwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema hapa Waheshimiwa Wabunge kwamba *TTCL* inaidai Serikali na Wizara fedha nyingi tu za kutosha na ukiangalia ripoti ya *CAG* ya mwaka 2019/20 katika ukurasa wake wa 337 inasema kwamba *TTCL* ilipaswa ilipwe zaidi ya shilingi bilioni 15. Hii ni kutokana na huduma ya mkongo. Lakini ripoti ya Kamati imetuambia mpaka hivi leo tayari imeshafika dola za kimarekani milioni 68. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tunaweza tukaona ni fedha kiasi gani ambayo *TTCL* wanaitafuta, Serikali mko mmeishikilia. Kinachoumiza hapa, *TTCL* inatoa mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuendesha na kuhudumia mkonge ambapo taasisi binafsi zinatoa hizi huduma za simu kwa kupitia mkongo huo. Niseme kuwa wanalipa, lakini kile kinacholipwa kinaenda kwenye Wizara, sasa tunamkamua ng'ombe huyu *TTCL* pasipo kumlisha majani. Kwa maana hiyo, Serikali muda umefika wa kuhakikisha mnatoa hela mnawapa *TTCL* ili waweze kufanya kazi yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia ripoti hiyo hiyo ya CAG inasema *TTCL* inadai Serikali madeni ya huko nyuma ya miaka 10 karibu bilioni 40. Kwa hiyo, kuna hizi milioni 68, kuna hizi bilioni 40, zote hizi tukiwapatia *TTCL* angalau watakuwa na sehemu ya kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imesemwa hapa naomba nisisitize kwamba taasisi ama mashirika ya umma yanapata huduma kutoka katika shirika letu hili la *TTCL* lakini kimsingi hawalipi. Wanapata huduma ya *Internet*, wanapata huduma ya *data*, wanapata huduma ya simu, hawalipi! Sasa tukitegemea kwamba eti siku moja *TTCL* ije ifanye maajabu hii *TTCL* itakuwa tu kama *zombie*, ilikuwepo, inakufa, tukaifufua kwa sheria tena mpya sijui 2017 tulifanya marekebisho ya sheria, leo tunajaribu kushauri tena tena lakini bado Serikali haitaki kupokea ushauri wetu. Ama hakika, hili shirika litakufa tena halafu tutegemee litakuja litafufuka tena huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya manunuzi, Sheria ya Manunuzi ya Umma tunaiona ni kwa jinsi gani ambavyo ina mchakato mrefu na mgumu. Kwa mashirika kama *TTCL* na yanayofanana na hayo kama *ATCL*, hebu sasa Serikali ifike wakati, ifike mahali mtengeneze kanuni mahsusi kwa ajili ya mashirika haya ya umma yanayofanya kazi kibiashara, kwa sababu leo *Vodacom* wakitaka kununua mitambo mipya, wakikaa tu ile Bodi, wakijadili wakiamua ikionekana inafaa, kesho wanaenda kununua. Lakini, *TTCL*, ni mchakato utachukua mwezi mzima hata mitatu ili waweze kukidhi mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ili waweze kununua hiyo mitambo, wafunge mitambo kwa ajili ya kuweza kutoa huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie na Mkoa wangu wa Pwani. Maeneo mengi ndani ya Mkoa wetu wa Pwani kumekuwa na kusuasua kwa mawasiliano. Ukichukua kwa mfano katika Wilaya ya Mkuranga maeneo ya Sotele, Chamgoni, Kibuyuni pamoja na Mbezi, huku mawasiliano ya simu imekuwa ni changamoto. Lakini pia kwa upande wa wilaya ya Kibiti, maeneo ya kule Delta, Msala kule,

Kihomboloni, changamoto kubwa ya mawasiliano. Pia ukichukua kwa upande wa Mafia, visiwa vya Jibondo na visiwa vya Chole, mawasiliano yamekuwa yakisuasua. Hata kule kwa Mheshimiwa Jaffo, maeneo ya Mafizi, maeneo ya Manyani, vikumburu, mawasiliano yamekuwa ya kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, tunamuomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu, pasipo hivyo, jioni tunakusudia kushika shilingi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Tadayo, jiandae Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Nicodemus Henry Maganga.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia na hasa kupata nafasi ya kuzungumza baada ya Mheshimiwa Mchafu kuzungumza ili tu uniruhusu nimpe kataarifa kidogo kwamba tutakapocheza Simba na Arsenal tutawafunga sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri lakini niipongeze zaidi Kamati kwa sababu wasilisho lao limesaidia hata uchangiaji wetu kwenda vizuri. Wamefanya kazi nzuri sana. Amesema mambo mazuri sana katika hoja ya Wizara hii. Nizungumze machache sana nikianza hasa yanayohusiana na Jimbo langu la Mwanga. Sehemu ya ninachotaka kuzungumza, kimeguswa juu ya mawasiliano katika maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mwanga lina Kata 20 na katika hizo, Kata 6 ziko kwenye maeneo ya mipakani na pengine kwa kumbukumbu nikizitaja tu. Kuna Kata ya Kileo, Kivisini, Jipe, Kigonigoni, Kwakoa na Kata ya Toloha. Zaidi ya nusu ya maeneo haya ukiingia na simu yako ya mkono kuna mahali unafika unaambiwa karibu *Safaricom*, sasa *Safaricom* na haya ma-*bundle* ya vijana wetu akifika kule hapati mawasiliano. Ni kijana wa bodaboda alikuwa

kule, mteja wake anamtafuta hampati, wanapoteza *income*.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wenzetu wa *TCRA* wanapotoa leseni pia wana jukumu la kufuatilia mambo ya udhibiti ubora. Wasiachie haya makampuni yanawekeza kule halafu hawajali juu ya ubora wa huduma zao wanazozitoa kule wanaendelea kutuumiza. Hili jambo nashukuru kwamba Mheshimiwa Ndugulile alishaanza kunong'ona na sisi Wabunge ambao tunatoka kwenye maeneo ya mipaka naamini kabisa kwamba atalitia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko kata nyingine ya Mlimani ambayo kuna mnara wa Halotel lakini ule mnara unatumia *solar*, sasa kule kwetu ni kama Uswisi. Wakati mwingine hatuoni jua kutwa nzima. Kwa hiyo, siku kama hakuna jua basi na mawasiliano hakuna. Mimi sidhani kampuni kubwa kama ile inasubiri umeme wa *REA*, wavute nguzo ziende pale ili mawasiliano yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu baada ya hapo nije tu kwenye hoja moja ya Kitaifa ya *TTCL* ambayo imezungumzwa sana na ninasema hivyo kwa sababu ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 96 imezungumzia juu ya kuwekeza kwenye shirika hili la mawasiliano. Shirika hili tunapozungumzia juu ya kulifufua, kupata *National Telecom*, nafikiri ni sawasawa na tulipokuwa tukizungumzia habari ya kupata *National Carrier ATCL*, kwamba ni jambo la muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika nchi nyingi, mashirika haya, hizi *National Telecoms* ni mashirika makubwa sana ukianza Egypt *Telecom* ni shirika kubwa tu, ukienda *BOTNET* Botswana ni shirika kubwa, China *Telecom* ndiyo usiseme na *Ethio Telecom* ya Ethiopia, *turnover* yake kwa taarifa za 2020 ilikuwa ni dolla bilioni 1.35. walipoelekea tu kutaka kutoa asilimia 45 ya hisa wawekezaji walifoleni pale kwa sababu ni shirika ambalo lina tija kubwa sana. *TTCL*, halikadhalika tukiwekeza kwa ile miundombinu ya msingi ambayo tayari ilikuwepo, tukiwekeza na kuiboresha inaweza

ikawa kampuni kubwa, ikaleta ajira nyingi na ikaleta kodi nyingi ukiacha faida nyingine nyingi ambazo zimezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza kidogo hapa, kuna watu walitaja juu ya uwekezaji kwenye Sekta hii ya Mawasiliano. Hawa watu walionunua *TIGO* na *ZANTEL*, *Exim* nilisoma kwenye gazeti la *East African*, lazima nikiri hii ni taarifa ya kwenye gazeti wana mpango wa kuwekeza mbali na fedha walizonunulia, wanawekeza dola milioni 400 ndani ya miaka mitano kufufua haya mashirika. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba sisi tukizungumzia uwekezaji mdogo mdogo tutaendelea kucheza hapa hili shirika halitafufuka na tutaendelea kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mchango wangu ni mfupi kwa sababu mengi yamezungumzwa. Naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, jiandae Nicodemus Henry Maganga.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala, ninaomba nichangie kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano. Kwanza kabisa, naomba nijielekeze kwenye suala zima la usalama wa fedha za mtu anaye-*transfer* fedha kutoka kwenye mtandao mmoja kwenda kwenye mtandao wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa kwa watumiaji wa mitandao wanaofanya *transfer* kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao wa pili juu ya usalama wao wa fedha mahali ambapo wanakosema kutuma fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano na mwenyewe ni muathirika, mimi ni mtumiaji wa mtandao wa *Airtel*/na inapotokea bahati mbaya ninatuma fedha kwenda kwenye mtandao mathalani wa Vodacom, inapotokea



nimekosea usalama wa fedha unakuwa ni mdogo. Kwa hiyo, naomba nishauri Wizara iweze kuona namna gani basi sasa ianze kushauri kampuni hizi zijikite katika kuhakikisha kwamba wanaweka *coordination* ili ku-secure zile fedha za mtumiaji anayetuma mtandao mmoja kwenda mtandao wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze moja kwa moja kwenye Jimbo langu sasa la Msalala. Jimbo langu la Msalala lina kata 18 na lina vijiji 92 lakini katika Kata zaidi ya 12 hatuna mawasiliano. Kumekuwa na changamoto nyingi sana juu ya ukosefu wa mawasiliano katika Jimbo langu la Msalala na hasa katika Kata ya Jana, Mwaruguru, Mwanase, Kashishi, Lunguya, Ntobo, Shilela, Mega na kata nyingine nyingi. Matatizo haya yanasababisha sasa ndoa kuvunjika. Leo hii katika maeneo mbalimbali katika Jimbo langu la Msalala ukitaka kupiga simu mpaka utafuta mti au mbuyu mrefu ili uende ukapige simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya nimeshawasilisha kwa Waziri na nimemuomba Waziri kwamba aone namna gani anaweza kutusaidia sisi wa Jimbo la Msalala ili tuondokane na adha hii. Ndoa nyingi zinavunjika kwa sababu ya kisingizio cha mtu kwenda kwenye mlima fulani kupiga simu, unakuta ameshaandaa mchepuko hukohuko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosekanaji wa mawasiliano haya unahatarisha sasa ndoa za wananchi wangu wa Jimbo la Msalala. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, chondechonde, makao makuu ya wilaya hatuna mtandao. Wanapotaka kuchapisha *document* za halmashauri ni mpaka wasafiri waende Kahama Mjini, Mheshimiwa Waziri hebu tuangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hilo tu, tuna maeneo mengi ya machimbo katika Jimbo langu la Msalala. Kama mnavyofahamu suala zima la biashara ya madini na biashara nyingine linaenda kimtandao, lakini suala la *applications* mbalimbali linaenda kimtandao, ukosekanaji wa mawasiliano katika Jimbo langu la Msalala, hasa katika Kata

ya Segese, Kata ya Bulyanhulu, Kijiji cha Nyangalata, Kata ya Jana na maeneo mengine, unasababisha kuwanyima haki wananchi juu ya kufanya *application* ya kuomba leseni za madini na kibali cha mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu wananchi wetu ili kupata kibali cha kusafirisha mazao unatakiwa u-*apply* kwa mtandao na maeneo yale hayana mtandao. Mheshimiwa Waziri ukosefu wa mawasiliano katika Jimbo la Msalala unasababisha anguko kubwa la kiuchumi. Tunakuomba chondechonde katika kata hizi ambazo nimezitaja angalia namna gani basi unaweza kutupatia mawasiliano, ili wananchi wetu waweze kuondokana na adha hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo. Naunga mkono hoja, naomba Mheshimiwa Waziri chondechonde akina mama na akina baba wanalalamika ndoa zao ziko hatihati, tuangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Magessa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo la kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu tena kwa siku ya leo kuniona wa maana kwamba niweze kuchangia hii sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Mawasiliano, Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, lakini kuna shida kubwa sijui unakwama wapi kaka. Toka tufahamiane nimekuwa nikikueleza kilio changu cha mawasiliano katika Jimbo la Mbogwe. Jimbo la Mbogwe lina kata 17, vijiji 87, lakini kuna uhaba mkubwa wa mawasiliano. Ninazo kata 17 lakini kata 10 mawasiliano hakuna kabisa, kuna Nyasato, Buligonzi, Ushirika na Mbogwe Makao Makuu

pale ambapo halmashauri yangu ya wilaya ndio iinatokea pale lakini hakuna *network* hivyo, inafanya kazi za Serikali kuwa ngumu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ulimwengu wa sasa mawasiliano ndiyo mtaji wetu mkubwa, tunafanya mambo ya *posa* ikiwemo *transaction* za kibenki. Kwa maana hiyo sasa nakuomba Waziri uone aibu ufike Mbogwe ili kusudi uone namna gani vipi, usiangalie maneno tu ya humu Bungeni mnakula kiyoyozi halafu kazi hazifanyiki. Umekuwa mteja mkubwa wa mawasiliano mimi mara nakuona Kigamboni na wilaya zilizoendelea na sehemu nyingine, hebu utuone na sisi vijijini kule kwamba tuna umuhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Jimbo la Mbogwe lina migodi 11 midogo midogo ambapo siku moja Waziri wa Madini amesimama na kulihakikishia Taifa tumeingiza shilingi bilioni 528, lakini wananchi wanaochimba haya madini hawana mawasiliano. Kuna Mgodzi mzuri kabisa Nyakafuru na Kanegere, wachimbaji wakienda kwenye migodi ile hakuna mawasiliano. Kaka yangu nihurumie pamoja na Naibu Waziri wa Mawasiliano mdogo wangu Mheshimiwa Kundo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata ya Iponya na Lugunga pamoja na Ikungwigazi, Isebya, Ilorwanguru, Mpakali, Mponda na Nhomolwa, haya maeneo ninayoyazungumza Waziri ni maeneo yenye uzalishaji na kuna binadamu wenye akili timamu kushinda hata Wagogo walioko huku Dodoma pamoja na sehemu nyingine na Wazaramo kule. Kwa maana hiyo, nikuombe Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Mawasiliano msikae mjini tu hebu twendeni shamba huko maana mambo mazuri yanatoka shamba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nichangie kwenye upande wa mawasiliano kwenye vifurushi. Unapoweka kifurushi inakwambia ni mwezi mmoja, nikiangalia leseni mmetupa leseni za mwaka mzima ni kwa nini napotaka nijunge na mawasiliano kwenye *internet*

unaambiwa ni mwezi mmoja tu? Hilo nikuombe Waziri uje na majibu kamili, tofauti na hapo mimi jioni nitashikilia shilingi haipo sababu ya kupitisha bajeti yako mpaka utupe ufafanuzi ni kwa nini mtu anapokuwa na Sh.50,000/= kwa mfano, lakini unapoingiza kwenye kifurushi unaambiwa ni siku 30 tu wakati leseni ni ya mwaka mzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine Mheshimiwa Waziri kwenye sekta yako huku wizi unaongoza sana. Unaona namba tu unaambiwa tuma kwa namba hii, mimi fulani bin fulani tuwasiliane kupitia mawasiliano haya kumbe ni tapeli tu. Najua kuna sheria zetu za mawasiliano zinatungoza, sijui unaweza kuwa na majibu leo tuna miezi sita sasa unaelekea wa saba, umeshitaki matapeli wa namna hiyo wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zile ukienda Polisi kunakuwa na mizunguko mingi utafikiri hata askari wanajua labda tatizo linalofanyika kwenye wizi wa mawasiliano. Hivyo, kaka yangu kwa kuwa Mama Samia, Rais wetu amekuamini, hebu jaribu kuumiza kichwa hawa matapeli wanaotapeli wananchi na kama unavyojua wananchi wetu hawana uelewa sana, maana hivi vitu ni vipya zamani havikuwepo, kwa hiyo, anapoibiwa mwananchi mmoja hasara yake ni kubwa sana maana umeambiwa tuma kwa namba 07 by hiyo, sasa hivi tuma au unaweza ukapigiwa na mtu akakwambia mimi sijui nani-nani *Tigo Pesa* huku, tukutane sehemu fulani, lakini ukianza ufuatiliaji unakuta hata kwenye Jeshi la Polisi kituo kizima labda askari ni wawili wanaohusika na hicho kitongo, lakini mwisho wa siku na wenyewe...

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

## **T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hili ambalo analizungumza Mbunge wa Mbogwe

ni kweli kumekuwa na wizi mkubwa kupitia mitandao. Hata mimi hapa kwenye simu yangu nimepokea *message* ambayo inasema tuma fedha kwenye namba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Rais wakati anazungumza na Jeshi la Polisi ameigiza Wizara watuambie ni kwa nini kama tulifanya usajili wa *line* kwa kupitia *finger prints* lakini utapeli huu bado unaendelea. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali jioni hapa wakati inatoa majibu itujibu pia katika hili, naomba kutoa Taarifa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeipokea Taarifa?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa ya Mheshimiwa, naiunga mkono tuko na pamoja kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba niendeleo kwa kukushauri Waziri, tunapokushauri kwenye vyombo hapa sio kwamba labda tunakuchukua, tunakupenda sana, unajua mtu anayekueleza ukweli anakuthamini. Tunatamani sana uendeleo kuwa Waziri, lakini umiza kichwa, hiki kitengo chako ni kigumu, watu wanaibiwa, watu wanapoteza haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Jirushe, unaweza ukaweka 10,000/= ukapewa siku 30, dakika 20 pesa inakuwa imeshaisha wakati umeambiwa ni mwezi mmoja. Jaribuni sasa kuumiza vichwa pamoja na CAG na vyombo vingine muangalie tunaibiwa kupitia njia gani, ili kusudi utatuzi uweze kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, Mheshimiwa Waziri...

## TAARIFA

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa matapeli wanaoiba kwa mitandao hawaibi kwa mitandao peke yake mpaka na minara. Hii minara yote imeenda kuwekwa kwenye maeneo ya milima ya vijiji, unaambiwa mwenye leseni yuko Dar-es-Salaam anaitwa Gasper Gap; sasa unashangaa nani aliyempa leseni kwenye mlima wa kijiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii taarifa pia nampa Mheshimiwa Maganga ajue wanaiba mpaka kwenye minara. Tunaomba Waziri aje atuambie nani mwenye hiyo minara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Taarifa umeipokea?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa. Unajua mimi naogopa kufunguka sana maana Naibu Waziri pale na Waziri wananiangalia sana na wanafikiria kwamba labda kweli bajeti yao haitapita. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoomba niwashauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, hebu tumieni taaluma zenu pamoja na uwezo mliopewa na Mwenyezi Mungu muweze kulisaidia Taifa. Tofauti na hapo sekta hii ndio inaongoza kwa ujambazi na wizi, ina maana hatutasonga mbele. Wananchi wana matumaini makubwa sana na sisi, ili tuweze sasa kuutoa uchumi wetu kwenye kiwango cha kati, tukiacha kuibiwaibiwa huku kwenye minara au kwenye sekta ya mawasiliano lazima tutapiga hatua tu, lakini kama tunawapa shilingi 10,000 inaisha saa 24 hatuwezi kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi watu tumeshalemaa, mimi hapa sasa hivi nikiwa sina simu ninahisi kama niko kaburini. Ina maana simu ni kitu muhimu kuliko vitu vyote. Sasa unapokuwa na simu tena inakulia hela pasipo utaratibu unakuwa kama vile una wake zaidi ya 10 wakati

una simu moja kwa ajili ya kupata tu *connections*. Kwa maana hiyo, mimi Waziri nikuombe sana jitume, pambana, lakini Kanda ya Ziwa lina maeneo makubwa sana yenye milima na lina wananchi wengi sana; hebu ukija Mbogwe sasa mimi nitakutembeza na uone migodi jinsi ilivyo huko. Kuna migodi mingi Mwakitolyo, kwa Mheshimiwa Iddi Kassim kule Nyangalata, kuna Mwabomba, yale maeneo yote hayana mawasiliano. Kwa hiyo, hakuna haja ya kukaa Kigamboni Mheshimiwa ukumbuke uchaguzi mpaka 2025 na hata kama hauna mafuta sisi ni wauza mafuta mimi na mwenzangu Mheshimiwa Tabasam tutakuwa tunachanga kwenye magari yako ili uweze kufika kwa wananchi wenye shida. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tujaribu kuchukua tahadhari ya kutaja majina ya watu Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni ya 81 wana haki ya kuja kulalamika kwa Spika kuwatuhumu kwa vitu ambavyo hawana nafasi ya kujitetea humu. Kwa hiyo, nafikiri mnaweza mkajenga hoja kwa kusema tu kuna hiki na hiki, lakini kutaja jina la mtu *specifically* inaweza ikaleta *conflict* humu ndani.

Tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikupongeze sana kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo amenipatia kuweza kuchangia Wizara hii. Wizara hii ni nyeti na yenye mambo ya kisasa nafikiri kuliko Wizara zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye mambo machache sana, kwanza ni *tower sharing, co-location*. Nilitegemea kabisa kwa sababu tumeingia kwenye *tower sharing* au *co-location* hiyo basi hatuna haja ya kuwa na minara mingi nchini. Kwa mfano, Kiyegeya kuna minara nane,

tunategemea minara hii ipungue kwa sababu tunaweza ku-*co-locate* tukawa na minara miwili ikafanya kazi yote ya minara nane iliyopo na tukaokoa mazingira yetu badala ya kuwa na minara mingi ndani ya nchi ambayo haina kazi kubwa sana tuwe na minara michache na *co-location* iipunguze hiyo minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiipunguza minara hiyo basi tutoe hizo *structures* huko milimani zisendelee kuharibu mazingira tuliyonayo na hayo ma-*dishes* ambayo yanaonekana yatakuwa hayana kazi. Toka tumeanza kufanya *co-location* ni karibu miaka saba, nane, sina uhakika Wizara ina minara mingapi ambayo imei-*demolish* na sasa tunajua imepungua kiasi fulani na hali yetu ya mazingira kwenye milima yetu imekuwa bora, sina uhakika sana. Nishauri Serikali tupunguze idadi ya minara kwa sababu tunaweza kufanya *co-location* au *sharing*. *Sharing* itiliwe mkazi ili minara isiendelee kusambaa kila mahali a ku-*pollute* mazingira yetu, kila mtu anaonekana ana mnara wake na anataka kuwasiliana na wananchi walewale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo nataka nilichangie hapa ni mkongo huu, nimesikia unaongelewa sana. Ukienda kule wilayani baada ya teknolojia kuongezeka tunatumia mifumo kulipa, mifumo mingi ya Serikali sasa inatakiwa iwalipe wakandarasi na wananchi, mkongo unapokuwa una shida maana yake ni kwamba kwenye wilaya kule kila anayeenda kufanyiwa malipo anaambiwa leo mfumo hauko vizuri, lakini shida yetu ni huu Mkongo wa Taifa. Inaonekana kabisa *inter-connections* imeshafanyika mahali pakubwa sana, lakini kuna udhaifu mkubwa sana kwenye maeneo ya vijijini kwa sababu ya uhakika wa hiyo *bandwidth* ambayo inaenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maneno mazuri sana tumeyataja, lakini ukienda kwenye wilaya kabisa kule ndani ndani kule ambako ndiyo tunasema Mkongo wa Taifa umefika tumefanya hiyo *inter-connection* utagundua kuna wakati wanashindwa kufanya shughuli zao kwa sababu leo mtandao uko chini. Niiombe sana na niishauri Serikali ifanye



ukaguzi wa kutosha kwenye maeneo hayo ili wananchi waweze kuhudumiwa na teknolojia hii kwa urahisi zaidi badala ya kuingia kwenye tatizo ambalo inaonekana malipo hayawezi kufanyika na vitu vingine vinakuwa vimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudi sasa Busanda jimboni kwangu, tuna kata 22. Kila nikikimbia kilometa mbili-tatu mtandao unapotea, maana yake *coverage* yetu ya mtandao ni dhaifu, hiyo *radius* ya *coverage* itakuwa ni dhaifu. Niombe sana huu Mfuko wa Mawasiliano (*UCSAF*) ambapo kazi kubwa nimesoma hapa kwenye hotuba hii inaonesha ni kuimarisha na kuongeza mtandao wa mawasiliano kule vijijini, vijijini mawasiliano bado yana shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wenzangu wanasema wanaomba hata wachangie mafuta ili Mawaziri waweze kwenda, mimi sitachangia. Niombe tu mje muangalie uhalisia kwamba kuna zaidi ya kata 11 mawasiliano yake yana matatizo. Naamini kabisa mkifika huko tuna-*test* wote tutajua kabisa mahali fulani hakuna mawasiliano na mtaweza kutusaidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nishauri sasa mizunguko yenu ifike kwenye maeneo yetu ambayo tunawakilisha wananchi waweze kupata kupata mawasiliano, wakipata mawasiliano tutakuwa na uhakika wa mambo kdhaa ambayo sasa hivi hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa kijijini leo, kwa mfano niko Kata ya Nyakagomba ambako natoka mimi, kuna walimu wanataka kufanya *application* nikimwambia fanya *application* halafu unirushe hapa, hawezi kurusha. Kwa sababu akifanya *application* anagundua hakuna *3G* kuna *2G*, kama kuna *2G* maana yake kile anachofanya hakiwezi kuingia kwenye *data*. Kwa hiyo, tuna shida hiyo kwamba, iko minara ilikwenda vijijini kule, lakini iko kwenye *2G* hawajaingia kwenye *3G* na huku mbele kwenye *4G* na huku tunakokwenda kwenye *5G* sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana mpite kwenye maeneo ya vijijini. Namuona Ndugu yangu hapa Burongwa anagonga mkono, anajua kabisa Burongwa kule *2G* ndio iko

3G hakuna. Kwa hiyo, niombe sana tuteembeleeni huko tuliko ili matatizo haya ambayo tumeyata hapa tukayaseme na nyie mkiwa mnaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina kata 13 zinachimba dhahabu. Wanachimba dhahabu, pesa wanayo, hawawezi kuwasiliana vizuri. Nilifikiri ukiwa na pesa inabidi maisha yako yawe rahisi kidogo, unakuwa na pesa lakini na maisha yako yanaendelea kuwa magumu. Niombe sana tufanyiwe huduma hii kama ni *UCSAF*, kama ni hawa *vendors* wengine waweze kuja kwenye maeneo yetu kuhakikisha kwamba tunapata mawasiliano. Tukishayapata hii kasi ya maendeleo na mchango wa sekta hii ambayo najua unaendelea kukua haraka kwenye pato la Taifa, niwaombe sana tuweze kuweka mchakato wa kutosha kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaweza kupata mawasiliano na mwisho wa siku tutaona maendeleo yetu yanakwenda kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kwenye mawasiliano sasa hivi wanaweza kufanya *operation*, mtu akiwa *South Africa* anaweza kufanya *operation* Benjamin Mkapa akiwa kwenye mfumo huu. Sasa kama tutaonekana kwamba sisi mawasiliano yetu ni dhaifu maana yake akianza kufanya *operation* kuna mahali patakatika na huyu mgonjwa atafia kitandani huyu. Kwa hiyo, niombe sana tuwe na *stable communication*, lakini *coverage* yetu sasa iongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa naona muda uliobakia ni mdogo, *unless* kama Mheshimiwa Yahya Ally yuko tayari kuchangia kwa dakika sita.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari.

**MWENYEKITI:** Uko tayari, haya karibu.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote walio chini ya Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 05 Mei, 2021, niliuliza swali la mawasiliano ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu, Mheshimiwa Waziri alitoa majibu yenye uhakika kwamba tenda inatangazwa na maeneo yote yenye changamoto yatachukuliwa hatua zinazostahili. Ni matarajio yangu kabla hatujaondoka ndani ya Bunge hili nitapata taarifa sahihi tenda imetangazwa lini na nani anakuja katika jimbo langu kufanya kazi hii ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni changamoto ambayo tumeanza kuishuhudia ndani ya nchi yetu. Wiki mbili zilizopita *TRA* ilikumbana na changamoto ya mtandao wake wa malipo kutokufanya kazi, karibu siku tatu uchumi wa nchi hii uliyumba, watu hawakulipa na hakuna malipo ya aina yoyote yalifanyika *TRA*. Siku tatu zilizopita tumeshuhudia Kampuni yetu ya *TANESCO* imeshindwa kutoa huduma ya kununua LUKU. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni tahadhari, nawaomba sana Wizara, nawaomba sana wataalamu wetu wa *TSA* wawe waangalifu, dhahama inakuja. Kama hatutakuwa na *backup system* ya kukabiliana na utaratibu huu iko siku hapa tutakwama kabisa kufanya shughuli zetu. Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* atueleze ni mikakati gani inayofanywa na Wizara yake kukabiliana na hizi changamoto ambazo zimeanza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni minara. Kuna wajanja ambao wapo ndani ya nchi hii wanapata taarifa kwamba kuna Kijiji A kutawekwa mnara, Kijiji B na Kijiji C. Wanakuja kule wanunua maeneo ya wananchi wetu kwa kujua kwamba kesho unakuja kuwekwa mnara, hawa ni matapeli. Namuomba Mheshimiwa Waziri niko tayari kumsaidia wale wote waliokuja ndani ya jimbo langu wakanunua maeneo ya wakulima kumbe lengo lao ni

kuwekwa minara, minara ile walipwe wahusika. Huu ni wizi mkubwa, haiwezekani mtu atoke huko atokako aje kununua eneo ndani ya kijiji chetu kumbe kesho unawekwa mnara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake Serikali ya Vijiji imekosa mapato, wananchi wamekosa mapato na yule mtu kanunua lile eneo na haonekani yuko wapi. Jambo hili kwa kweli linaumiza sana.

## T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe Taarifa mzungumzaji, katika Wilaya yangu ya Liwale kuna Kijiji cha Kibutuka kuna tapeli mmoja ameenda kuchukua eneo la shule, mnara uko kwenye eneo la shule lakini unasoma mtu yuko Arusha.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo naipokea. Ndani ya Wilaya yangu kwenye Kata ya Sengenya, kwenye Kijiji cha Mkumbaru, kuna hao matapeli wamekuja na wamechukua hayo maeneo na wameweka minara. Kwenye Kata ya Mkonona, kwenye Vijiji vya Mangara Mbuyuni kuna watu wa aina hiyo. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ihakikishe kwamba jambo hili kwa kweli linakoma na hawa watu warudishe minara hiyo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Shirika letu la *TTCL*. Ni jambo la kushangaza sana inakuwaje Serikali inadaiwa na Shirika hili? Ndani ya bajeti tunapitisha hapa bajeti za Wizara, inakuwaje leo wanashindwa kuwalipa? Hhili jambo halikubaliki. *TTCL* pia mimi naomba niwalaumu inakuwaje unambembeleza mteja? Kama hakulipi si

umkatie? Mbona *private sector* wanafanya hivyo sisi tunashindwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kulialia hapa kumbe *powertunazo*, tukate. Vinginevyo kama utaratibu huu wa kubembelezana utaendelea mashirika yetu ya umma yatakufa. Tunapitisha bajeti tutalipa umeme, maji, simu, kwa nini wewe Mtendaji Mkuu wa Shirika hukulipa simu *TTCL*? Unapata huduma bure na unaendelea kuchekewa, hili jambo halikubaliki. Mimi naishauri Serikali, *TTCL* nendeni mkawakatie wale wote mnaowadai vinginevyo tutakuwa tunakwama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Shirika letu la Taifa (*TBC*) matangazo yake hayasikiki maeneo mengi ya nchi yetu. Jimbo letu la Nanyumbu *TBC* haisikiki kabisa. Mfuko huu wa Mawasiliano kwa nini hawawawezeshi *TBC* wakasikika nchini kwetu? Hili ni eneo ambalo wananchi wetu wanategemea kupata mawasiliano ya uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko mpakani na Msumbiji, tunatarajia mawasiliano ya uhakika yapatikane kutoka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja lakini namuomba Mheshimiwa Waziri jioni hapa hapataeleweka kama hakutakuwa na majibu sahihi. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana umekwisha, jioni tutaanza na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Nashon William atafuata kwa utaratibu nilioutangaza.

Baada ya maneno haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 07.03 Mchana Bunge Liisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

## HOJA ZA SERIKALI

### MAKADIRIO YA MAPATO A MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

*(Majadiliano yanendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mchana nilitangaza atakayeanza ni Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Nashon William ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi niungane na wenzangu kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake. Tunatambua Wizara hii amekabidhiwa muda mfupi, lakini anachanja mbuga kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Mbinga Vijijini amezungumza ndugu yangu Mheshimiwa Judith, sisi wa Mbinga Vijijini kama inavyoitwa vijijini tuna changamoto kidogo ya mawasiliano. Tuna kata 29 na miongoni mwa kata hizi, baadhi ya Kata hazina mawasiliano kabisa. Mheshimiwa Judith alijaribu kuzitaja, nami naomba nirudie kwa Kata ambazo hazina mawasiliano kabisa. Kata ya Ukata, Kata ya Kipololo, Kata ya Kitura, Kata ya Kiyangimauka, Kata ya Muhongozi na Kata ya Kitumbalomo. Kata hizi ili wananchi waweze kuwasiliana lazima wasogee kata jirani ndiyo wanaweza kuwasiliana, ama wategeshe simu maeneo fulani fulani; akitikisika kidogo tu, basi hana

mawasiliano tena. Sasa kwa karne hii tunawanyima fursa wananchi hawa, wanakosa fursa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye randama hapa Mheshimiwa Waziri ameonesha baadhi ya kata hizi zinaenda kupata mitandao na kwa bahati nzuri katika hii taarifa anaonesha kwanza baadhi ya Kata zilipata wakandarasi muda mrefu, lakini toka mwaka 2018 baadhi ya kata hizi hao wakandarasi bado hawajaenda kujenga minara. Namwomba Waziri akija kuhitimisha hapa atueleze sisi wananchi wa Mbinga, lini na sisi sasa tunaenda kupata mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizuri nimeona pia hapa kuna baadhi ya kata saba zimejengewa minara; na ile minara ni ya muda mrefu, lakini hadi leo haijawashwa. Kuna mnara upo Lunolo Kata ya Kipololo haujawashwa; kuna mnara upo Litoho Kata ya Ukata, haujawashwa; kuna mnara upo Kitura, Kata ya Kitura, haujawashwa; na pia kuna mnara upo Muhongozi, Kata ya Muhongozi, haujawashwa. Minara hii ikiwashwa angalau hizi kata nazo zitapata mawasiliano japo siyo kwa kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba wananchi wa Mbinga wako vizuri. Nami nashangaa haya makampuni ya kibiashara yana hofu na Wilaya ya Mbinga; sisi ni wakulima wa Kahawa, tunalima kweli kweli. Kama tuliweza kununua mashine za kusaga kila nyumba, hivi tutashindwa kununua *Airtime* hii! Nashangaa kweli kweli wanapofikiri uchumi wetu ni wa chini. Uchumi wetu ni mkubwa kweli kweli! Kwa hiyo, nawaomba na ni-*encourage* haya makampuni yasiwe na hofu na Wilaya ya Mbinga; wananchi wa Mbinga wapo vizuri kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kata moja ina uwezo wa kuingiza shilingi bilioni nane, sasa kuna shida gani hapo? Kwa kweli nawaomba sana watu wa mitandao kwa Wilaya ya Mbinga na hususan Mkoa wa Ruvuma kiujumla, kiuchumi tupo vizuri, kwa hiyo, msihofu kwamba mkipeleka mitandao kule hamtafanya biashara. Siyo sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi kule tupo mpakani. Kuwa na mtandao wa mawasiliano ni ulinzi kwa nchi. Sasa hivi tunapokea mawasiliano ya Malawi, ya Msumbiji, inakuwa haipendezi kidogo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa hilo; na anapokuja kuhitimisha hapa atueleze hizi kata ambazo hazina mawasiliano kabisa ni lini sasa na zenyewe zinaenda kuingia kwenye mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, yale maeneo ambayo kidogo yana mawasiliano, yanakosa mawasiliano ya *Internet*; hatuna kabisa mawasiliano ya *Internet*. Amezungumza mwenzangu hapa, ku-*download* kitu ni lazima ufike mjini, lakini sasa kipindi hiki kama manavyotambua mambo sasa hivi ni ya kimtandao tu; unataka kusoma, unasoma *online*; Serikali yenyewe inafanya kazi na kutoa maelekezo *online*; sasa mtu yupo kijijini kule, Afisa Mtendaji ametumiwa kitu na Mkurugenzi, hawezi ku-*download*. Ni lazima aende sehemu nyingine huko akatafute mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, kuna baadhi ya maeneo mliweka siku kadhaa, baadaye wakatoa. Sasa sijajua kwa nini watoe? Kwa kweli naomba sana sana nasi tupate nawasiliano haya ya *Internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, zile kata sita nilizozitaja ambazo zimeshafungiwa minara, pengine Waziri unapokuja kutoa hitimisho hapa utuambie kwa nini imechelewa? Cha msingi zaidi, ni lini sasa tunaenda kuwasha ile mitandao? Nakushukuru sana, ahsante sana kwa muda. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Hamida Mohamed, ajiandae Mheshimiwa Nashon William. Hamida Mohamed hayupo, Mheshimiwa Neema Lugangira halafu Mheshimiwa Ally Kassinge, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa



kutoa mwongozo na nia yake ya kuhakikisha miundombinu ya teknolojia ya mawasiliano inafika asilimia 80 ifikapo mwaka 2025. Haya ni maono makubwa ambayo yataupelekea kuimarisha uchumi wetu zaidi. Eneo la teknolojia ya mawasiliano ni sekta mpya ambayo ikiangaliwa kwa umakini, nchi hii inaweza kujipatia kipato kikubwa pamoja na kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo kwa ndugu zetu Wakenya, sekta ya teknolojia ya mawasiliano inachangia asilimia nane ya pato ghafi la Taifa; na tayari sekta hii kwa Kenya imeshatengeneza kakribani ajira 250,000; na hii ni kwa takwimu ya Serikali ya Kenya. Ukuaji wa sekta *ICT* Kenya umepita ukuaji wa sekta zote kwa zaidi ya asilimia 23 na hii ni kwa mlongo uliopita peke yake. Kwetu hapa Tanzania bado kuna changamoto ambazo tukiziangalia vizuri zitaisaidia kuongeza ajira katika sekta hii ambayo hivi sasa tumeifunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano mdogo, wachangiaji wengi asubuhi waliongelea kuhusu *YouTube*. Hivi sasa kwa Tanzania *YouTube* mazingira yake siyo Rafiki. Nasema hivi kwa sababu wako wanamuziki wachache ama wadau ambao wanatumia *YouTube* kama akina Dimond, Alikiba na Milard Ayo ambao wamenufaika; lakini baada ya kuleta sheria ambazo zimepelekea changamoto, wako pia watu wengi ambao wamejiiondoa kutumia mtandao huu ambao wengi wao ni vijana. Sasa hii inaleta changamoto kubwa kwa sababu vijana hawa wanatumia teknolojia hii na sekta hii kujipatia ajira ambazo ni changamoto. Kwa hiyo, sera zetu lazima ziweke mazingira ya kuwawezesha wao kujijiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hii, tofauti na nchi nyingine, hapa Tanzania vijana wengi ambao wapo kwenye sekta hii hawana elimu rasmi ya masuala ya kidijitali. Kwa hiyo, tunapowaongezea gharama za kulipa ni kufifisha jitihada zao binafsi ambazo wao wenyewe wamezichukua kama vijana kujitengeneza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba niishauri Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia masuala yafuatayo: jambo la kwanza, Wizara ione namna gani itaweza kupunguza gharama zinazolipwa na Watanzania hususan hawa vijana kwa sababu hivi sasa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, naiomba Wizara ifanye mapitio ya sheria ili kuona namna ya kuondoa baadhi ya makosa kutoka kuwa makosa ya jinai iwe makosa ya madai, kwa sababu na yenyewe inaleta changamoto kubwa sana kuhakikisha kwamba watu wananufaika na sekta hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, tuongeze ufikaji wa *internet* kama ambavyo wengine wamechangia, hususan kule vijijini, hata tukiweza kufikia 3G. Tumeona kwenye miji mikubwa hii *access* ya *internet* inasaidia sana kufanya biashara, hususan kwa vijana na wanawake. Ukiingia mtandao wa *Instagram*, wengi wananufaika sana, lakini fursa hizi hazitunufaishi wale ambao tunatoka hususan Mikoa ya pembezoni. Kwa hiyo, nadhani lazima jitihada zifanyike katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile bado gharama za kupata *internet* hapa nchini Tanzania ni kubwa ukilinganisha na majirani zetu. Nitatoa mfano mdogo. Nairobi gharama ya uzito kwa mwezi ni Dola za Kimarekani 5.5, tukienda Uganda ni Dola za Kimarekani 10; Uganda kwa maana ya Mji wa Kampala, lakini tukija Tanzania kwa maana ya Mji wa Dar es Salaam ni dola za Kimarekani 15.5.

Kwa hiyo, unaweza kuona ulinganishi. Kwa Nairobi ni 5.5 kwa Dar es Salaam 15.5. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu tufanye tena uanalizi wa gharama hizi, kwa sababu kwa ilivyo sasa hivi Watanzania wengi hawafaidiki na hawanufaiki na sekta hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kufanya hivyo, tutaipunguzia Serikali mzigo wa ajira kwa vijana, kwa sababu tutaweza kufungua vijana kujajiri kupitia Sekta hii. Katika hili

naomba niishukuru Kamati kwa sababu na wenyewe pia wamelisemea suala hili kwenye wasilisho lao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tano, naomba Serikali iangalie namna ya kushirikiana na wabunifu ili kuongeza faida ambayo inapatikana na sekta hii. Yaani Wizara msijifungie, kwa sababu wako vijana ambao ni wabunifu tuone ni namna gani tunaweza tukashirikiana nao. Katika eneo hili nichukue fursa hii nimpungeze sana Spika, Mheshimiwa Job Ndugai kwa sababu kwa jitihada zake awali alifungua milango akakutana na vijana ambao ni wabunifu hadi wakatengeneza App iliyokuwa inawezesha vijana pamoja na wananchi kuwa karibu na Wabunge wao. Kwa hiyo, huo ni mfano tosha kwamba hata Wizara ikishirikiana na hao wabunifu inaweza ikaleta tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza, nirudie tena kwamba tunaweza tukajifunza kwa wenzetu wa Kenya ambao wana Sera ya *Digital Economy Blueprint* ambayo hivi sasa sisi Tanzania hatuna. Yote ambayo yamechangiwa hapa, kama tutakuwa hatuna sera madhubuti ya *Digital Economy Blueprint*, mengi haya yatashindikana kwa sababu hii ni sekta ambayo inahitaji iwe na miongozo thabiti na iwe na njia zote ambazo zitahakikisha zinawalinda watumiaji na walaji wa hii sekta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuwasilisha, angalau pia atueleze: Je, ana mpango gani wa kuja na Sera ya *Digital Economy Blueprint*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa fursa hii, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniita mchangiaji wa tatu, nipo hapa William Nashon.

**MWENYEKITI:** Ulipoitwa hukuwepo.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo.

**MWENYEKITI:** Haukusimama lakini.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama, nilikuwepo.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana ambayo ni Wizara ya Mawasiliano.

Kwanza naomba nimpongeze ndugu yangu Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara hii ni Wizara nyeti sana, kwa sababu sasa hivi kwa kweli wananchi wameshaelimishwa na wanazo simu zao na njia nyingi ni kutumia simu. Ukitaka kulipia maji, ni lazima utumie simu, lakini pia ukitaka kulipia umeme lazima utumie simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna shida kwenye mtandao huu wa kulipia umeme. Nadhani mnaweza mkaona kabisa, yaani hakuna namna ya kulipia umeme, kuna shida sana. Kwa hiyo, bado Wizara ina kazi kweli ya kufanya hii shughuli ili iweze kuwa na ufanisi mkubwa kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Wilaya ya Uvinza ambayo kwa kweli ni Wilaya ambayo watu waliitikia sana katika utaratibu huu wa wananchi kuwa na simu, kwa sababu hakuna namna nyingine, maisha ni simu. Kwa hiyo, Wizara hii ni Wizara ambayo inawagusa watu. Kwangu ninazo kata 16, lakini zipo kata nne, zote zina matatizo ya mawasiliano. Yaani ukienda kule Mbunge unafanya ziara, hata kama ningekwenda na Waziri, yaani siku hiyo tunashinda hakuna mawasiliano kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni Kata ya Mtegowanoti, yaani haina mawasiliano kabisa na hakuna mnara hata mmoja; ya pili ni Kata ya Kandaga hasa katika Kijiji cha Kandaga chenyewe. Kwa kweli na Kijiji kile ndipo ninapotokea; mimi nikishaingia kijijini pale, hakuna mawasiliano mpaka kesho nitoke kule, niende eneo lingine ambalo lina mawasiliano. Ni aibu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwakweli jambo hili Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia hasa katika eneo langu hilo la Kandaga na vijiji hivi ambavyo nimevitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Herembe ina vijiji vitatu, lakini vyote havina mawasiliano; Kata ya Igalula ina vijiji saba lakini vijiji ambavyo vina mawasiliano ni viwili; ambavyo ni Lukoma pamoja na Igalula yenyewe, vilivyobaki vyote, havina mawasiliano. Sasa kwa kweli ukiangalia hili ni tatizo. Ukienda kule wananchi wanamlalamikia Mbunge kwamba ni vipi sisi tumetengwa? Mbona wengine wana mawasiliano, sisi inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani, kwa kuwa na sisi Serikali inao mtandao wa *TTCL*, kwa nini basi tusiweze kupata minara ya *TTCL* ili tuweze kuondokana na hilo tatizo? Kwa sababu makampuni mengine haya yanafanya kazi kibiashara zaidi, lakini mtandao wetu huu wa kampuni ya *TTCL*, pamoja na kwamba na yenyewe inafanya kazi kibiashara, lakini pia mtandao ni wa Serikali. Kwa maana hiyo, ina huduma pia. Wenzetu hawa hawana huduma; wakiweka eneo mtandao au huo mnara, wakiona hali siyo nzuri ya mapato, wanahamisha. Sasa wakiamisha wale wachache maana yake wanaobaki, hawana huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika Jimbo langu eneo la mawasiliano, tukimaliza bajeti yake yeye mwenyewe Waziri twende Pamoja. Haiwezekani tuwe marafiki, halafu mimi nyumba inaungua. Mheshimiwa Waziri nitafurahi sana tukienda wote huko ili uone. Simu zako utazima, kwa sababu hutakuwa na uwezo wa kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Kama Mheshimiwa atanifanyia hivyo, basi hata shilingi yake sitashika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ally Kisinge atakayefuata ajajandae Mheshimiwa Stephen Kiruswa.

**MHE. ALLY M. KISSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza rafiki yangu Dkt. Faustine Ndungulile kwa kuwa Mtanzania muasisi wa Wizara hii mpya ambapo Mheshimiwa Rais amemdamini, amemuamini na kwa changamoto ambazo Wabunge tunazielezea katika Bunge lako Tukufu, naamini kabisa rafiki yangu Mheshimiwa Ndugulile ataweza kuitendea haki Wizara hii. Atasaidiana na timu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii, tuna imani nanyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la kwanza la mchango, ni kuishauri Serikali Wizara hii ya Mawasiliano Teknolojia na Habari kupitia taasisi yake ya *TCRA*. Kimsingi *TCRA* ni *regulator*, lakini Watanzania tunahitaji kufahamu ina *regulate* nini, masuala yote ambayo *TCRA* inadhhibiti yafahamike. Kama ingelikuwa ni mpira tasnia ya kabumbu au kandanda maana yake ni kwamba *TCRA* ni *referee* na makampuni ya simu ndiyo timu wachezaji, sisi watumiaji ndiyo washangiliaji na washabiki. Tunataka tujue sisi washabiki nini *TCRA* ina *regulate*. Twende mbali zaidi ipendeze zaidi tufikie wakati kwamba sisi washangiliaji, watumiaji, tupate muda wa kupata *forum* ya kutoa maoni yetu kwa huyu *regulator* anayelitwa *TCRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili gharama za simu. Huko nyuma tulikuwa tunatumia gharama za simu kwa utaratibu wa ukinunua Sh.1000 au Sh.2000 maana yake ndivyo utakavyotumia, lakini kumekuwa na utaratibu sasa wa kununua bando au vifurushi, imekuwa kana kwamba ni lazima ununue vifurushi, hivi utaratibu huu *TCRA* na Mheshimiwa Waziri wanasemaje, kwamba ni lazima Watanzania tulazimishwe kutumia simu kwa utaratibu wa vifurushi, usipohitaji vifurushi unataka utumie moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado kuna matatizo na tunahisi kwamba sisi wadau wa tasnia hii ya mawasiliano kuna kuibiwa kupitia utaratibu wa vifurushi. Kwa mfano, unakuta unajunga kifurushi cha wiki au kifurushi cha siku cha saa 24, badala ya kutumia akiba yako kadiri ulivyoweka, muda ukifika wa saa 24 imekata, sasa hii iliyokatwa inakwenda wapi, hapa ndiyo ambapo tunamtaka *regulator*, TCRA asikilize maoni ya sisi wadau ambao ni watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ushauri kwa Wizara hii, nianze sasa kuelezea changamoto ambazo zipo katika Jimbo langu la Kilwa Kusini lakini pia Jimbo la mwenzangu, jirani yangu ndugu yangu, Mheshimiwa Ndulane la Kilwa Kaskazini. Katika Wilaya ya Kilwa, wilaya yenye kata 23, kata 22 hazina uhakika wa mawasiliano. Nitumie fursa hii kumkumbusha rafiki yangu Mheshimiwa Dkt Ndungulile, nimefika ofisini kwake mara kadhaa kumkumbusha kwamba Likawage ambayo ni kilometa zaidi ya 110 kutoka Makao Makuu ya Wilaya hawana mawasiliano, kitu ambacho ni tishio kwa usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukumbuke kwamba Kata hii ya Likawage na Vijiji vyake vyote vitatu vya Likawage na Inoke na Liwiti, ni kata ambayo ipo katika eneo kubwa linazungukwa na Mbuga ya Selous. Wanapata shida ya kwenda kupiga simu mbali karibu na mpakani ukielekea Njinjo kule na usalama wa maisha yao unakuwa hatarini, tunapata shida kupata taarifa za dharura ikiwemo misiba, lakini shida kubwa ni suala la mtandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alinipokea vizuri ofisini kwake na kupitia sasa katika mjadala wa bajeti yake, nimkumbushe ahadi yake ya kuhakikisha kwamba Wanalikawage wanapata mnara wana uhakika wa mawasiliano. Sambamba na hilo bado zipo kata zingine ambazo mawasiliano ni shida katika Wilaya ya Kilwa ikiwemo Kata ya Nanjilinji hususan Nakiu pamoja na Kigombo, lakini pia ikiwemo Kata ya Lihimalyao hususan Kisongo na maeneo ya Mabanda kule. Pia Kata ya Kandawale, Kipatimu,

Miguruwe, Mitole, Kibata, Kinjumbi, Namayuni pamoja na Chumo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile awatendee haki Watanzania wa Wilaya ya Kilwa kuhakikisha kwamba wanapata mawasiliano ya uhakika. Mbaya zaidi hata zile sehemu ambazo mawasiliano yanapatikana, uhakika wa 4G haupo. Kwa hiyo tunaomba kwamba minara hii sasa iongezewe nguvu ili watanzania wa Kilwa nao waishi kidigitali kama maeneo mengine ya mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani ya Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii mpya ambayo kazi wanayoifanya ni muhimu na ni kazi nyeti sana katika kuweka Taifa letu kwenye *chart* ya hiki kitu kinachoitwa mawasiliano ya kisasa *ICT*. Kwa sababu mawasiliano ndiyo nyenzo muhimu ya kufanyia biashara ya kipesa, ya kielimu, sasa hivi kuna haja kubwa sana ya kudhibiti masuala ya mawasiliano katika maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatolea mfano Jimbo langu la Longido ambalo lina takriban kilomita 350 za mpaka ambao tunashiriki na nchi ya Jirani ya Kenya kuanzia Rombo mpaka kule tunapopakana na wilaya ya Ngorongoro karibu na Ziwa *Natron*. Katika ukanda huo wananchi wake wanategemea kwa asilimia zaidi ya 90 mitandao ya nchi Jirani kupata mawasiliano. Hili siyo jambo jema kwa sababu hata wanapotaka kutoa taarifa kwa viongozi wao kama sisi tukiwa Bungeni inabidi afanye *roaming* atumie *safaricom* ndiyo aweze kupiga simu hapa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mtovu wa shukrani kwa sababu katika kipindi kifupi ambacho Wizara hii imeundwa, kulikuwa na kata kama mbili ambazo hazikuwa kabisa na namna ya kupata mawasiliano ya Lang' atadapash na Nondoto, lakini mnara wa *Vodacom* umeshaanza kufanya kazi unasubiri tu kuzinduliwa rasmi na hivyo sasa hivi katika katika kata hizo mbili wananchi wamefarijika japo zile kata ni kubwa, kwa hiyo mnara mmoja hautoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona katika ukurasa wa 47, kiambatisho Na.3 kwamba Waziri ametaja kwenye hotuba yake kata ambazo zimeshapata huduma ya mawasiliano kufikia mwezi Aprili na kweli akatamka hiyo la Elang'ata Dapash na Noondoto ambayo *Vodacom* wameshatoa huduma lakini pia ametamka ya Engarenaibor akimaanisha mnara wa *TTCL* ulioko katika Kijiji cha Ngoswak kwamba umewashwa. Nipende kutoa taarifa kupitia Bunge hili kwamba huo mnara haujawashwa na wananchi wanasubiri kwa hamu sana mnara wa *TTCL* wa Kijiji cha Ngoswak ambao ulitegemewa kutoa huduma katika Vijiji vya Mairowa, Sinonik mpaka Kimwati utakapowashwa utakua umeondoa kero na kupunguza huo utegemezi wa minara ya nchi ya Jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Gelai Lumbwa pia hotuba ya Waziri inaonyesha kwamba mnara wa *airtel* unahudumia Kijiji cha Lumbwa na Alaililai ni kweli, lakini kuna kijiji kingine kinaitwa Ilchangitsapukin ambacho kinaenda mpaka Kenya na wao pia bado hawana kabisa mawasiliano katika Kata ya Gelai Lumbwa. Hivyo hivyo katika Kata ya Gelai Meirugoi kuna mnara wa *TTCL* ambao Waziri alionyesha kama unawasha mpaka Magadini lakini kweli Magadini hawana mtandao kabisa na ukitaka wapate mawasiliano bora uweke Ngaresero upande wa Ngorongoro mnara mkubwa ambao utasaidia upande wa Ngorongoro na upande wa Magadini kwa ukanda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kiambatisho Na.4 ukurasa wa 69, hotuba ya Waziri inatamka maeneo ambayo yanakwenda sasa kuwekewa minara ya mawasiliano.

Kwenye Kata ya Engaranaibo, Kijiji cha Mairowa, Ngoswak na Sinonik *TTCL* watakwenda kuweka minara, tunaomba hiyo minara ipewe kipaumbele kwa sababu hiyo ni kata inayopakana na mpaka wa nchi jirani moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Engikaret kuna Kijiji cha Kiserian hiki kijiji kwa kweli ni kama kisiwa kwa barabara ni ngumu kufika, mitandao hakuna na umeme haujafika. Naomba pia hilo lipewe kipaumbele kwa sababu Waziri ameorodhesha lakini kuna maeneo zaidi ya 14 katika mpaka mzima ambayo bado hayana minara ya mawasiliano. Baadhi nimeshayasema Kijiji cha Magadini, Wosiwosi, Matala B, Matala A, Kitongoji cha Irgong'wen, Kimwati, Sinonik, Eworendeke, Kimokouwa, Leremeta, Elerai, Kitenden, Irkaswa na maeneo Lerang'wa hivi ni vijiji vyote vilivyoshikamana na mpaka na hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kutoa angalizo kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo wameshapata minara kama Matala A, lakini mnara ule unawaka mchana tu, ikifika jioni maana unategemea *solar*, hivyo mawasiliano hukatika. Naomba sana kwa kampuni yoyote itakayoweka mnara, waweke *backup generator* pale ambapo umeme haujafika. Hali hiyo inajitokeza katika Kijiji cha Kamwanga inayopakana na Rombo na Kijiji cha Matala A, lakini mbaya Zaidi minara huko ni ya *2G*.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji anayeongea Mheshimiwa Kiruswa kwamba nadhani umefika wakati sasa Wizara hii kuangalia kwamba hatuwezi kuwa na minara sijui 300 nchi nzima, tufike wakati tuongee na makampuni kama kuna mnara mmoja kwenye eneo moja kama ni mnara wa *airtel*, basi makampuni yote ya-*share* kwenye mnara huo ili kuweka mtandao wa pamoja. Haiwezekani tukajenga

minara mingi katika nchi nzima kwa sababu minara na yenyewe ni magonjwa kutokana na mionzi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiruswa taarifa umeikubali?

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa yake na sina ubishi kabisa kwamba ikiwezekana basi ikafanyika *collaboration* kati ya makampuni, minara ipunguzwe, lakini mawasiliano yawafikie wananchi wote ambao wanahitaji huduma ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ni eneo la redio; vijiji hivi vya mpakani pia vina uhaba mkubwa wa kupata usikivu wa redio na *television* za nchini kwetu. Nishukuru Wizara kwa sababu wamejaribu kuweka *booster* za kuleta Redio Tanzania mpaka mpakani kule Namanga na Longido, lakini bado usikivu ni hafifu mno.

Kwa hiyo, naomba katika mipango ya Mheshimiwa Waziri atambue tu kwamba bado usikivu wa TBC maeneo ya Namanga, Longido na vijiji vya pembezoni ni sawa na hakuna, kwa hiyo wafanye kitu ili tuweze kupata mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sababu nimeshasemea hili la *2G* kwamba ndiyo liko katika minara mingi na ningeoomba sana iongezwe na wengine wengi wameshalisemea. Kuna hili suala la hii *channel* ya utalii inaitwa *Safari Channel*. Naona hii *channel* ina maudhui mazuri sana ya kuhamasisha biashara ya utalii kama ingeweza kununua hata *segment* ya dakika chake katika *TV* kubwa kubwa duniani, wakarusha zile *clips*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hii linaenda kugusa Wizara ya Utalii, lakini pia inaweza ikasaidia sekta hii ambayo inatakiwa isaidie katika kukuza utalii wa nchi yetu kwa kutafuta nafasi *CNN*, *BBC* na *channel* nyingine kubwa kubwa za Kimataifa kama hizo ili tuweze kutangaza utalii wa nchi yetu na kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kihenzile jiandae, Mheshimiwa Husna Juma. Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Jiandae Mheshimiwa Husna Juma na Mheshimiwa Hamisi Mwinjuma.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa fursa hii ambayo umenipatia. Nitaongea kwa kifupi na mambo machache; ukiacha kupongeza kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii mpya pamoja na wataalam, lakini niongee kwenye *angle* mbili tu. *Angle* ya kwanza, mara kadhaa nimezungumza na Mheshimiwa Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Mfuko wa Mawasiliano juu ya changamoto kubwa sana ya mawasiliano kwenye eneo letu la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani waliwahi kuniahidi kwamba wangeleta hiyo minara, niwaombe tu sasa wafanye utekelezaji. Tunayo changamoto kubwa sana kwenye Kata ya Idete ambako wananchi wanabidi wapande kwenye miti ndiyo afanye mawasiliano. Kwa mfano, ukiende pale Idete, utakuta kuna sehemu maalum kama *center*, zimewekwa Kamba pale kuna mtu anakodisha unapeleka simu yako pale halafu unaweka ukimaliza kuzungumza unarudi nyumbani. Hii si sawa kwa nchi ya *level* ya maendeleo ambayo tumefikia mpaka sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe wenzetu, walishaanza kufanyia kazi tayari pale lakini ziko kata jirani ambazo zina changamoto kubwa *especially* Kata ya Maduma, Idunda, Makungu, Kiyowela pamoja na maeneo

mengine machache ambayo yameainishwa. Kwa hiyo niwaombe sana Mheshimiwa Waziri na timu yake watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka pia kutazama eneo moja. Tuna mfumo mzuri ambao tumeuanzisha sasa hivi *especially* kwa kuanzisha masomo ya *computer* mashuleni. Hata hivyo, naishauri Wizara wakae chini, watafakari ni namna gani tunaweza kuwafanya vijana wetu wakawa *competent*.

Mambo mawili; moja masomo yale wanayosoma yawe na uhalisia, yawe ya kivitendo zaidi. Wapo vijana wanamaliza mpaka Vyuo Vikuu lakini pengine hata kutengeneza simu hawezi wa masomo ya *IT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa sana. Hivyo, niwaombe waitazame vizuri mitaala yetu, ni namna gani vijana wanaosoma pengine wako Vyuo Vikuu kama ni ma-*IT* kama ni ma-*engineer* wapo kwenye mifumo ya habari, namna gani sasa wakimaliza wanaweza kuja kusaidia huku mtaani ambako kuna changamoto kubwa sana kwenye eneo hili. Kila kitu tunasema sasa hivi kinakwenda kiteknolojia na vijana wako mtaani hawana kazi, kwa hiyo ni changamoto kubwa sana.

Namba mbili, tutazame namna ya kutengeneza *centers* kama *hubs*, baadhi ya nchi zilizoendelea waliandaa *technological hubs* kama zamani tulivyokuwa tunafanya maktaba. Unakwenda pale Dodoma Mjini kuna maktaba, vijana wanakwenda pale wanasoma, wanajifunza na kadhalika. Tunaweza kufanya hivyo hivyo kwa maeneo yetu kwenye *level* ya halmashauri, vijana walio mashuleni na wasio mashuleni wenye uelewa na uelewa mdogo, wakawa wanakutana inasaidia ku-*exchange* yale mawazo na ku-*develop* pengine mifumo mbalimbali ya ki-*computer*, matokeo yake tukaongeza *confidence* kubwa kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka tu niongee mambo hayo mafupi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Husna Juma jandae Mheshimiwa Hamis Mwinjuma.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mawasiliano ambayo ni moja ya Wizara muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Napenda kupitia kwenye mambo mawili, lakini kabla sijapitia huko naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya katika Wizara hii mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo napenda kulizungumza limezungumzwa na Wabunge wengi ni kuhusiana na mawasiliano kwenye baadhi ya vijiji. *Actually*, inasikitisha na inashangaza sana kwa nchi ya Tanzania nchi ambayo sasa tunajinasibu kwamba tuko kwenye uchumi wa kati lakini tunashindwa kukusanya mapato haya yaliyo wazi kabisa kutoka kwenye simu, kwa kutokupeleka mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata nyingi zinakosa mawasiliano lakini pamoja na kukosekana kwa hayo mawasiliano tunayo kampuni yetu ya Serikali ya simu ya *TTCL* ambayo ingeweza kuchukua hiyo fursa, hiyo changamoto ikageuza kuwa fursa na kwenda kuwekeza kwenye hayo maeneo kwa maana ya kujenga minara na kuweka mawasiliano ya simu na *internet* kwa ajili ya kurahisisha huduma kwa wananchi, lakini vilevile kupata soko na kuimarisha uchumi wa Shirika hilo. Hata hivyo, hilo halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii sasa kuishauri Serikali na Shirika letu la *TTCL*, kuamua kwa dhati kabisa kwenda kuwekeza huduma hii ya mawasiliano katika yale maeneo ambayo mitandao mingine haijafika. Nina mfano wa baadhi ya maeneo kule Lushoto Jimbo la Mlalo kuna maeneo ya Bustani kule Rangwi na kuna maeneo ya Umba kule Mlalo, kuna shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia kwenye maeneo ya Muheza kuna Kata inaitwa Kwemigondo ni *around* kilometa 30 tu kutoka Makao Makuu ya Wilaya pale Muheza, lakini uwezi kuamini kwamba ukaribu wa kiasi hicho kutoka kwenye Makao Makuu ya kwenda kwenye hiko kijiji ama hizo kata hakuna mawasiliano ya simu kabisa siyo makampuni mengine wala siyo kampuni yetu ya *TTCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kidogo inaleta shida ni vizuri wenzetu wakaona sasa umuhimu wa kwenda kuwekeza huko siyo tu kwa ajili ya kukusanya mapato kwa sababu wakitumia simu wanalipia siyo tu kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano. Lakini vile vile, kwa ajili ya kuwasaidia hawa watu kuwaweka salama kwa maana watakuwa wanapata nafasi nzuri ya kutoa taarifa ya kiusalama pale ambapo panakuwa na changamoto kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo nilitamani kulisema ni kuhusiana na uwekezaji ambao kwenye kampuni ya *TTCL*. Kampuni kwa kipindi kirefu sasa tangu uhuru, tangu tupate uhuru kampuni hii imekuwa ikifanya kazi kwa mazoea kiasi cha kutokuwa na mabadiliko makubwa ukiendana na uwekezaji mwingine unaofanywa kwenye makampuni ya binafsi. Sasa nishauri Serikali kuwekeza kwa maana ya kufanya pia mapinduzi kwenye utumishi wa kampuni ya hii kwa maana ya kuajiri vijana ambao wanahari na uwezo wa kuwajibika na ambao wako tayari kuwa na mawazo mapya ya kimtandao kama ambavyo yanaonekana sasa kuliko kuendelea kuwekeza fedha nyingi kwenye kampuni hii tunaipa mishahara mingi, lakini hakuna mabadiliko eneo linaloleta tija katika kampuni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilipenda kulizungumzia kuhusiana na gharama za mawasiliano. Hapo kati pametokea sana sinto fahamu ya kupanda na kushuka kwa gharama za mawasiliano hasa kwa maana ya muda wa mazungumzo na bando, lakini bado hatujawa na utaratibu ambao kweli una *tu-guide* namna gani ambavyo tunaweza tukatumia hizi bando hizi dakika kwenye

mitandao mingine ambayo wanafanya biashara, mitandao mingine unakuta wana bei tofauti na mitandao mingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mtanzania mlaji tuko kwenye soko huria, lakini je kama nchi tunapaswa kununua vifurushi hivi angalau isizidi kiasi gani na isipungue kiasi gani? Ni jambo muhimu sana wananchi wetu wakalifahamu hilo ili waweze kupata huduma hiyo wakiwa wanafahamu kiunagaubaga namna gani inatakiwa kugharamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba nikushukuru kwa fursa hii naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunawageni muhimu sana wameingia Bungeni mchana huu na kutokana na dharura wanataka kuondoka mapema na wageni hawa ni wa Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba ambao ni tawi la Yanga Group Tanzania, iliyopo Ilala Dar es Salaam nimewapa kipaumbele kwa sasabu ni wapiga kura wangu wako Ilala wakiongozwa na Mwenyekiti wao Akida Sungura, tunawatakia kila kheri kurudi nyumbani salama wasalimie. (Makofi)

Sasa Mheshimiwa bi. Hamida Mohamed hayupo, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, jiandae, Mheshimiwa Casato David Chumi.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kifupi kabisa mambo machache kwenye hotuba hii ambayo imewasilishwa. Naomba nianzie suala la makampuni ya kimataifa ambayo yanafanya kazi katika nchi yetu. Yapo makampuni mengi yanafanya kazi na makampuni au biashara ndogo ndogo, zipo kampuni za *tax* kama *Uber*, *Taxify* na pamoja na nyingine za namna hiyo. Zipo kampuni za *booking* kwenye mahotel mbalimbali zipo *hoteli.com*, *booking.com* na nyingine za namna hiyo. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri atakua anaenda kuhitimisha atufahamishe ni namna gani wanaweza kupata kodi kupitia makampuni haya haswa yale ambayo hayana ofisi *locally* ambayo yanafanya biashara na yanakusanya fedha nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepia pia niguusie kwenye suala la wizi, watu wengi wamegusia suala la wizi ninaomba niliguusie kwa sehemu mbili, kuna wizi kwa maana wizi wa *software* na wizi kwa maana *hard ware*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi mtu akiibiwa simu ambayo imeshasajiliwa na *IMEI* yake hipo kuweza kufuatilia inaonekana ni jambo kubwa sana, wakati teknolojia imeshakwenda mbali sana, simu hizo zinaweza kuzimwa na zisiweze kutumika na kwa bahati mbaya sijaelewa shida inakuwa wapi kwa sababu inabidi uende kwa *subscriber* wako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani wizara inaweza kuweka utaratibu kukawa kuna *call center* moja ambyo ukiibiwa simu *regardless* na mitandao wako ukipeleka taarifa zako pale wanaweza ku-*share* kwa mitandao yote na wakai-*block* hiyo simu. Lakini hiyo ya *ku-block* ni hatua ya mbele zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nadhani njia rahisi ya kukomesha kwa haraka ni kwamba ikishaibiwa simu ikisetiwa *call center* ya namna hiyo basi hizi *IMEI number* ikiweza kuwa *shared* kwenye hiyo mitandao basi waweze ku-*trace line* nyingine itakayowekwa hata kama ni ya mtandao mwingine anayetumia akamatwe vitendo vya namna hiyo vikiendelea vinakomesha wizi wa simu na baadaye *laptop* pamoja na vyombo vingine hivi vinavyotumia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili niwashauri Serikali kama wanaona ni gharama *ku-run* kitu cha namna hiyo, mimi nadhani kuna vijana wa kitanzania wengi baadhi

ni watu nawafahamu wanaweza kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Serikali na wengine walishapeleka mpaka maombi wakaambiwa ni mpaka tubadili *policy*. Sasa unaibiwa simu unaenda kutoa taarifa polisi inabidi kusubiri siku tatu nne na hapo ikishafikia hivyo uwezi kuokoa kitu chochote haswa *information* zinazokuwa kwenye vyombo vile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningepomba hili lifanyiwe kazi tunacho chuo cha *Cyber Crime* pale CCP kimeanzishwa, ninadhani ni muda sasa kama wataona ni gharama kufanya hivyo tunaweza kupitisha sheria kwamba mtu anaibiwa kifaa cha umeme hicho, kama simu *computer* au *tablet* aweze kupewa huduma ndani ya masaa 24, ndani ya masaa 24 maana yake mtu anaweza *aka-trace* watu walioiba na kupata kifaa chake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende upande wa *software* na huu nadhani kidogo watu wengi wamegusia na Mheshimiwa Rais alipokuwa anaongea naye aligusia, kwamba inawezekanaje mpaka sasa tunasajili mpaka line zetu kwa kutumia *fingerprint* lakini wale wezi wa kwenye mtandao bado wapo na bahati mbaya fedha hizi zinamlolongo au zina cheni kama ukimtumia hawezi kuzitumia bila kwenda kwenye wakala na kuzitoa au kulipia huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inaonekana bado wizi huu unashamiri na watu tunao na teknolojia, walizima zile simu za kichina ndani ya siku kadhaa tu wakaweza kuzizima, lakini kwa sasa hivi hawa watu wanaiba kwa mtandao kila siku wanaweza kuwasha laini hatujui wanasajilije bila kuwa na *fingerprint* na hatujui kwanini hawawezi kukamatwa mpaka viongozi wa nchi atoe rai kwenye jambo dogo kama hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri wizara wajipange kwa ajili ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Casato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mheshimiwa Anatropia, ajiandae Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. CASATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi na ninapenda kuchukuwa nafasi hii, kwanza kuwa shukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake, lakini pia shukrani za pekee kwa Mamlaka ya Mawasiliano kwa maana ya *TCRA* ambapo miaka miwili iliyopita walitusaidia watu wa Mafinga katika Shule ya Msingi Mchanganyiko ya Makalala hii ni shule ya watoto wenye mahitaji maalumu siku hizi tunaita watoto wenye uono hafifu zamani tulikuwa naita watoto vipofu, wale wanamahitaji maalumu kwa maana vifaa wanavyotumia katika kujifundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *TCRA* walitusaidia lakini pia walitusaidia pale shule ya Sekondari Luganga kuwapa vifaa ili kuwawezesha wanafunzi kupata masomo katika namna ambayo kidogo inawepesi kwa hiyo, napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano huo na kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na shukrani hizo ninayo maombi machache na mchango mdogo kwa wizara na kwa Serikali kwa ujumla. Asubuhi nilikuwa nina swali kwa Wizara ya Nishati kuhusu masuala ya umeme na sehemu ya majibu ya Mheshimiwa Waziri akijibu swali lake, alikiri kwamba Mji wa Mafinga unakuwa kwa kasi na kunaviwanda vikubwa 80, maana yake ni kwamba huu ni mji wenye mchango mkubwa sana katika uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili Mafinga na Wilaya ya Mufindi kwa ujumla kama alivyosema pacha wangu David Kihenzile iendelee kuwa na mchango mkubwa na kama alivyosema Waheshimiwa wengine katika michango yao masuala haya ya matumizi ya simu yanaumuhimu wake. Kwa hiyo, niombe Serikali kuna maeneo kwa mfano; Kijiji cha Mtula, Itimbo, Buliainga, Kisada, Ulole, na Maduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi viko umbali wa kama kilometa zisizozidi tano kutoka katikati wa mji wa Mafinga, lakini mawasiliano yake hayana huhakika. Sasa kama nilivyosema kama ni huu mji wenye viwanja vikubwa 80 maana yake kwanza kwa kukosa mawasiliano inachelewesha mchango wa hawa watu katika ukuwaji wa uchumi wa Taifa na wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namba mbili pia inacheleweza mapato ya Serikali kwa sababu wangukuwa na mawasiliano inamaana kwamba wangetumia simu wangenunua data, wangenunua muda wa maongezi lakini pia wangepanya miamala ya fedha kwa hiyo katika mzunguko mzima ule Serikali ingepata kitu ambacho inastahili kupitia kodi na tozo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwa Serikali kwenye yale maeneo ambayo yanashughuli kubwa za kiuchumi ni kweli hii ni huduma lakini pia ni biashara. Sasa unapowekeza lazima pia kama ni huduma maana yake kila mmoja itabidi imfikie ile huduma, lakini ukilingalia kwa jicho la kibiashara elekeza nguvu maeneo ambapo itakupa faida kwa haraka ili uweze kuwapelekea huduma wale ambao kwao mzunguko ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwangu na hususani na watu wa Mafinga na Mufundi kwa ujumla kutokana na uchumi wetu kutokana na mazao ya misitu na bidii namna watu wanavyofanya kazi, naishauri Serikali sana itupie jicho kule wanaweza wakawekeza kule shilingi milioni 10 ikakupatia wewe milioni 100 ambayo ikaweza kupeleka huduma maeneo mengine. Kwa hiyo, nashauri namna hii ya kupeleka hizi huduma uziangalie pia katika jicho la kibiashara, kwamba unaweza ukanicheleweshea A ukamuwahishia B ili kusudi kesho uweze kumhudumia C na D na F kwa hiyo naomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma sana ripoti ya mara kadhaa *PWC* inaitwa *Entertainment and Media Outlook 2018/2022 yaani African Perspective* hawa mabwana

wameelezea kwa matumizi ya *internet* kama Wabunge wengine walivyosema siyo tu katika suala nzima *Media and Entertainment Industry*,

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika mchango wake wa uchumi katika mataifa mbalimbali kwa mfano; mchana watu wengi wamesema sisi hapa Tanzania kweli tunanufaika na matumizi ya *data* na uwelewa umekuwa mkubwa tumeona juzi *TCRA* wametupa *workshop* na imetusaidia sana kupanua wigo wa mawasiliano na ufahamu wa suala nzima la *internet* katika maisha yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe wito kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yako kwa ujumla na vyombo vyake Mfuko wa Mawasiliano na *TCRA* najua inawezekana huwa *mna-platform*, lakini niombe muwe na *platform* za watu ambao ni wasanii tuseme watu wa *entertainment* ili waweze kuwaambia ni changamoto gani ambazo wanakutana nazo inapokuja suala nzima la suala la matumizi mawasiliano katika ujumla wake. Kwa sababu tunaweza tukadhani kwamba tume *exhaust* hii *potential* lakini kumbe bado kwa sababu sisi pengine tumejifungia tuko na makaratasi na na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, semina ya juzi ya *TCRA* sisi wengine imetufungua sana kwa mfano mimi nilikua najua kwamba gharama za simu katika Tanzania ni kubwa sana, lakini kutokana na Takwimu ambazo tumepewa kwenye ile semina nimebaina kwamba kumbe sisi katika Afrika Mashariki na katika *SADC* sisi ndiyo the *cheapest*. Sasa unaweza ukawa unatengeneza manunguniko na lawama kutoka kwa wananchi au kwa wadau kumbe *simple because* hawako *informed*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, kutana na jamii ya *Media and Entertainment Industry*, fahamu changamoto wanazokutana nazo, fahamu na wenyewe fursa gani wameziona katika jicho la *Media and Entertainment Industry*, bila shaka kwa pamoja mnaweza kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini usiishie hapo tu ningeomba katika hiyo *platform* kadri itakavyo kupendeza washirikishe pia na watu wa izara ya habari na utamaduni kwa sababu wao pia wanawasimamia wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano leo hii mtu akitengeneza filamu yake inatakiwa ikaguliwe na bodi ya filamu, lakini hiyo bodi ya filamu ofisi yao ipo Dar es Salaam tu. Hili jambo nimelisema sana TCRA nadhani wapo *level* ya kanda, NEMC wapo *level* ya kanda, lakini kwanini bodi ya filamu, BASATA na COSOTA wao wakae tu pale Dar es Salaam na siku moja nilisema hapa. Msanii ametoka Mafiga Bumilahinga au ametoka Tandahimba au ametoka Kigoma, kwanza ameingia gharama au Shinyanga kwa dada yangu Lucy, ameingia gharama za kusafiri, anaingia gharama za malazi anafika katika zile ofisi anaambiwa bwana *printer* imearibika. Sasa katika dhama hizi unamwingizia huyu mtu gharama za kile kitu anachokifanya, lakini wakati mwingine unakuwa *ume-discourage*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana kuna *portion* kubwa sana katika suala nzima la *Media and Entertainment Industry*, Mheshimiwa Waziri kaa na hawa wasanii, kaa pia na wizara inayohusika na hilo jambo kwa pamoja naamini na wataalamu wako walivyokuwa wasikivu kwa jinsi nilivyowaona TCRA juzi mtajuwa tu kuna *potential* kubwa kiasi gani wapi watu hawa muweze kuwasaidia wapi muweze *kuwa-guide*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtu mwingine alikua analalamika kwamba wakati mwingine sheria zetu yaani haziko *ku-facilitate* zimejiongoza sana kwenye kudhibiti kuliko *ku-facilitate*. Kwa hiyo, ukikaa na hawa wadau wataweza kukupa mawazo na kueleza kwamba jamani hapa rekebisheni hili hapa *lina-potential* hii, hapa sisi kama wasanii tutanufaika moja mbili ta, hapa kama Serikali tutanufaika moja, mbili, tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni siku ya tatu na asubuhi nilisema nimepita pale TANESCO kuna foleni

unawakuta hadi watu wazima wamesimama pale, watu hawawezi kununua *LUKU online* mpaka sasa hivi. Nimeona Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa maana Waziri wa Nishati ameshaanza kuchukuwa hatua, lakini *that one is not enough* na nimesema hii mambo ya kuombana *excuse* kutupa tahadhari na kutuomba radhi kwamba kutakuwa na 1,2,3 kweli haya mamifumo pengine siyo ya kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwenye wizara yako na *TCRA* ukishirikiana na vyo, kampasi zinazohusika na hayo mambo ya *IT, DIT, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, UDOM* mnaweza mkawa na mifumo ambayo itakuwa na *backup system*, kwamba mfumo A ukifa kuna weza ukawepo mfumo wa dharura ambao unaweza kusaidia lile tatizo kwa muda ule ili kusudi kupata suluhisho la kudumu katika tatizo kuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa mimi hapa ninajitolea mfano; naomba *ku- declare interest*, nina hotel Mikumi toka jana tunawasha *generator* siyo kwamba hatuna fedha ya kununulia Luku, tunayo fedha ya kununulia luku lakini *you can't buy online* kweli Waziri amesema twende ofisi ya *TANESCO* hivi mtu leo hii atoke Mkonze kwa hapa Dodoma kwa mfano aje akasongamane pale *TANESCO*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwanza *TANESCO* yenyewe inajikosesha mapato ambayo ni Serikali, lakini pili unapararize shughuli za uzalishaji sisi wenye viwanda 80 Mafinga kama leo viwanda 30 vimekosa kuwa na *LUKU* toka juzi. Hivi ni ajira kiasi gani umeziathiri, *pay as you n* kiasi gani umeathiri, *SDL* kiasi gani, umeathiri? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza kuona Mheshimiwa Waziri nakuomba sana hii sekta na hii wizara nikwambie kitu yaani wewe ndiyo kila kitu, ukienda kwenye umeme ni wewe, nimesema *Media and Entertainment Industry* ni wewe, ukienda kwa Mheshimiwa Lukuvi unataka kulipa hizo kodi za ardhi itakuwa ni wewe, ukienda kwenye kulipa mishahara utakuwa ni wewe. Kwa hiyo, ninaomba uangalie hii wizara na wataalamu wako kwa jicho ambalo

ni pana kweli kweli ili kusudi changamoto unazokutana nazo kwenye mambo ya *online* tuweze kuondokana nayo kwa sababu tunaenda kwenye uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, kwanza tupate mapato lakini pia *tu-speed up* uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwanza nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Faustine Ndogulile, na wasaidizi wake *Engineer* Kundo Mathew, dada yangu Dkt. Zainab Chaula na Mwalimu wangu Jim Yonazi kwa hotuba nzuri yenye matumaini inayoonyesha kwamba nchi yetu inajielekeza kwenda sawa sawa na dunia nzima kwenye upande wa teknolojia. Tuna walakini hapa na pale lakini lengo lenu linaonekana wazi kabisa ni kwamba mmekusudia tusiachwe na kasi ya dunia hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo mawili ya kuchangia japokuwa nina mengi kwa sababu nimekuwa hapa toka asubuhi leo na michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imekuwa ya kitaalamu na iliyojitosheleza sana, sitaki kuijazia nzi, kuipigia miluzi mingi na kumpotosha Waziri, nafikiri ameandika mengi na anajua mahali pa kushughulikia ili kupata mwelekeo ambao tunaokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na mimi napenda nilitilie msisitizo ni kuhusiana na udhaifu au kukosekana kabisa kwa mawasiliano sehemu kubwa ya vijijini katika nchi yetu. Mimi natoka Jimbo la Muheza ambapo kimsingi zaidi ya nusu ya



Jimbo la Muheza aidha lina mawasiliano dhaifu sana ya simu ama hakuna kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahali ukiambiwa mtu yupo halafu ukampata kwenye simu unaanza kumuuliza kwanza unatumia simu ya aina gani mpaka inapatikana hapo ambayo inaweza kushika mtandao kibabe namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tarafa, kata vijiji na vitongoji vingi ambavyo havina kabisa mawasiliano. Kwa mfano tuna Kata ya Kwezitu iliyopo katika Tarafa ya Amani sehemu yake kubwa haina mawasiliano, Lanzoni kule Kwemingoji hakuna mawasiliano, Kiwanda na Mangugu kwenye Kata ya Tongwe hakuna mawasiliano, Magoroto na Ufinga, Mtindiro, Kwemhanya, Kwebada, Songa, Kwafungo; zote aidha hazina mawasiliano kabisa ama mawasiliano ni dhaifu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nikienda kijijini kwangu yaani simu inakuwa ni ya kuchezea *game* ama kama unataka kufanya shughuli yenye manufaa kwenye simu hiyo uwe umesha-*download* kitabu uende ukaitumie kusomea lakini suala la kuitumia kwa ajili ya mawasiliano halipo kabisa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, sitaki kulalamika tu na kuliacha hili suala linaelea, kwa sababu najua kimsingi *operators* wetu wanafanya biashara na pengine wanasema kwa sababu ya gharama ya kusimika aidha minara hii na gharama ya kuiendesha inawafanya wasifike baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu ninyi ni watu wa kisasa sana, mimi katika pitapita zangu nimeshakutana baadhi ya watu ambao wanatoa teknolojia mbadala ya kufanya shughuli hizi ili tupate matokeo hayahaya tunayoyalilia na wananchi wote waweze kupata mawasiliano kwa kadri inavyotakikana. Mheshimiwa Waziri nikuombe suala la mawasiliano kwenye nchi hii tusilifanye baadhi ya sehemu likawa ni jambo la anasa. Kwa hisani yako nakuomba wewe na Wizara yako sasa muangalie namna

ambavyo mnaweza kupata teknolojia mbadala na kuhakikisha hili suala linatatulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu alikuwa ananiambia kuhusiana na teknolojia ya *new line wireless* na kwa jinsi gharama alivyokuwa anazilinganisha japokuwa mimi sio injinia nilikuwa najuliza kwa nini tumechelewa, kwamba gharama ya kusimika minara hii ni ndogo sana, teknolojia hii haitumii umeme ama mafuta kama inavyotumia hii minara mikubwa ya makampuni kwa maana ya *ma-operator* wetu wa sasa na uwezekano wa kufanya *project* ndogondogo kwa ajili ya kutatua kero za sehemu husika ni mkubwa vilevile.

Kwa hiyo, nawaomba muangalie namna ambavyo tunaweza kupata teknolojia hii na nyingine nyingi za aina hii, najua ziko nyingi na ninyi ni watu wajanja, watu wa kisasa mnaweza kuzipata kwa sababu mme-*specialize* kwenye Wizara mnayoishikilia, mnaweza kutupatia ufumbuzi. Narudia tena Mheshimiwa Waziri tusiache mawasiliano ya kueleweka yakaonekana ni kitu cha anasa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la *YouTube*. Nimekuwa kwenye Bunge lako Tukufu hili toka asubuhi na nimesikiliza michango mingi, nimefurahishwa na *concerns* za Wabunge wengi kuhusiana na mapato yanayopotea ya Serikali na wasanii husika kwenye makusanyo ambayo yanaweza kupatikana kwenye mtandao wa *YouTube*. Kwanza, niseme kwamba ni kweli *YouTube* ina hela lakini kuna *misconception* kubwa, sio hela hizo ambazo Waheshimiwa Wabunge wengi wanaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *YouTube* ni miongoni mwa *platforms* ambazo zinafanya shughuli ya kuuza muziki (*streaming*) lakini sio peke yake, kuna *platforms* nyingi ambazo zinafanya shughuli hii na kimsingi *platforms* ambazo zinapatikana kwenye nchi hii *YouTube* ni ya mwisho kwenye kuingiza mapato yaani inalipa kidogo kuliko *platforms* zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, *YouTube* kwa *views* milioni moja kwa nchi yetu inalipa kati ya dola 400 na

500. Kimsingi *YouTube* inalipa kutokana na nchi ambayo aliyei-*upload* yuko. Kama kuna nchi nyingine ambazo matangazo mengi yanaweza kuwekwa wanalipwa Zaidi, kuna mahali wanalipwa mpaka dola 1,000 kwa *views* milioni moja lakini kwetu ni kati ya dola 400 na 500 kwa *views* milioni moja. Wakati *Spotify* wanalipa kwa namba hiyohiyo ya *views* kati ya dola 7,000 mpaka 10,000 kwa *streams* hizohizo. Tofauti ya *YouTube* na hizi *platforms* zingine ni kwamba *YouTube* yenyewe ni *visual* hizi nyingine unaweza kusikiliza peke yake. Kina *Spotify, Apple Music, Napster, Deezer, Tudor*, zote hizi zinafanya shughuli hiyohiyo na zinalipa zaidi ya inavyolipa *YouTube*. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa tusitoe tu macho kwamba *YouTube* ndio *platform* peke yake inayolipa, kuna sehemu nyingi sana ambazo wasanii wanaweza kupata kipato kikubwa na zinatakiwa kutolewa macho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi *YouTube* inabidi kuwa na *aggregator* lakini nchini kwetu hatuna *aggregator* hata mmoja. Nilimsikia Mheshimiwa mmoja asubuhi ameliweka kama wasanii na *content creators* ni kosa lao au ni ufahamu wao kuwa mdogo. Sisi wengine tumejaribu kuhakikisha nchi hii inakuwa na *aggregator* kwa miaka karibuni minne au mitano iliyopita, siyo suala rahisi, haliwezekani kirahisirahisi. Pengine nimuombe Mheshimiwa Waziri kama tunataka kuwa na *aggregator* basi Serikali iingilie kati ijaribu ku-*harmonize* haya majadiliano kati yetu na *YouTube* tuone kama tunaweza kupata *aggregator* kwenye nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika Mashariki na Kati yote *aggregator* ni mmoja tu Mkenya Ngomma VAS lakini wasanii wote wengine wanatumia *Believe* ambayo ni ya Ufaransa *agent* wao ni Zeze ambao wako Kenya, *Spice Digital* ambayo ni ya *South Africa* ambaye *agent* wao kwa hapa ni Muziki, *Metal Music* ya Nigeria ambayo haina *agent* hapa na Ngomma ambayo ni ya rafiki yangu CLEMO ndiyo ya Kenya. Kimsingi sisi hatuna *aggregator* na watu wengi naowafahamu nikiwemo mimi mwenyewe tumejaribu kupata *aggregator* kwenye nchi hii imeshindikana. Ndugu zangu Wasafi watakuwa mashahidi, *Diamond Platinum* najua alienda

mbele sana lakini kuna mahali alikwama mpaka leo hana hiyo huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yetu iangalie namna ambavyo inaweza kulinda *content creators* wake lakini pia na walaji, yaani watazamaji na wasikilizaji wa kazi hizi zinazowekwa kwenye mitandao. Kwa mfano, *YouTube* ukiwa na *views* zinaonyesha kabisa nyimbo imesikilizwa mara ngapi nchi gani. Kwa hiyo, Marekani wao wanachukua kodi asilimia 30 ya *content* zote zinazoangaliwa ikiwa zimeangaliwa nchini Marekani. Wao wanachukulia kwamba kama mlaji ni Mmarekani basi ametumia *facillities* zetu kuitumia hii *YouTube* kwa hiyo asilimia 30 yetu tunaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali na sisi tuna wasanii wetu wengi na wasanii wa nje ambao wanaangaliwa hapa. Kwa mfano DJ Khaled akiangaliwa Tanzania si inakuwa imeonekana kwamba ameangaliwa mara ngapi na sisi tupate *percent* yetu kama sio 20, 30 lakini tuichukue. Kwa nini Wamarekani wachukue asilimia 30 na sisi tusipate hata *percent* moja wakati walaji ni wetu, fedha na *facillities* walizotumia ni za kwetu na sisi tunastahili kupata fedha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna *platforms* zingine nyingi ambazo ni *plugs* ambazo wasanii wetu wanaweza kuweka mziki wao na wasikatwe hata senti moja yaani wasipite kwa hawa *aggregators*. Ndio maana kwa sasa tumepunguza sana kufuatilia kuwa na *aggregator* kwa sababu tunaona kwamba kuna namna mbadala tunaweza tukaendesha shughuli zetu bila kuwa nao. Kwa mfano, *Caller Tune* wanakutoza kwa wimbo unao-*upload* ama *album* na ni dola kumi ama dola 100 kwa album na unapata ingizo lako lote ya nyimbo zako namna ambavyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakuongeza sekunde ishirini.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nihitimishe kwa kusema kwamba naiomba Serikali hasa Wizara ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iweke dawati maalumu la kwa ajili ya kuwasaidia watu wetu hasa wasanii na *content creator* kuhusiana na ufahamu wa masuala haya. Nasema hivyo kwa sababu tunapoteza pesa nyingi na tuna vijana wengi wa Kitanzania ambao ufahamu wao kwenye masuala haya ni mkubwa wanaweza kutusaidia kutuongozea pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri hiyo *Appipo* ni *Average Revenue Per Viewer*, kila *viewer* akitizama ina gharama yake. Kwa hiyo, wasanii hawa watapata mapato mengi sana na ndiyo maana tunasema kuna ile *digital externalization*, hiyo ndiyo kitu muhimu sasa hivi na ninyi mu-*embark on that*.

Tunakwenda kwa Mheshimiwa Anatropia aliomba dakika tatu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niipongeze michango ya Wabunge walio wengi lakini pia mimi nieleze changamoto ya mawasiliano na hasa ya simu kwa Mkoa wetu wa Kagera. Wakati ninyi mnaongelea kijiji kwa kijiji sisi tunaongelea changamoto ya kata kwa kata yaani inafika mahali kata nzima hawana mawasiliano. Changamoto kubwa ya maeneo yale ni kwa sababu yana miinuko, unaweza kuweka eneo moja kwa sababu kuna bonde eneo la pili lipo na changamoto ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimeomba dakika tatu kueleza changamoto kubwa ya mawasiliano hususani kwenye Jimbo la Karagwe na Kyerwa kwa ndugu yangu pale. Jimbo la Kyerwa kama maeneo mengine tuna changamoto pia au tuna fursa ya kupatikana kwenye mipaka ya nchi ya Rwanda na Burundi. Sasa changamoto

hiyo ambayo inapaswa kuwa fursa ya kibiashara kwetu imekuwa ni changamoto kwenye suala la mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya kuingiliana kwa mawasiliano upande wa Uganda. Ukiangalia kata nyingi ambazo ziko mpakani ina maana sisi tunakuwa na *weak connection* muda wote zinakuwa zinaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama Kata za kama za Murongo, Bugomora, Kibale, Kibingo ukifika tu unapata meseji ya *welcome to Uganda* hapo wewe huwezi kufanya mawasiliano ni changamoto kubwa sana. Sio hapo tu ukifika Kata kama za Isingiro, Kaisho na maeneo mengine unaambiwa *welcome to Airtel Rwanda*, kwa hiyo, tunajikuta muda mrefu sana tuna changamoto ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni kama bonde na liko mpakani wa Rwanda katika Kata ya Songambe linaitwa Kitega, siku moja nimeenda huko nikasema hivi hii nchi mbona kama hili eneo linaweza likavamiwa likachukuliwa kwa sababu hawana mawasiliano ya aina yoyote na wako jirani sana na Rwanda. Kwa hiyo, naomba nieleze...

## TAARIFA

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI.** Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Anatropia kwamba kweli kabisa sisi tunaokaa mipakani kwa mfano kule Tarime ukifika mitaa ya Sirari wanakuambia *welcome to Kenya* unaingia kwenye *roaming*. Kwa hiyo, wale watu wanaingia gharama kubwa maana wanaoneka kama vile wako nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe hiyo taarifa kwamba hayo matatizo yanawakumba watu ambao wako mipakani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, changamoto ya mawasiliano aliyoyasema Mheshimiwa wa Tarime na maeneo mengine ndiyo kwa kiwango inatukuta Kagera. Niombe sana na sisi Kagera hebu tukumbukeni na oneni Kagera kuna fursa ya biashara. Nimeeleza sisi Kyerwa tunapakana na nchi nyingi, kwa hiyo, tuna fursa nyingi za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa changamoto ya mawasiliano ya redio, jamani kwa nini mmeamua kutufundisha tuanze kuongea Kinyarwanda na Kiganda tu maana ndiyo redio tunazosisikia kule. Unataka kupata redio za Tanzania mpaka ifike saa kumi na mbili jioni ndiyo utasikia Redio Tanzania wamefungua, nadhani sio sahihi kabisa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI.** Ahsante, dakika tatu zako zimekwisha. Tunaendelea Mheshimiwa Oscar Kikoyo dakika tatu na wewe.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipatia fursa hii niweze kuchangia kwa dakika tatu kwenye hoja iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuja hapa Bungeni nilimueleza Mheshimiwa Waziri kwamba katika Jimbo la Muleba na Wilaya ya Muleba kwa ujumla tunayo changamoto kubwa ya mawasiliano na kwa heshima kubwa

nilimpatia maeneo yote ambayo yana matatizo ya mawasiliano. Hata hivyo, leo wakati nasoma hotuba ambayo ameivasilisha mbele yetu nimeshangaa sana, hakuna hata kata moja ambayo imezingatiwa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kati ya kata zote ambazo nimempatia, kama mchangiaji aliyetangulia kusema Mkoa wa Kagera tunalo tatizo kubwa la mawasiliano, naomba chonde chonde atusaidie. Kata zote ambazo tumekupatia na sisi kama Mkoa wa kagera tunapaswa kuwa na usikivu wa mitandao, redio ambazo zinachangiwa na walipa kodi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo unakwenda ukipotewa tu huwezi kupata msaada. Tunapongelea Kata za Karambi, Mmbunda na Buhigi hakuna mawasiliano hata kidogo. Nilikuwa na dhamira ya kushika shilingi lakini najua Mheshimiwa Waziri ni msikivu nakuomba utakapokuja kuhitimisha bajeti yako useme neno ili wakazi wa Mkoa wa Kagera roho zao zitulie kwamba tunakwenda kuwawekea mitandao au mawasiliano ili na wao wajisikie wanaweza kuwasiliana na Watanzania wenzao na dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Ahsante. Mheshimiwa Kiswaga dakika saba na Mheshikiwa Dkt. Kimei dakika saba.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia jioni ya leo katika sekta hii muhimu sana ambayo ni sekta mtambuka kabisa katika nchi yetu. Nafahamu kwamba mawasiliano ni muhimu sana ndiyo maana hata ukiangalia Waheshimiwa Wabunge wote hapa wameinamia simu zao kuonyesha kwamba mambo mengi hayawezi kwenda pasipo kuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia eneo moja, mimi niombe kwanza Serikali iwekeze sana kwenye *TTCL* kwa sababu kazi yake ni kutoa huduma. Nimeona mara



nyingi hapa watu wanamlazimisha Waziri kwamba waambie watu wa mitandao waende wakajenge hap ana pale, watu wa mitandao hawawezi kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi kwenye mitandao miaka 20, nilikuwa Mkurugenzi wa Kanda, unaomba minara 50 unaambiwa useme utaturudishia nini (*Return on Investments*). Kwa hiyo, *unless* Serikali wakati inatoa ile *license* ilimwambia yule mtoa huduma kwamba tunataka uende vijijini utujengee minara vijiji 500 lakini kama ulimkaribisha tu ukampa leseni huwezi ukamlazimisha. Kwa hiyo, ni kazi ya Serikali kuona kwamba inaiwezesha hii *TTCL* ipate pesa ya kutosha. Tukiiambia Serikali itoe pesa hizo ndiyo tutakuwa na haki ya kuiambia Serikali hapa sina mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kushauri ni kwamba *TTCL* ijiendeshe kibiashara. Kwenye mawasiliano kuna ushindani mkubwa sana, yaani ushindani kwenye mawasiliano katika nchi ya Tanzania ni mkubwa mno. Huwezi ukasema kwamba *TTCL* ifanye vizuri kama hujaipe pesa! Hata kuajiri kwenye mitandao huwa kunyangana wafanyakazi, mtandao huu ukiona kuna mfanyakazi mahali fulani anafanya vizuri zaidi unapanda dau unamchukua aje kwako. Sasa na sisi kwenye *TTCL* kama Serikali tunaweza kuamua kubadilisha kanuni kwamba namna tunavyoajiri iwe tofauti na yanavyoajiri mashirika mengine ili tuwe na ushindani wa kweli. Tusipofanya hivyo hatuwezi kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo nataka kuzungumzia hapohapo kwenye *TTCL*, mwaka 2003 niliingia kwenye *Task Force* ambacho ni kikosi maalum kwa ajili ya kuuza simu za mezani zilikuwa zinaitwa *People's Phone*, wengi mtakuwa mnazifahamu. Baada ya kuona haziende Kampuni yangu ya Vodacom kwa wakati huo ikaunda timu ya watu watatu na mimi ikaniweka kitengo cha mauzo. Nikafikiria nifanye nini, mimi ndiyo mwanzilishi wa hao mnaowaita *freelancers*, ikabidi niishauri kampuni yangu inipe pesa ili mimi nilete vijana ambao watakwenda mlango kwa mlango kuuza simu. Baada ya kunikubalia, tuliua zile simu

ndani ya mwaka mmoja nchi nzima ilikuwa tayari imeshapata hizo simu za mezani. Kwa hiyo, tuipe nafasi pia *TTCL* ili iweze kutumia huu mfumo wa *freelancers*. Tukifanya hivyo, itaweza kupata wateja wengi, hilo nilipenda kushauri pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ni upande wa Shirika hili la Mawasiliano (*TCRA*). Ninaiomba sana *TCRA* iimarisha mahusiano na watoa huduma. Kumekuwa kama kuna uadui fulani. Nilizungumza siku moja na Waziri kwamba huyu mtoa huduma akifanya kosa kidogo, anapigwa faini kubwa. Kwa hiyo, kumekuwa kuna uhasama wakati mwingine kati ya watoa huduma na hiki chombo ambacho kinadhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara inahitaji mahusiano duniani, usipokuwa na mahusiano, huwezi kufanya biashara. Kwa hiyo, napenda Waziri hilo alisisitize sana kwa watu wake. Hii *TCRA* isiwe Polisi. Ikiwa Polisi, itaharibu biashara, nasi tunahitaji biashara. Kama tunataka hawa watu wawekeze, ni lazima tuwabembeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni *UCSAF*. *UCSAF* nayo siamini sana kama inapewa pesa ya kutosha. Naishukuru Serikali kwa kuamua kutengeneza huu mfuko ili kusaidia mawasiliano vijijini. Kama nilivyosema kwamba hawa watoa huduma wengine kwenda vijijini hawawezi kwa sababu minara mingi vijijini, unakuta mnara unaleta shilingi milioni moja. Wewe umejenga kwa shilingi milioni 300, lakini kwa mwezi unakupatia shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unauhudumia huu mnara kwa shilingi milioni 4.8 kwa sababu mnara mmoja kuweka majenereta unaweka lita 2,000 za mafuta unakuta kwamba unatumia kati ya shilingi milioni 4.8 mpaka shilingi milioni tano kwa ajili ya kuuhudumia, lakini unakupa shilingi milioni moja au shilingi 800,000. Kwa hiyo, hakuna mtoa huduma ambaye atakuwa na hamu ya kwenda huko. Ndiyo maana tunaomba

hii UCSAF ipewe pesa ya kutosha ili Watanzania wengi wapate mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nije kwenye Jimbo langu. Jimbo langu nalo lina mawasiliano hafifu katika kata nyingi. Ukiangalia Kata za Magulilo, Wasa, Mgama, Kiwele, Ulanda, mawasiliano yako hafifu.

Pia kuna Kata moja ya Masaka, haina mawasiliano kabisa na Kata ya Kihanga pamoja na Kata ya Wasa, naiomba Serikali, kale kasungura kadogo ambako tunakwenda kugawana, nami basi kule Kalenga Waziri unikumbuke kidogo kupitia mfuko huu. Siwezi kusema nikushikie shilingi hapa, siwezi kwa sababu najua huna pesa. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsaidia tu Mheshimiwa kwa kumwambia kwamba *TTCL* ilikuwa na minara nchi nzima ikauza kwa *American Tower*, sasa hivi inakodi. Yaani iliua kwa gharama nafuu, sasa hivi inakodi minara. Sasa tutapataje mawasiliano? Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninachosema ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, ni kwamba nami mwenzako...

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa hiyo, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafafanua anachozungumza huyu; anachozungumza ni suala tu la kimazingira kwamba ilikuwa ni makubaliano ya makampuni

na Serikali iliridhia kwamba hatuwezi kuwa na minara mingi, kwa sababu mnara ule mmoja siyo mawasiliano, kinacholeta mawasiliano ni zile *antenna* tunazofunga.

Kwa hiyo, kampuni hata tano zinaweza zikafunga kwenye mnara mmoja na bado watu wakapata mawasiliano ya makampuni tofauti. Kwa hiyo, hilo lisikutishe kuona mahali minara inaondolewa, lakini hata ukibaki mmoja, makampuni hata kumi yanaweza yakautumia mnara mmoja na mawasiliano bado watu wakaweza kupata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kule Kalenga...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dakika zako saba zimekwisha. Mheshimiwa Dkt. Kimei. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nami nianze kwa kumpongeza Waziri mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa kuweza kuwasilisha hotuba yake vizuri, hotuba nzuri iliyosheheni ubunifu mkubwa na ninaamini kwamba atakwenda kutekeleza kama walivyoainisha kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba tunamshukuru Waziri kwa sababu ni mtu mnyenyekevu sana. Mimi toka nije hapa Bungeni sijaona Waziri amenifuata akaniambia pale kwako vipi mambo? Kwenye mambo ya mawasiliano yako sawa? Sijaona. Sijaona mwingine aliyenifuata akaniambia vipi maji? Sijaona; lakini yeye ameweza kuja kwetu na kutuuliza kwamba vipi tunaonaje mambo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa kuamini kwamba zile Kata zetu za Kirua Vunjo, Marangu, Mwika na

Makuyuni ambapo pia tuko mpakani, lakini zaidi ni kwamba vijiji vingi vimepakana na Mlima Kilimanjaro na msitu. Kwa hiyo, kule mawasiliano yanakuwa ni vigumu sana. Naamini tutatafuta mbinu ya kupeleka minara au kupeleka njia nyingine za mawasiliano kwa hawa watu walio kule kwenye mpaka na kwenye vijiji ambavyo kusema kweli hawapati mawasiliano sasa hivi na kidogo wanayopata ni ya Kenya, hata kama ni redio pia zinapatikana za Kenya na siyo sehemu nyingine. Kwa hiyo, nataka niwaombe watekeleze hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kukazia mambo machache. Natumai yanaweza yakawa yamezungumzwa, *issue* ni kwamba ni lini tutaweza kufungamanisha mifumo yetu ya utambulisho wa wananchi? Utambulisho wa wananchi umekuwa ni tatizo kubwa. Ukitaka kwenda kwenye *Passport* unaambiwa jaza fomu zile zile ambazo unajaza unapokwenda *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mahali utakapokwenda utajaza; hospitali utajaza, utarudia na bado una kitambulisho chako cha *NIDA*, lakini bado ukienda hospitali hawawezi kutumia kile kitambulisho waka-*access* zile *data* kwa sababu ile *database* inaonekana kwamba bado hajifungamanishwa ili iweze kuwa *accessed* na wadau wote wanaotaka kupata taarifa za mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungamanisha huko pia kunawezesha kabisa hata kuongeza usalama kwa sababu ukweli ni kwamba mtu anapofanya makosa; na kama anajua kwamba namba ya *NIDA* aliyonayo, yale makosa yataandikishwa kule, basi anakuwa na uwoga zaidi kwa sababu inakuwa ni rahisi kumfuatilia mtu makosa aliyofanya na mazuri aliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na inakuwa ni rahisi sana hata kwa mabenki kuweza kumfahamu huyu mtu ni wa namna gani wanaku-*access* katika *database* ile ambayo itakuwa imefungamanishwa kwa watu wote, iwe ni simu na kila kitu kitakuwa kule. Naamini kwamba kwa zile *reference bureau* nazo zitaingiza *database* yao huko. Kwa hiyo,

tutakuwa tunaweza kufanya mambo kama hayo. Nchi zote zilizoendelea zinafanya hivyo, mtu anakuwa na namba moja, hawi na namba mbili, na ninaamini kwamba kitambulisho kinakuwa ni kimoja siyo viwili ili mtu yule aweze kutambulika kila mahali anapokwenda na saa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba sekta ya TEHAMA ndiyo inayokuwa kwa kasi zaidi sasa. Sasa tumeunda Wizara ya Teknolojia na TEHAMA kwa ujumla. Nataka niseme hivi, fursa zilizopo ni nyingi sana, nchi nyingine zimeamua kufanya kwamba TEHAMA ndiyo sekta ya muhimu kuliko zote; nchi kama Rwanda mnafahamu. Nia yake ni nini? Ni kwa sababu wako vijana wengi wanapokwenda shule na kwenye vyuo wanajiunga kwenye hii fani, lakini kuwatumia inakuwa vigumu. Kwa sababu hakuna mitandao inayofanya kazi vizuri kwenye maeneo yale ambayo vijana hao wanamalizia shule zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna mkonga, kwa nini hatuwezi kuwezesha *Wifi* ikapatikana kwenye maeneo mengi tu hata kwa bure? Nami nakubaliana na mwenzangu aliyesema kwamba *TTCL* ikiwezesha ikatumia mkonga huu ikawekeza vizuri kwenye maeneo mengi ya vijijini, siyo mijini tu, vijijini zaidi kwa sababu kuna fursa. Sasa hebu niulize kwa mfano, masoko sasa hivi hayatafutwi kwa mtu kusafiri kwenda kuangalia soko, mtu anatumia simu, hii simu imekuwa ni ofisi, huhitaji ofisi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawaambia wapigakura wangu kwamba hii simu ni ofisi yenu, huna haja ya kwenda kutafuta mnunuzi wa ndizi Dar es Salaam wakati unaweza ukapiga ndizi yako picha ukaituma kwa rafiki yako Dar es Salaam akakwambia nitumie kwa shilingi fulani, umeshafanya biashara. Kwa hiyo, biashara unaweza ukaifanya kwa kutumia tu kiganja chako na uwe na simu, lakini iwe janja kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niombe hiyo kwamba kweli tufanye hivyo. Pia Wizara ione namna ya kutoa mafunzo kwenye vyombo vya Habari; kwenye TV na

kwenye redio, kueleza watu ni fursa zipi zinafunguliwa kwa kuwa na uwezo wa kuwasiliana nchi nzima na nchi za jirani, hata dunia nzima inawasiliana na hii simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vile vile lazima gharama zipunguzwe. Sasa tutapunguzaje gharama? Nafikiri kwamba tunavyozidi kuongeza mtandao, hasa huu wa *TTCL*; na tunaamini kwamba wataweza kuleta ushindani ambao utalazimisha wale wengine ambao wanafanya tu biashara waweze kushusha bei zao, lakini ni lazima *TTCL* ifanye kazi kwa nguvu zaidi. Kwa hiyo, naomba kwamba kuwepo na hivyo vipindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mheshimiwa alizungumzia kuhusu *technology hub*. Tuna *COSTECH*, imeweza kuanzisha *incubation centers* na hizo *incubation centers* ndiyo zinachukua na zinashindanisha; unaweza ukatangaza kwamba watu wenye uwezo hasa wale waliosoma *IT*, ambao wana ubunifu wowote wa teknolojia, waweze kufikisha pale. Hiyo ndiyo njia ambayo itaweza kuwaajiri hawa vijana na pia ku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kimei kwa mchango mzuri.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kwa michango mizuri sana ambapo mmeonesha weledi mkubwa sana katika Bunge hili. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa

rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwepo ndani ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda niwapongeze Menejimenti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Faustine Ndugulile; Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula; na Dkt. Jim Yonazi, kwa ajili ya kazi hii kubwa ambayo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango, maoni na ushauri walioutoa, hakika imeonesha namna gani sote tunatembea katika njia moja ya kuhakikisha kwamba sekta yetu na Wizara yetu ya Mawasiliano inazidi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyagusia. Tukianza na masuala ya minara ambapo baadhi ya Wabunge wameweza kuonesha kwamba katika maeneo yao kuna changamoto ya minara; mingine ambayo haijawaka, pia ambapo inasababisha na wengine wanasema kwamba ndoa zinavunjika na wengine wanatumia miti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala ambalo linahusika na masuala ya mipakani ambapo kuna changamoto ya gharama za mawasiliano kupitia *roaming* ambayo inafanyika katika mipaka. Naomba nikufahamishe kuwa suala la *roaming* tayari Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano tumeshalifanyia kazi na tayari tumeshaingia mkataba, *Roaming Agreement* na wenzetu wa *East Africa* ili kuhakikisha kwamba gharama za kupiga simu ukiwa katika maeneo ya mipakani zinashuka. Hivyo basi, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wakiwepo katika maeneo hayo, basi hili ndilo ambalo linakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu tuna changamoto ya mawasiliano mipakani. Changamoto hii



inatokana na mwingiliano wa mawasiliano na kuna maeneo mengine ambayo hakuna kabisa mawasiliano, lakini kupitia Mfuko wa Mawasiliano wa Wote, tumeshafanya tathmini na tunakwenda kuhakikisha kwamba mipaka yetu yote inakwenda kufikishiwa mawasiliano ili kuhakikisha kwamba changamoto hii inaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mipaka hiyo takribani minara 160 ambayo itajengwa katika kuzunguka nchi yetu yote katika maeneo ya mipaka, tunafahamu pia kuna baadhi ya ofisi za Halmashauri ambazo ni mpya lakini bado zina changamoto ya mawasiliano ikiwepo Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ambapo tunakwenda kuweka huduma ya mawasiliano; tuna Wilaya ya Tanganyika, Kakonko, Malinyi, Mtwara DC, Msalala DC, Bariadi, Nzega, Kilindi pamoja na Pangani. Maeneo haya tunakwenda kuhakikisha kwamba katika zabuni ya awamu ya sita yanaingizwa na utekelezaji wake utaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wameongelea masuala ya *co-location*. Nasi tangu tulivyoteuliwa tarehe 5 Desemba, 2020 na kwa maelekezo mahususi kabisa, mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri tulitoa maelekezo kwamba kuanzia sasa hatutajenga mnara ambao utakuwa unatoa huduma ya *operator* mmoja. Kuanzia sasa tutakuwa na *cost sharing*, maana yake kutakuwa na *co-location*, mnara mmoja uweze kuhudumia makampuni mawili au matatu kulingana na uhitaji wa eneo husika. Kwa hiyo, hayo tunakwenda kuyafanyia kazi kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo haya yameendana sambamba na kuhakikisha kwamba tunatoa maelekezo kwa watoa huduma kuhakikisha minara yote ambayo ilijengwa ikiwa inatumia teknolojia ya 2G, yote inakuwa *upgraded* na inatoa huduma ya 3G na 4G. Pia Serikali bado inaendelea kujiridhisha na uhitaji iwapo tutahitaji 5G na pia soko litaamua ni nani atahitaji kutumia. Serikali kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu na sera

safi za kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu wanaweza kufanya biashara bila kuwa na changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu kabisa kwamba tuna changamoto; na Waheshimiwa Wabunge wamegusia masuala ya vifurushi. Katika suala la vifurushi Waheshimiwa Wabunge wameuliza kwa nini tuwe na *bundles*? Kwa nini tusiwe na utaratibu wa kutumia mpaka ukamaliza salio lako wewe mwenyewe? Kwa kutumia nafasi hii, naomba nikufahamisha kwamba suala la *bundles* ni sawa sawa na gharama au biashara ya jumla, lakini Mtanzania hajalazimishwa kununua vifurushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna huduma ya aina mbili; *pay as you go*, maana yake ni kwamba unatumia kwa kadri wewe mwenyewe unavyohitaji, lakini pia tuna huduma ambayo ndiyo ya vifurushi sasa ambapo utaamua kuchagua kifurushi cha siku moja, siku mbili, siku tano, ni wewe mwenyewe. Changamoto ambayo tumeiona, siyo kwamba ni kwa nini tununue vifurushi? Watanzania hawajui matumizi, namna gani yanatumika katika simu zao? Sasa hilo Serikali tumeanza kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba Mtanzania awe anajua *bundle* lake limetumika wapi; na ametumia kiasi gani na kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumekuja na utaratibu ambao tunakwenda kuhakikisha kwamba ukishanunua *bundle* lako kuna njia mbili za kuhakikisha kwamba halipotei. Iwapo muda wa matumizi, kwa mfano, umenunua *bundle* la siku saba, lakini inafika siku ya saba umeshatumia *GB* labda tatu na ulikuwa umenunua *GB* kumi, utakuwa na fursa mbili; ya kwanza ni ku-*top up*, maana yake utanunua *bundle* lile lile ambalo ulikuwa umenunua hapo awali maana yake tuta-*carry forward* ile *balance* ya *bundle* lako la hapo awali, maana yake ni kwamba utalitumia. Kama ulikuwa umebakiza saba, maana yake ni kwamba ukinunua 10 utakuwa na 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukajua kwamba kuna changamoto nyingine, mwingine atakutwa hana salio la

kununua hilo *bundle* au ku-*top up*, maana yake ni kwamba utakuwa unaruhusiwa sasa kuhakikisha kwamba unamhamishia rafiki yako ambaye ataweza kuitumia hiyo *bundle*, nafikiri itakuwa kwa maelewano yenu ninyi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuwa umehakikisha kwamba *bundle* lako, kama ni *10 GB* utakuwa umeweza kuzitumia zote. Kama utashindwa kuzitumia zote, basi rafiki yako. Tutakuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba kiwango cha chini cha kuhamisha *bundle* ni *MB250*, lakini utakayemhamishia hataruhusiwa yeye kumhamishia mtu mwingine. Utakayemhamishia, yeye ataruhusiwa kuitumia mpaka itakapokwisha. Haya yote tunaendelea kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu kwamba kuna changamoto ya masuala ya gharama. Serikali ni Sikivu; na hili tunaendelea kulifanyia mchakato, tutakapokuwa tumejiridhisha, kwa sababu biashara hii inahusisha pande tatu; Serikali, watumiaji na watoa huduma, pale ambapo tutaamini sasa kwamba tumefikia maelewano ya kutosha, basi tutakuja na mpango ambao utahakikisha kwamba unawasaidia Watanzania ili waendeleo kufanya biashara mtandao na kufanya mambo mengine ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba tunaelekea katika uchumi wa kidigitali. Uchumi huu wa kidigitali tunahitaji kuwa na uwezo wa kufanya biashara mtandao, biashara mtandao hii inatokana na miundombinu ambayo tutakuwa nayo sisi Watanzania, miundombinu ambayo itakuwa wezeshi ambazo ndiyo *drivers* za kutufikisha sasa kwenye uchumi wa kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa tuna miundombinu ya aina tofauti; kuna Mkongo wa Taifa ambao mpaka sasa tumeshajenga takribani kilometa 7,910 na tayari kuna zingine tena tunaelekea kujenga kilometa 409. Vilevile katika mwaka fedha huu ambao tunaomba bajeti hii tunaenda kujenga kilometa 1,880. Kadri ambavyo muda

unaenda, tutakuwa tunahakikisha kwamba baadhi ya changamoto tunazifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nashukuru Waheshimiwa Wabunge wamegusia suala la *National Internet Data Center*, kwa kweli *Data Center* yetu ina uwezo mkubwa ni *three tier* kama walivyosema ambayo ina *interruption* ambayo inaenda kwenye 99.82 ambapo kwa kweli hii ni ya kiwango cha juu, kwa sababu kiwango cha juu kabisa katika ubora wa *Data Center* ni *tier four*. Sasa tunaamini kabisa kwamba katika Afrika Mashariki na Kati *Data Center* yetu inatosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wakiwa na biashara zao, wakiwa na makampuni yao, *Data Center* yetu ni sehemu sahihi kwa ajili ya kutunza taarifa zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miundombinu ya anuani za makazi na postikodi; ili tuweze kufanya biashara mtandao kuna mazingira ambayo yatatufanya sasa tuweze kufanya biashara yetu bila kuwa na changamoto yoyote. Wizara yetu tayari imeshatenga bilioni tatu katika mwaka wa fedha 2020/2021, lakini imetengewa kiasi kingine katika bajeti hii inayokuja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anuani za makazi na postikodi zinakuwa vizuri. Hii faida yake ni kwamba; wenzetu wa halmashauri itawasaidia kupanua wigo katika ukusanyaji wa mapato. Pia Mamlaka ya Mapato Tanzania itawasaidia kuwajua walipakodi wao na wafanyabiashara wao ili kuweza kuhakikisha kwamba wanapofikia hatua ya kukusanya kodi, basi watawafikia kiurahisi, kwa sababu hii itaweza kutoa anuani pale ambapo mlipa kodi alipo na nyumba anayokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuja na mfumo wa kuhakikisha kwamba una uwezo wa kumfikia mwenzako pale alipo kwa kutumia *application* inaitwa *NAPA*, ambapo sasa badala ya kutumia *Google Map*, sisi tumejiongeza na kuhakikisha kwamba tunatumia mfumo wetu ambao umejengwa na vijana wa Kitanzania, ambao ni vijana wetu,

kwa sababu sisi kama Serikali tumeamua kuhakikisha kwamba tunawekeza zaidi katika *local content*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo *local content* ambayo ni ya watu wa kutoka nje, ni *local content* ikiwa na maana anayefanya kazi ni Mtanzania mwenyewe na vilevile anayedeployni Mtanzania mwenyewe. Kwa hiyo tunaamini kabisa iwapo anuani za makazi, mradi huu utakapokamilika na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tutakapofika katika halmashauri zao waweze kutupa ushirikiano pale ambapo tutakuwa tunaweka hizi alama na majina ya mitaa, basi tusiwe na changamoto yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tunautekeleza kwa ushirikiano mzuri sana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Pia tunawapongeza sana Wakurugenzi nchini kote wamekuwa wakitoa ushirikiano wa kutosha. Tunaamini kwamba tukishafikia hapa basi tutakuwa tuna uwezo wa kufanya biashara mtandao, tutaweza kuagiza bidhaa yoyote ukiwa umekaa nyumbani na ukaweza kufikishiwa nyumbani bila kuwa na changamoto yoyote. Tunaendelea vile vile kuimarisha mifumo yetu ya kifedha ambayo haitotoa nafasi ya udanganyifu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba teknolojia inakimbia kwelikweli lakini na sisi tumejipanga kwelikweli kuhakikisha kwamba iwe kama mwizi na Polisi, kwamba hatutaki kuachwa nyuma, kama itafikia sasa wakati ambapo itabidi tutumie *block chain technology* huu ndiyo wakati wenyewe. Tutajiridhisha wapi tutumie na tutakapokuwa tayari Waheshimiwa Wabunge, basi tutakuwa tumefikia katika lengo ambalo litakuwa linasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge pia wameongelea suala la utapeli mtandaoni, hasa tuma pesa kwa fulani, tuma kwenye namba hii. Naomba nikujulishe, tumeunda Kamati, ambapo kikao cha Makatibu Wakuu ambao tunalenga katika hii sekta sana sana katika masuala ya *cybercrime*, maana kwamba nani hii makosa ya kimtandao, wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia Habari na watu wa Sheria watakaa tarehe 20 kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuhakikisha kwamba haya masuala tunayatataua. Ikiendana sambamba na hiyo, tarehe 26 kikao cha Mawaziri pia kitakaa kwa ajili ya ku-*finalize* na kujua kwamba tufanye jambo gani. (*Makofi*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Dakika ishirini.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwashukuru Wabunge wote pamoja na Kamati kwa maoni mazuri. Nami niwahakikishieni ma-*crownyote* tumeyachukua na tutayazingatia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wachangiaji wote; tumepokea michango 28 ya Wabunge ambao wallichangia hapa ndani Bungeni, 40 michango kupitia kwenye kamati lakini tumepata michango nane kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba Wizara yetu sisi ni Wizara mtambuka. Ni Wizara wezeshi na Wizara ambayo inasaidia sekta nyingine zote na kuwezesha sekta nyingine zote. Kwa nini kumeanzishwa Wizara hii, nataka nitumie fursa hii kutoa elimu kidogo kwa Wabunge, kwamba Wizara hii imeanzishwa mahsusi kuangalia jinsi gani sisi kama nchi wakati dunia inaongelea mapinduzi ya nne ya viwanda *forth industry revolution* ambayo msingi wake mkubwa ni TEHAMA, basi na sisi kama nchi tuweze kujiandaa katika msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inaongelea masuala ya *digital economy* na ukiangalia sasa hivi, ukiangazia miaka 10 iliyopita, makampuni makubwa duniani yalikuwa katika *manufacturing*, lakini sasa hivi ukiangalia makampuni makubwa yapo katika sekta ya TEHAMA. Kwa hiyo, sisi kama nchi ni lazima tuangalie na tuangazie huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu swali ambalo ameniuliza Mheshimiwa Neema Lugangila ni kwamba ndiyo tupo katika maandalizi ya sasa hivi ya kuandika *digital economy blue prints* ya Tanzania. Kazi hiyo tumeshaanza hatua za awali na tunatarajia andiko hilo litaweza kuanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunataka kuangazia *e-commerce* na Wabunge wamesema, *element* za *e-commerce* tumeanza nazo nchini. Sasa hivi ukiangalia wafanyabiashara wanjanja ama vijana hawatumi sasa na wala hawaendi pale Kariakoo kukodisha fremu, mtu anaagiza mzigo wake anaweka nyumbani, anapiga picha anaweka kwenye mitandao ya jamii. Wewe ukitamani, unaingia katika mtandao ya jamii, unachagua pale, mnalipana kwa miamala ya simu, anamtuma boda boda anakuletea nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale hamna kodi ya jengo, hakuna leseni za *TRA*, wala leseni za biashara ni lazima na sisi tuwezeshe ili kuweka mifumo mizuri kuhakikisha kwamba *e-commerce* hata wewe sasa hivi unaweza ukaagiza mzigo nchi yoyote ya nje na mzigo wako ukaweza kukufikia. Huo utaratibu ambao tunakwenda nao wa anuani za makazi na postikodi, tunataka mzigo ukufikie wewe nyumbani pale pale ulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaangazia sasa hivi kuhakikisha kwamba Serikali inamfuata mwananchi mkononi badala ya mwananchi kwenda kupanga foleni katika Ofisi za Serikali, tunataka ku-*digitize service* za Serikali ili mwananchi aweze kupata kiganjani, kodi

za ardhi, masuala haya ya umeme na huduma nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangazia vilevile kuhakikisha kwamba huduma za jamii, hawa Walimu wachache tuliokuwa nao nchini hao hao tuweze kuwatumia waweze kutoa huduma za elimu katika maeneo mengine ambayo wana-*shortage* ya Walimu. Tuangazie kwamba badala ya Waziri wa Elimu kuhangaika kuchapisha vitabu, tunaweza tukatengeneza *DG e-books* na kuweza kuzisambaza na mwanafunzi akawa na kitabu chake kwa njia ya mtandao. Tukaachana na hizi *library* ambazo zimejazana vitabu vikuu vikuu, hizo *space* zikageuzwa kuwa madarasa badala yake mtoto akawa anasoma na akapata kitabu pale pale alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangazia kwamba Madaktari wetu wachache tuliokuwa nao waweze kutoa huduma kwa maeneo mengine ya pembezoni ambapo hakuna Madaktari Bingwa. Hilo tumelianza katika upande wa *teleradiology* ambapo sasa hivi tunafanya *installation* ya *digital x-ray*, Madaktari wetu Bingwa ambao wanaweza wakasoma *x-ray*, *MRI* na vitu vingine, picha inaweza ikapigwa Tandahimba ikatumwa Dar es Salaam pale *MOI* ikasomwa na majibu ndani ya dakika 15 yakarudishiwa kule kule alipo mwananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuangazia katika Sekta ya Kilimo, mkulima kule kule alipo akiwa na simu janja aweze kupata ushauri kuhusiana na masuala ya mbegu, masuala ya wadudu waharibifu, kuhusiana na mbolea na kuhusiana na masoko kule kule katika eneo ambalo yeye yupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuangazia mchango wa sekta hii katika uchumi na pato la Taifa letu. Wataalam wanasema tukiwekeza katika Sekta ya TEHAMA *by 10 percent* inaweza kusaidia kukuza Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 1.5. Sasa nini tunachotaka kukiangazia, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetuelekeza



sisi, kuhakikisha kwamba tunakuza Mkongo wa Taifa kutoka asilimia 45 tuliokuwepo sasa hivi hadi kufikia asilimia 80 na kuongeza mahitaji ya matumizi ya *internet* kutoka asilimia 43 mpaka asilimia 80 ambayo imeelezwa pale katika Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua gani ambazo tunazichukua sasa hivi? Mheshimiwa Naibu Waziri ametoka kusema, sasa hivi tunavyoongea Mkongo wa Taifa tunakwenda kufikia kilometa 8,319. Katika mwaka huu wa fedha bajeti kama Wabunge watatupitishia tena hapa tutakwenda kujenga kilometa 1,880, tumeshafika katika Makao Makuu yote ya Mikoa, bajeti wakitupitishia Wabunge tunakwenda kufikisha katika Makao Makuu ya Wilaya zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu tukifika 2025 tunataka tufikie Mkongo kilometa 15,000. Sasa hivi tumeweza kufikia nchi zote za Jirani, sasa hivi tunafanya upembuzi yakinifu tuweze kuunganisha na *DRC*. Changamoto ambayo tumeipata sasa hivi kwa sababu ya kina cha Ziwa la Tanganyika ndiyo tunajaribu kuangalia teknolojia gani ambayo tunaweza kutumia ili kuhakikisha kwamba mkongo na sisi tunaweza tukaufikisha kule *DRC*. Lengo letu na sisi tuwe ni *hub* ya *TEHAMA* katika Afrika Mashariki na tuweze kuwafikia wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea na nikimaliza Bunge naenda Mtambaswala sasa hivi tunafanya kwenye *connectivity* na Msumbiji, ili kuhakikisha kwamba mawasiliano yetu na sisi tunawafikishia kule Msumbiji. Sasa na hatua gani nyingine ambazo tunaendelea kuzichukua ili sasa tuweze kuwa na usimamizi mkongo ambao ndiyo *highway*, ndiyo njia kuu ya mawasiliano na ndiyo moja ya njia kuu ya uchumi kama ilivyo reli, barabara pamoja na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa nao ni moja ya njia kuu, tutakapokuwa tunaongelea huko masuala ya barabara na tukumbuke vile vile suala la Mkongo wa Taifa

ambao ndiyo njia kuu ya mawasiliano ndani ya nchi yetu. Mawasiliano sasa hivi si anasa ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Tunakwenda kuboresha usimamizi wa mkongo na tunakwenda kuanzisha chombo ambacho kazi yake kikiamka asubuhi ni kusimamia, kuendesha na kuendeleza suala hili la mkongo, tumeshaanza mchakato huo na tunaamini ifikikapo Julai Mosi, jambo hili tutakwenda kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo suala la kuwekeza katika miundombinu halitoshi peke yake, tunataka sasa tuwekeze katika *digital literacy*. Tukiangalia Watanzania wengi bado hawana uelewa mzuri wa matumizi ya *internet*, hata sisi Wabunge tunatumia chini ya asilimia 50 ya uwezo wa simu zetu. Tunakata tu-*invest* kuhakikisha kwamba tunajenga *digital literacy*, elimu ya kutosha katika masuala ya haya ya TEHAMA, lakini sambamba na hilo kuhakikisha kwamba tunakuwa na matumizi sahihi na mazuri ya *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya hayatakuwa na tija kama uwezo wa Watanzania kuweza kumudu kununua simu janja na vifaa mpakato. Sasa hivi tunataka kujielekeza kuhakikisha kwamba vifaa mpakato vinapatikana kwa gharama nafuu. Moja ya mkakati ambao tunao ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda vya ku-*assemble* ama kujenga viwanda ambavyo vitatengeneza simu janja hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunataka kuongeza wigo wa *internet* na tumewasikia Waheshimiwa Wabunge, ni kweli mwanzoni tulipokuwa tunaanza mikakati yetu ilikuwa lengo ni kuwafikishia mawasiliano na ndiyo maana mitandao yetu mingi ilikuwa 2G, lakini tumekubaliana sasa minara yote tunayoenda kujenga sasa hivi itakuwa ni 3G kwenda juu, ili kuwezesha sasa Watanzania walio wengi waweze kupata huduma za *internet*. Hakuna mtu ambaye anayesema kwamba vijijini eti nao hawahitaji *internets*, tunataka hata wale wa vijijini waweze kutumia *internet* kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kujiletea maendeleo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda ku-*harmonize system*, sasa hivi kama unavyofahamu miaka mitano iliyopita mifumo yote nchini ilikuwa ya kutoka nje ya nchi, lakini sasa hivi tumepiga hatua mifumo mingi ya TEHAMA ndani ya nchi sasa hivi asilimia 80 tunaitengeneza hapa hapa nchini. Changamoto ni kama hizi ambazo zimejitokeza kwa hii katika mifumo ya LUKU, bado kuna changamoto ya mifumo kuingiliana, bado kuweka mifumo ya *backup* na bado kuna mianya kidogo ambayo inaweza ikawa ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote Wizara yetu itaendelea kuyasimamia na kuhakikisha kwamba tunaweka mifumo mizuri na sahihi. Pia tutahakikisha kwamba hii mifumo ambayo imetengenezwa na vijana wetu wazalendo inakuwa ni *robust* na inaweza ikasimama na tunakuwa na mifumo mingine ya *backup* ambayo inaweza ikasaidia, pakitokea tatizo basi kunakuwa na njia mbadala ya kuweza kupata huduma zile husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunakwenda kufanya maboresho ya sheria. Wizara yangu na sekta yangu ni sekta ambayo inakwenda kwa kasi sana. Tumekuwa na sheria ambazo zimekuwa ni za muda mrefu sana. Niombe kusema na nasimama mbele ya Bunge hili kusema, sitaki kukumbukwa kama Waziri ambaye alikuwa ni Polisi wa sekta, nataka nikumbukwe kwamba ni Waziri ambaye alikwenda kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya TEHAMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, sitaki kukumbukwa kwamba Waziri ambaye alienda kuminya na kuwa Polisi wa sekta, nataka nikumbukwe kwamba ni Waziri aliyeweza kuweka mazingira wezeshi ya Sekta ya TEHAMA kukua ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara tunakwenda kufanya mabadiliko makubwa sana ya kimuundo ya taasisi zangu, lakini muundo wa kisheria, ikiwa ni pamoja na hawa vijana wetu ambao wanajajiri kupitia TEHAMA. Kijana ni *MC* anafanya shughuli zake za harusi,

anarusha picha zake kwenye *You Tube* ili watu wengine mumwone umahiri wake wa kazi halafu sisi tunataka kumtoza kodi, hili tunataka tuondokane nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu hawa wasanii, wanatengeneza nyimbo zao, sasa hivi hawauzi *cassette* wala hawauzi *flash*, wanaziweka huko kwenye mitandao na huko ndipo wanapata mapato yao sisi tunaenda kuwaminya tena kule. Tunataka kwenda kufanya maboresho makubwa ambayo yatatengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha hizi *platform* sisi tusiwe ni kizuizi bali tuwe ni watu ambao wanakwenda kuhakikisha kwamba hawa vijana wanaweza kujiajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tutakwenda kuliangalia suala la visimbuzi nalo nimeshatoa maelekezo tarehe 21 watoa huduma, watoa huduma sijui wa visimbuzi wote, watu wa *television* wote tarehe 21 nimewaambia wakae, wakae kama wadau wakubaliane yale makubaliano sisi Serikali tutayachukua na tutayabariki, tunataka tufanye mapinduzi makubwa hata katika hii tasnia ya wenzetu ya *television*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunahitaji tuwe na mabadiliko ya fikra na sisi kama Wabunge tunahitaji tufikiri upya sasa hivi katika sekta hii TEHAMA, Tanzania tupo nyuma sana, wenzetu Kenya, Rwanda, Ghana, Nigeria wapo mbali, kuna vitu vinaitwa *startup* sasa hivi. Vijana wa sasa hivi hawatengenezi makampuni ya wajukuu wao kuja kurithi, wanatengeneza makampuni ambayo lile wazo lake likikubalika likaingia katika soko anauza, anaenda kuanzisha kampuni mpya. Wale vijana hawana hela wana mawazo na wazo lake lile ndiyo hela. Ni lazima tuwatengenezee mazingira wezeshi hawa vijana yao ili kazi ziweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wa *software development*, nawafahamu wanafanya kazi kubwa Israel, wanafanyia kazi Uingereza, ni Watanzania, lakini sisi hatuwatambui na wala hatuwatumii. Nimeongea na vijana baada ya Bunge hili, naenda kukutana na *Tanzania Startup*

*Association*, kukaa na kuangalia mahitaji yao na pale tutakapohitaji tutawaleta Waheshimiwa Wabunge mabadiliko ya sheria ili kutengeneza mazingira wezeshi kwa hawa *Startups*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimenong'ona na Waziri mwenzangu wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, wasanii Mheshimiwa Mwinjuma tumewasikia tutakuja tukae tuongee na nyinyi tuangalie *challenge* zenu, tuangalie hayo masuala ya *aggregation* na tuangalie jinsi gani tunaweza kufanya ili sasa tupige hatua kwenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TTCL*, ni kampuni yetu na katika Ilani ya uchaguzi imeelezwa kwamba, tunahitaji tuiboreshe kimenejimenti na kiuwezesaji ili iwe ni kampuni yetu ya kimkakati, ni lazima na sisi kama Serikali tuwe na kampuni yetu ya kimkakati ya mawasiliano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili sisi kama Wizara na tukumbuke kwamba Waheshimiwa Wabunge sasa hivi sisi Wizara yetu ina miezi mitano tu, lakini hili na sisi tumelichukulia kwa uzito ambao unastahili. Tumeshakaa na wenzetu wa *TTCL* wameandika andiko lao la mahitaji yao na tumeshalipokea na tumeshalipitia na tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, ili kuangalia huo mkakati wa kibiashara ambao wanataka kuja nao jinsi gani sisi kama Serikali tutakwenda *kuwa-support*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeanza kufanya mapitio ya sheria ili kuhakikisha sasa na hili shirika letu ambalo linajiendesha kibiashara kuna sheria nyingi ambazo zinatukwaza. Kwa hiyo, mambo hayo mengine kwa mfano shirika letu sasa hivi haliruhusiwi kununua minara ambayo imetumika. Kwa hiyo, nayo tunataka kwenda kufanya mabadiliko ya sheria za manunuzi, ili tuwaruhusu kuweza kufanya manunuzi ya minara ambayo imetumika ama vitu vingine na kurahisisha utoaji huduma zao kama wanavyoweza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba tu kuna maboresho makubwa sana tunakwenda kuyafanya katika nyanja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la *digital taxes* na hili nilishawahi kulisema lakini nadhani ilitafsiriwa vibaya, lengo letu sio sisi kuja kuweka kodi kwenye *Whatsaps, Instagram na twitter* huko siko. Lengo letu wale wakubwa sisi tunatumia mitandao hii bure, wanaotengeneza ni wale wakubwa ambao wanapata fedha nyingi za matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni sisi tuwafikie wale sio mlaji huyu wa mwisho ambaye anakuja anatomia *Instagram, Twitter na Facebook*. Kwa hiyo, sisi tunajiangalia jinsi gani ya *ku-analyze potential ya digital taxes* kule badala ya kumbana mtumiaji huyu mmoja mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili nilitaka nalo niliseme, lakini sambamba na hilo tunakwenda kufanya maboresho ya sheria ya kulinda faragha za watu. Tuna *data* nyingi *tunazi-generates* unapotumia mitandao hii hii unapokwenda sehemu mbalimbali, kuna taarifa nyingi sana za kwako ziko pale zinaeleaelea.

Kwa hiyo, tunakwenda kutengeneza sheria mpya ya data *privacy* na data *protection* lengo sio kuminya uhuru wa watu, lengo ni kukulinda wewe taarifa zako ambazo zinauzwa huko duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo tutakwenda kuwekeza katika *innovation hub* natamani kuona miaka mitano ijayo Tanzania na sisi tunakuwa *seal convert* vijana wabunifu, *sectoral developers*, masuala ya *cyber security, internet of things, block chain technology, artificial intelligence*, tunajenga *capacity* ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tunatambua jambo hili la uhalifu wa mitandao na usajili wa *online* tunakwenda kuboresha mifumo na hiyo tarehe 26,

tutakaa na Mawaziri wenzangu tuangalie njia bora zaidi ya kuangalia jinsi gani tunaweza kubana katika usajili huu wa *line* za simu. Ikiwa ni pamoja tunaweza tukaja na zoezi tena jipya la uhakiki wa watu wote ambao wamejisajili kwa njia ya *biometric*, ili kuhakikisha kwamba ni watu ambao wana kadi za simu wote wamesajiliwa na tunaweza kuweka mifumo ya kuweza kuwabaini. Na teknolojia tunayo ya kuangalia jinsi gani na kuweza *kuzi-block* hizo simu ambazo zinaweza kuwa zinatumiwa kwa njia ya kiuhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimejielekeza zaidi katika kutoa elimu zaidi kuliko kuwaadhibu kwasababu, nimeona kwamba watu wengi hatujui sheria, watu wengi hatujui haki zetu, watu wengi hatujui matumizi sahihi ya mitandao. Kwa hiyo, na mimi nataka kama Waziri kujielekeza katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri niwahakikishieni yote haya ambayo mnayasema tunaenda kuyafanyia kazi na kuweka mipango mikakati ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na Tanzania ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI**

Kifungu 1001 – *Administration and Human  
Resource Management ... ..* Sh.1,761,855,700

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa hapa ndio kwenye mshahara wa Waziri na wengi mlisema mtaukamata mshahara wa Waziri lakini hapa naona orodha ya watu watatu tu. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli yamejitosheleza sana hoja yangu ameifikia kwa hiyo, namtakia kila la kheri katika utekelezaji tunamuomba aendelee na ujasiri na uchapakazi huo huo ili Taifa liweze kunufaika. (*Makoff*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sera yetu ya Taifa ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yaani *National Information and Communication Technology Policy*, inaelekeza kuwa lazima kuwepo kwa huduma za mtandao zenye uhakika, unafuu pamoja na *speed* nchini kote Tanzania. Yaani *availability and accessibility of reliable and affordable broad per services countrywide*. Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Tanzania hususani watumiaji wa mtandao wa *internet* ambao ni takribani milioni 29 wamekuwa wakighafilika na masuala mbalimbali katika matumizi ya mtandao wa *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, huduma za *data* zimekuwa zikipandishwa gharama mara kwa mara bila ushirikishwaji. Lakini pili huduma za *data* zimekuwa zikitolewa



pasipo kuzingatia *speed* na hela ambayo inalinda thamani ya mlaji. Lakini tatu, kumekuwa kuna matamko ya mara kwa mara yanayovuruga biashara ya kimtandao kama mtakumbuka suala za *line* za wale wasajili wa *line* za simu. Lakini masuala haya yote yamekuwa *yakiwa-resolved* kwa matamka tu ya hapa kwa hapa sasa, naomba kupata maelezo kwa Waziri kwamba, Serikali imejipanga vipi kuwa na mkakati wa kudumu ambao hauangalii tu matamko ya hapa kwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kudumu ambao utalinda huduma za kimtandao na kumlinda mlaji kutokupandishiwa gharama lakini vile vile italinda *speed* za mitandao. Tunataka mkakati wa kudumu Serikali inatuambia nini na tunaona kwamba matamko ya mara kwa mara hayaleti tija kwasababu matatizo yanakuwa yanajiongeza mara kwa mara. Naomba maelezo hayo Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Judith Kapinga Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sisi kama Wizara nilivyosema hapo awali, sisi tuna miezi kama mitano na tumejaribu sana kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi. Moja ya kitu ambacho tumekifanya kama Wizara, ni kutengeneza kitu inaitwa *National Broadband Strategy* na hii sasa ndio inaweka mkakati wa muda mrefu wa nini tunaenda kukifanya kama Serikali na niliigusia pale kusudio letu tufike kilometa zaidi ya 15,000 tuko kilometa ngapi sasa hivi mwakani tunajenga kilometa ngapi. Na lengo ni kuhakikisha kwamba mkongo wa Taifa tunazidi kuusogeza karibu na wananchi ili huduma za mawasiliano ziwe nafuu zaidi na tunataka sasa twende tupanue hata wigo wa zile *submarine cables* ambazo tunazo ndani ya nchi. Wenzetu Kenya wana zaidi ya tano nazo tuwaalike wadau wengine waje wawekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho nimekielekeza sasa hivi ambacho ninakifanya ni hicho ambacho Mheshimiwa Mwinjuma alikigusia, ni jinsi gani tunaweza tukasogeza mawasiliano kwa karibu zaidi kwa kutumia njia mbadala ya gharama nafuu. Tunatambua kwa mfano, mradi wa *REA* umeweza kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali lakini tunaweza tukatumia hizo hizo *poles* za umeme na sisi kuweza kusambaza huduma zetu za *internet*. Kwa hiyo, tunajaribu kuangalia njia gani rahisi tuweze kufikia yale yale malengo kwa gharama nyingine nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hii nyanja ya kujaribu kumlinda mteja ndio maana nimesema sasa hivi tunafanya maboresho makubwa sana ndani ya *TCRA*, kuhakikisha kwamba sasa hivi afanye kazi ya udhibiti sio polisi wa sekta ambaye kazi yake yeye ni kuadhibu, kazi yake anatakiwa kulea na kuhakikisha kwamba sekta inalindwa, sekta inakua, watumiaji wanalindwa. Lakini tunaimarisha taasisi nyingine ambayo inawezekana Wabunge wengine hamujui ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa sheria inaitwa *TCRCCC* hii ni *Consultative Council* ni taasisi ya walaji na watumiaji wa sekta ya mawasiliano, tunataka nayo tuiimarisha ili ichukue nafasi yake kuhakikisha kwamba inakuwa ni *caution* kati ya watoa huduma pamoja na mamlaka ili kuhakikisha kulinda haki za walaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuombe tu unirudishie hiyo shilingi ili sasa hii bajeti tukiipitisha ndio haya mambo makubwa ambayo tunakwenda kuyafanya. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na itakumbukwa kwamba tunatambua tuko kwenye awamu ya tatu na ya mwisho ya mpango wa miaka mitano mitano ya maendeleo na *actually* kila tukifanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo tunaipanga kwenye Bunge hili, kumekuwa na ucheleweshwaji na kutokupelekwa kwa bajeti zetu kadri

ambavyo Bunge hili linavyotaka kwenye miradi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tulizungumza humu ndani na imekuwa ikizungumzwa *before* kwamba, tunahitaji kuwa na vyanzo vya mapato vingi vya kutosha ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunaisaidia Serikali kwa namna nzuri ili Serikali iweze kupeleka pesa za kutosha kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *in the spirit* sasa ya *digital economy* tuna sehemu nyingine ya kupata mapato ambayo imeonekana. Sasa Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba ndio wanafanya *evaluation* kwenye *e-economy*. Ni kitu kizuri pamoja naweza kusema tu *we are lagging behind* kwasababu, wakati *Kenyan's* juzi wame-*introduce* kodi mpya ambayo inaitwa *digital services tax*, ambayo inasaidia sasa kwenye watu wanaotoa huduma kwenye mitandao. Lakini Serikali inapata kodi lakini na hao wanakuwa *regulated* kwa sababu wanatambulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka *commitment* ya Waziri ni kwa namna gani sasa yuko tayari yeye kama mkuu wa *segment* hii sasa ya Teknohama kwenye nchi, kushauri sasa Waziri wa Fedha na mamlaka za makusanyo ya kodi kwenye nchi kuangalia sasa kwa upekee wake, namna ambavyo tunaweza tukatengeneza pesa ili wananchi wetu wakapate miradi ya maendeleo. Wakapelekewe maji, tukapate barabara, tukatengeneze pesa nyingi ambazo tunaweza kuzipata huku kwa sababu dunia inakwenda kwenye *digital* yaani *the world is digitalized*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatuwezi tukaendelea kutegemea kodi ndogo ndogo kukata walimu, kukata watu ambao kimsingi tunawanyonya zaidi, wakati kuna watu wanafanya biashara kubwa na kwa sababu hatujafanya *evaluation* ya *e-commerce* hatujui kiasi gani tunatengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata Kenya leo wanafanya *aggregate* ndio maana wanaweza hata sisi

kukosa pesa ambazo Diamond anazipeleka Kenya kupitia *ngoma accn* kwasababu, hatukufanya *evaluation* mapema ya *e-commerce* ili tujue *social media* zetu zinaweza kutengeneza pesa kiasi gani. Kwa hiyo, nataka *commitment* ya Serikali namna gani ambapo... (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ya Serikali ipo, ukiangalia katika bajeti hii mwaka jana 2020 bajeti ya maendeleo ya Wizara hii ama sekta hii ilikuwa ni bilioni 11, ukiangalia bajeti ambayo tunakwenda kuipitisha ni bilioni 211 imeongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Lakini sambamba na hilo kitu mkitupitishia bajeti hii jambo lingine ambalo tunaenda kuliangalia ni kwenda kuongeza vyanzo vya mapato, kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya mkongo wa Taifa na kuhakikisha kwamba mawasiliano yanafika katika maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba Kenya wamepiga hatua lakini wanasema kawia ufike na sisi Wizara yetu ni changa lakini na sisi tunakimbia kweli kweli kuhakikisha kwamba yale mambo yote ya msingi ambayo wenzetu wamefikia kule kuanzisha hiyo *digital economy strategy, national broad band strategy, national cyber security strategy* yote haya tumeweza kuyafanya ndani ya muda mfupi kuhakikisha kwamba na sisi *tuna-catch up* katika eneo hilo. Lakini nikupe *commitment* kwamba sisi na Wizara ya Fedha tutakaa tunaongea na timu zetu za wataalam wameshaanza kukaa na kuongea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tuna Waziri wa Fedha muelewa sana na timu zangu hivi tunavyoongea timu zangu za wataalam wameanza kukaa na Wizara ya Fedha,

kuangalia *potential* ambazo ziko katika sekta hii na jinsi gani tunaweza *tukazi-nature* na kuzihakikisha kwamba *zina-grow* kuhakikisha kwamba Serikali nayo inakuja kupata mapato makubwa kupitia sekta hii.

Kwa hiyo, nitoe hiyo *commitment* kwamba tunafanya kazi kwa karibu. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> ... ..	Sh.410,982,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> ... ..	Sh.495,389,040
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> ... ..	Sh.165,528,400
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i> ... ..	Sh.151,999,604
Kifungu 1006 – <i>Government Communication Unit</i> ... ..	Sh.150,225,300
Kifungu 1007 – <i>Procurement Management Unit</i> ... ..	Sh. 282,375,900
Kifungu 2001 – <i>Communication Division</i> ... ..	Sh.747,480,656
Kifungu 2002 – <i>Information, Communication and Technology</i> ... ..	Sh.818,933,400

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## KITABU CHA NNE

### MIPANGO YA MAENDELEO

#### FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

Kifungu 2001 – <i>Communication Division</i> ... ..	Sh.45,000,000,000
Kifungu 2002 – <i>Information, Communication and Technology</i> ... ..	Sh.166,399,781,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lillirejea)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa hoja.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati na kupitia kifungu kwa kifungu Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yenye jumla ya shilingi 216,384,551,000.00 imepitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
(Hoja imeamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji, kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022.  
*(Makofi)*

Ahsanteni, Mheshimiwa Waziri na Naibu hongereni sana kwa kazi nzuri mliyofanya na watalaam, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa *TTCL, TCRA* na wengine wote wa Mfuko wa

Mawasiliano, Watendaji wote mmefanya kazi nzuri sana na mnastahili pongezi. Mmeona bajeti yenu imepita bila hakuna hata mtu mmoja aliyesema siyo kwa hiyo wote wameipitisha, kikubwa mkafanye kazi. (Makofi)

Kikubwa na ninyi *m-concentrate* na *cybercrimes* mtizame namna gani nchi iweze kulindwa na hasa kwenye maeneo ambayo kuna *privilege* ya mapato, kuna *traffic* kama zipo ambazo za simu hamzi-*monitor* mzikamate na muhakikishe Serikali inapata mapato yake stahiki. (Makofi)

Baada ya maneno haya nikushukuru *Chief Whip* na Msimamizi Mkuu wa Serikali Bungeni kwa kazi nzuri mliyoifanya. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. (Makofi)

(Saa 1.18 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 20 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)